**BUNGE LA TANZANIA**

---

# MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA KUMI NA TISA

**Kikao cha Nane – Tarehe 17 Aprili, 2025**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Naibu Spika (Mhe. Mussa A. Zungu) Alisoma Dua*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tukae.

Katibu.

**NDG. MICHAEL CHIKOKOTO, *ndc* – KATIBU MEZANI:**

## MASWALI NA MAJIBU

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, maswali, tutaanza na Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Anastazia James Wambura.

Na. 96

**Idadi ya Walimu Waliohama na Kuhamia Mkoa wa Mtwara**

**MHE. ANASTAZIA J. WAMBURA** aliuliza:-

Je, kwa nini idadi ya walimu wa shule za msingi na sekondari waliohama kutoka Mkoa wa Mtwara Julai, 2023 – Juni, 2024 ni 318 na waliohamia ni 113?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa uchambuzi wa maombi ya uhamisho, sababu nyingi za uhamisho ambazo zimekuwa zikiainishwa na waombaji ni pamoja na kusogea karibu na huduma za matibabu na kufuata familia. Kutokana na mazingira hayo, Ofisi ya Rais, TAMISEMI imekuwa ikifanya uchambuzi wa maombi hayo na kutoa vibali vya uhamisho kulingana na uzito wa changamoto. Aidha, vibali vya uhamisho vimekuwa vikitolewa kwa kuzingatia matakwa ya Kanuni ya 106 ya Kanuni za Utumishi wa Umma za mwaka 2022.

Mheshimiwa Naibu Spika, tofauti ya idadi ya watumishi waliohama na waliohamia katika halmashauri za Mkoa wa Mtwara inatokana na misingi ya sheria inayotumika katika utoaji wa vibali vya uhamisho. Aidha, Serikali imeendelea kuajiri na kupeleka walimu katika Mkoa wa Mtwara, ambapo katika ajira ya mwaka 2023/2024, halmashauri za Mkoa wa Mtwara zilipelekewa walimu 329.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itaendelea kuajiri wataalam katika Sekta ya Elimu na kuwapanga kwenye halmashauri zenye uhaba zaidi katika Mkoa wa Mtwara.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Wambura.

**MHE. ANASTAZIA J. WAMBURA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza. Nishukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri ambapo tumeweza kuletewa walimu idadi hiyo aliyoitaja.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza; kule Mtwara kuna tatizo kubwa sana, kwamba wale walimu ambao wanatakiwa kuhamia kule kwa ajili ya kujaza zile nafasi za waliohama hawafiki na muhanga mkubwa ni Halmashauri ya Newala *DC*. Je, ni lini Serikali itawaleta walimu wale ambao walitakiwa kuja kujaza zile nafasi za waliohama?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; ni kweli huwezi ukamlazimisha mtu kuhamia sehemu, lakini kuna tatizo kubwa katika mikoa ya pembezoni, wilaya za pembezoni na kata za pembezoni. Kimsingi ukiweka vivutio kwa vyovyote vile mtu anaweza akavutiwa kuhamia pale hata kama alikuwa hataki kuhamia. Je, ni lini Serikali sasa itahakikisha kwamba inaweka vivutio katika ile mikoa ya pembezoni, wilaya za pembezoni na kata za pembezoni ili wale wanaotakiwa kuhamia kule kuziba nafasi au kuhamia kule kwa namna yoyote ile waweze kuvutiwa na kushawishika kuhamia kule na wengine wasishawishike kuhama?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nianze kumpongeza Mheshimiwa Anastazia Wambura kwa kupaza sauti yake kuwazungumzia walimu na kutaka kuona kwamba Sekta ya Elimu inafanya vizuri na wanafunzi wetu wanapata walimu wa kutosha wa kuwafundisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na swali lake la kwanza, ninaomba, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali inaendelea kuajiri walimu na pia kufanya msawazo wa walimu kwa kuwatoa katika maeneo ambayo yana walimu wengi zaidi na kuwapeleka kwenye maeneo ambayo yana upungufu mkubwa. Kwa hiyo tunafahamu kuwa kuna upungufu wa walimu katika wilaya aliyoitaja na Serikali itahakikisha kwamba inaleta walimu kwa ajili ya kupunguza upungufu uliopo katika eneo husika.

Mheshimiwa Naibu Spika kuhusiana na swali lake la pili, Serikali ya Awamu ya Sita imefanya uwekezaji mkubwa sana katika Sekta ya Elimu ambapo zaidi ya trilioni 5.1 zimewekezwa katika Sekta ya Elimu msingi na elimu sekondari. Fedha hizi nyingi zimetumika kwa ajili ya kuboresha miundombinu ikiwemo nyumba za walimu. Nyumba hizi za walimu zinajengwa katika maeneo ya pembezoni ikiwa ni sehemu mojawapo ya kuboresha mazingira ya kazi na kupunguza yale mahitaji ya walimu kuona mazingira ni

magumu wanapokuwa wamepangwa kwenye maeneo ya pembezoni na kutaka kuhama.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile Serikali hii ya Awamu ya Sita imefanya uwekezaji mkubwa sana katika kuboresha huduma za msingi za kijamii, ndiyo maana utaona kuwa umeme unapelekwa mpaka vijijini, utaona huduma za maji zinaboreshwa, pamoja na huduma nyingine muhimu kama vile za afya na kadhalika. Kwa hiyo Serikali inatambua kwamba kuna baadhi ya walimu ambao kutokana na mazingira ya kuwa pembezoni wanataka kuhamia katika maeneo ya mjini na ndiyo maana Serikali inaboresha mazingira katika maeneo ya pembezoni ili walimu wapate sehemu nzuri ya kuendelea kufanya kazi zao na wasihame.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo Serikali itaendelea na jitihada hizo, itaendelea kujenga nyumba za walimu na kutengeneza motisha mbalimbali ambazo zitawafanya walimu wasihame kutoka kwenye maeneo ya pembezoni.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea Mheshimiwa Michael Kembaki, kwa niaba yake Mheshimiwa Neema.

Na. 97

**Ujenzi wa Barabara ya Kebaga - Tarime Mjini**

**MHE. NEEMA K. LUGANGIRA K.n.y. MHE. MICHAEL M. KEMBAKI** aliuliza:-

Je, lini Barabara ya Kibaga itajengwa kwa kiwango cha changarawe ili kuondoa kero ya watumiaji Tarime Mjini?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2023/2024, Serikali ilitumia shilingi 39.4 kufanya matengenezo ya kilomita mbili katika Barabara ya Kibaga kwa kiwango cha changarawe na matengenezo ya kawaida kilomita nne. Utekelezaji wa kazi hii umefikia 70% na mkandarasi yuko *site* anaendelea na kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itaendelea kuihudumia na kuiboresha barabara hii kwa kuijenga kwa tabaka la changarawe kulingana na upatikanaji wa fedha.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Neema.

**MHE. NEEMA K. LUGANGIRA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nina maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Michael Kembaki. Swali la kwanza; wakandarasi wamekuwa wakikimbia au kutokamilisha kazi za *tender* zao; je, ni hatua zipi zinachukuliwa na Serikali?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; je, Barabara ya Tarime – Nyamaga itaanza kujengwa lini?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nianze kujibu swali la kwanza la Mheshimiwa Mbunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, dhamira ya Serikali ya Awamu ya Sita ni kuboresha miundombinu ya barabara na hasa hizi barabara za wilaya zinazosimamiwa na *TARURA* na ndiyo maana katika kipindi cha Serikali hii ya Awamu ya Sita tutaona ongezeko kubwa la bajeti ya *TARURA* kutoka bilioni 275 kwa mwaka mpaka bilioni 710 kwa mwaka. Kwa hiyo, katika dhamira hiyo Serikali inakusudia pia kuwawezesha wakandarasi wazawa ili wapate nafasi ya ujenzi wa barabara hizi, ili wapate kandarasi kwa ajili ya kujenga barabara hizi za *TARURA*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo nitumie nafasi hii kutoa wito kwa wakandarasi wazawa wanaopatiwa kazi za ujenzi wa barabara hizi muhimu kabisa kwa Uchumi na kwa Watanzania kufikia huduma za muhimu za kijamii waweze kutimiza majukumu yao kimkataba. Wale wakandarasi ambao hawatimizi wajibu wao kimkataba watachukuliwa hatua kwa kufuata misingi ya kisheria.

Mheshimiwa Naibu Spika kuhusiana na swali la pili la Mheshimiwa Mbunge, Serikali itaendelea kufika katika maeneo mbalimbali ili kuongeza mtandao wa barabara hizi za *TARURA* na kuzipandisha hadhi mpaka zifikie katika hadhi ya lami. Kwa hiyo, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kuwa Serikali itafika katika barabara hii aliyoitaja kwa ajili ya kuijenga iwe katika hadhi nzuri iweze kuwanufaisha wananchi.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea; swali namba 98 Mheshimiwa George ameliondoa, amekwishatoa taarifa rasmi. Tunakwenda kwenye swali namba 99, Mheshimiwa Kisangi kwa niaba yake Mheshimiwa Minza.

**MHE. MINZA S. MJIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika mimi niliomba tu swali la nyongeza.

**MHE. JANEJELLY J. NTATE:** Mheshimiwa Naibu Spika kwa niaba ya Mheshimiwa Mariam Kisangi…

**NAIBU SPIKA:** Ngojeni kwanza, nimemwita Minza wewe umeingia yule kakaa wewe umesimama haya simama wewe sasa uliyesimama.

Na. 99

**Hitaji la watumishi Kituo cha Afya Kilakala - Temeke**

**MHE. JANEJELLY J. NTATE K.n.y. MHE. MARIAM N. KISANGI** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kupeleka watumishi katika Kituo cha Afya Kilakala Manispaa ya Temeke?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeendelea kuajiri watumishi wa kada ya afya na kuwapeleka kwenye vituo vya kutolea huduma za afya kote nchini. Katika Mwaka wa Fedha 2023/2024, jumla ya watumishi 9,384 waliajiriwa na kupangiwa kazi katika vituo vya kutolea huduma katika halmashauri, ambapo watumishi wa afya 69 walipangwa katika Manispaa ya Temeke na watumishi watatu katika Kituo cha Afya Kilakala.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na ajira kutoka Serikali kuu, Manispaa ya Temeke imeajiri kwa mkataba watumishi watatu na kuwapangia majukumu katika Kituo cha Afya Kilakala ambacho kina jumla ya watumishi 19 kati ya 35 wanaohitajika. Serikali itaendelea kutoa vibali vya ajira kwa kada za afya na kuwapanga katika halmashauri zenye upungufu kote nchini.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Janejelly.

**MHE. JANEJELLY J. NTATE:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Serikali na juhudi wanazofanya, ukiangalia jiografia ya pale bado kuna upungufu wa watumishi. Swali la kwanza; je, Serikali watafanya mkakati gani wa kuendelea kuwaongezea watumishi?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; hili suala liko kwa nchi nzima na tunajua wanaendelea kuajiri. Je, wamejipangaje katika kufanya msawazo ulio sahihi maana unakuta vituo vingine vina watumishi wengi, vituo vingine havina watumishi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba Kituo cha Afya cha Kilakala bado kina upungufu wa watumishi. Serikali katika kila kibali cha ajira katika kila mwaka wa fedha imeendelea kupeleka watumishi katika Halmashauri ya Manispaa ya Temeke. Nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba katika kila ajira zitafuata tutaendelea kupeleka watumishi katika vituo hivi vyenye upungufu wa watumishi ili waweze kutoa huduma bora zaidi kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie pia nafasi hii kumpongeza Mkurugenzi wa Manispaa ya Temeke kwa kutumia fedha za mapato ya ndani kuajiri watumishi. Nitoe wito kwa Wakurugenzi wa Halmashauri kote nchini kutumia fedha za mapato ya ndani kwa ajili ya kuajiri watumishi kwenye vituo vya huduma za afya pia hata walimu kwa sababu mwongozo wa kuajiri watumishi hao kwa mkataba umetolewa; na ni wajibu wa mapato ya ndani pia kulipa watumishi wa mkataba wakati wanasubiri ajira kutoka Serikali Kuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, tunafahamu kwamba kuna utofauti wa idadi ya watumishi kutoka kituo kimoja kwenda kingine na hususan katika maeneo ya vijijini ambako kuna upungufu mkubwa zaidi. Ndiyo maana katika ajira zetu zote kuanzia mwaka 2021/2022 zinazotolewa hutolewa kwa idadi kulingana na upungufu wa watumishi katika maeneo hayo. Serikali imeainisha mikoa yenye upungufu mkubwa zaidi na halmashauri zenye upungufu mkubwa zaidi pia vituo vyenye upungufu mkubwa zaidi na vinapewa kipaumbele na zoezi hili ni endelevu.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Minza.

**MHE. MINZA S. MJIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Mkoa wa Simiyu una changamoto kubwa sana ya watumishi wa afya. Je, ni lini Serikali italeta watumishi wa kutoka katika vituo vya afya?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoa wa Simiyu ni miongoni mwa mikoa 10 ambayo Ofisi ya Rais TAMISEMI imeiainisha ikiwa na upungufu mkubwa zaidi wa watumishi. Katika ajira zote ambazo zimekuwa zikitolewa na Serikali tumewapa kipaumbele cha hali ya juu zaidi mikoa hii 10 na kupeleka watumishi wengi zaidi. Kwa hiyo ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na Waheshimiwa Wabunge wote kutoka katika mikoa hiyo yenye upungufu mkubwa zaidi wa watumishi kuwa Serikali imeweka kipaumbele na kila ajira zikijitokeza watumishi wengi zaidi watapelekwa kwenye mikoa yenye upungufu mkubwa zaidi kuliko ile ambayo angalau ina hali nzuri ya watumishi. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Anatropia.

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Wilaya ya Kyerwa kama wilaya nyingine za mpakani pia zina changamoto ya watumishi wa afya na ina wastani wa watumishi watatu mpaka watano kwenye vituo. Ninataka kujua mkakati wa Serikali wa kuongeza idadi ya watumishi kwa kuwavutia ili waweze kupenda kukaa kwenye maeneo ambayo ni pembezoni?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba Wilaya ya Kyerwa ni moja ya halmashauri zenye upungufu wa watumishi. Serikali imeendelea kupeleka watumishi wa kada ya afya na kuwapangia kwenye vituo mbalimbali. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, katika vibali vya ajira vinavyofuata kwanza tutaendelea kutoa kipaumbele kwa Halmashauri ya Kyerwa na nyingine zenye upungufu kama hiyo na pili tumeendelea kujenga mazingira bora ya kuwezesha watumishi katika halmashauri zetu za vijijini kuweza kukaa na kufanya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, moja ya hatua ambayo tumechukua ni kujenga nyumba bora za watumishi ambazo katika Halmashauri ya Kyerwa pia tumeendelea kujenga nyumba za madaktari na wauguzi. Tutaendelea kujenga nyumba hizo pia kuboresha mafao yao, kwa maana ya fedha za saa za ziada *(on call allowance)* ili watumishi wale waweze kufurahia kazi hizo na waweze kudumu katika maeneo hayo pia.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri bado gharama za hospitali zinawasumbua wananchi wengi. Utakuta kuna mgonjwa yuko hospitali amelazwa anafanyiwa Dialysis, tiba ambayo ina gharama na wananchi wanachanga, ndugu zake wanachanga. Siku wakikosa kuchanga, siku wakiishiwa yule afanyiwi Dialysis; na ugonjwa huu bila kufanyiwa zoezi la kusafishwa damu kila siku ni hatari sana. Sasa mtu amekuwa *admitted,* yuko kitandani hospitali, wauguzi na madaktari wanapita wanamvuka sababu tu hana pesa ya kuchangia siku hiyo.

Hili jambo naomba mlitazame vizuri muwe na utu. Hospitali hizi ni za Serikali, mishahara inalipwa na Serikali, umeme unalipwa na Serikali, vifaa vinanunuliwa na Serikali na wananchi ni wa Serikali. Niwaombe sana wapeni taarifa huko kwamba wawe na utu kidogo, si kila mtu anakuwa na uwezo wa fedha. Kuna kesi za kawaida kabisa hata pale Muhimbili, watu wanalazwa, wanafanyiwa Dialysis lakini siku akishindwa kulipa hafanyiwi. *This is very bad.* Jibu basi umepokea? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, suala hili nimelipokea ni la ngazi ya Wizara ya Afya, lakini tutawasiliana kama Serikali ili tuweze kuona namna ambavyo Wizara ya Afya itaboresha utaratibu huo. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Nishati, Mheshimiwa Tarimba.

**MHE. TARIMBA G. ABBAS:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nikupongeze kuliamsha suala la utu katika matibabu.

Na. 100

**Kusambaza Gesi ya Kupikia Majumbani Kinondoni**

**MHE. TARIMBA G. ABBAS** aliuliza:-

Je, Serikali imefikia wapi katika mradi wa kusambaza gesi ya kupikia majumbani Wilayani Kinondoni?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII K.n.y. WAZIRI WA NISHATI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Wilaya ya Kinondoni Serikali imekwishakupeleka miundombinu ya usambazaji gesi asilia ambapo jumla ya nyumba 155 zimeunganishwa na mtandao wa matumizi ya gesi asilia katika eneo la Mikocheni. Pia Serikali kupitia *TPDC* ipo katika mpango wa kuunganisha nyumba zaidi ya 1,000 katika maeneo mbalimbali ya Jiji la Dar es Salaam ambapo kati ya nyumba hizo, nyumba 279 zitapatikana Wilaya ya Kinondoni.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Tarimba.

**MHE. TARIMBA G. ABBAS:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru Serikali kwa majibu yake. Nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza; mradi huu ulianza Januari, 2021; na lengo lilikuwa ni kuzifikia nyumba 170. Sasa hivi Serikali inasema imefikia nyumba 155. Je, ni lini Serikali itakwenda kumalizia mpango wake ambapo sasa ni miaka mitatu tangu mpango huo kuanza, watazifikia lini nyumba 170?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, sasa hivi gesi inapoisha mtumiaji hupelekewa *control number* na akipelekewa *control number* akilipa lazima apige tena simu *TPDC* ndiyo wamfungulie gesi. Kwa nini sasa Serikali isitumie mfumo rahisi kama ule wa *TANESCO* badala ya kuweza kutumia mfumo uliopo sasa ambao

unachelewesha sana upatikanaji wa huduma hii? Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII K.n.y. WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Tarimba kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba tumekuwa na mpango huo wa kuunganisha nyumba katika hii Wilaya ya Kinondoni, lakini wakati tunafanya zoezi hilo ikatokea kwamba maombi yakawa ni mengi. Kwa hiyo, ikaonekana ni busara *TPDC* iingie makubaliano na Kampuni ya *Taqa Dalbit* kwa ajili ya kufanya utafiti ili kupata mahitaji halisi ya wanaohitaji kuunganishiwa gesi katika nyumba zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kupitia upya vilevile ule mfumo au maeneo ambayo mabomba ya kusambaza gesi yanaweza kupitishwa na hili limesababisha kasi ya kupeleka gesi katika maeneo hayo kupungua, lakini kwa sababu tumekwishajipanga sasa, nimhakikishie kasi hii itaongezeka. Ndani ya kipindi kifupi Mheshimiwa Tarimba ataona jinsi ambavyo mradi huu utakamilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na eneo la pili ambalo amezungumzia ucheleweshaji wa huduma kutokana na mfumo, ni kweli tumepata malalamiko haya kutoka kwa wateja wetu na timu yetu ya wataalam ipo kazini kuona jinsi ambavyo tunaweza kuja na mfumo ambao utakuwa umetibu changamoto hii. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Komanya.

**MHE. LEAH J. KOMANYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru. Kwa kuwa mitungi iliyowekewa ruzuku ambayo inatolewa katika Jimbo la Meatu kwa bei ya shilingi 20,000 inazingatia Kitambulisho cha *NIDA* hivyo kunufaisha kaya chache. Je, Serikali haioni haja ya kutumia ugawaji wa mitungi hii kwa

kaya ili kaya nyingi ziweze kunufaika na wananchi wengi waweze kunufaika kama yalivyo matarajio ya Mheshimiwa Rais badala ya ile kutumia *NIDA*, kaya moja inajikuta inachukua mtungi mmoja hadi mitungi mitano? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII K.n.y. WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kujibu swali moja la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge. Tumepokea ushauri tutaenda kuufanyia kazi. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Hokororo.

**MHE. AGNES E. HOKORORO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru. Je, Serikali haioni iko haja ya kuunganisha gesi ya majumbani katika maeneo ya Mtwara Mjini na Vijijini ambao hasa ni walinzi wa rasilimali hiyo? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII K.n.y. WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kujibu swali moja la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeona ipo haja ndiyo maana tumeanza na Mradi wa Kuunganisha Gesi Majumbani kwenye eneo la Mtwara tutakwenda hatua kwa hatua ili tuweze kuwafikia wateja wengi zaidi.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea Wizara ya Elimu, Mheshimiwa Shigongo.

Na. 101

**Fedha za Ujenzi Chuo cha Ufundi Kayenze Buchosa**

**MHE. ERIC J. SHIGONGO** aliuliza:-

Je, fedha kiasi gani kimepelekwa kwenye ujenzi wa Chuo cha Ufundi Kayenze – Buchosa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Chuo cha *VETA* cha Wilaya ya Sengerema kinachojengwa katika Kata ya Kayenze, Halmashauri ya Wilaya ya Buchosa ni miongoni mwa Vyuo 64 vya *VETA* vya Wilaya na kimoja cha Mkoa wa Songwe vinavyojengwa na Serikali katika wilaya ambazo zilikuwa hazina Vyuo vya Ufundi Stadi. Hadi sasa Serikali imeshatumia jumla ya shilingi 932,016,616.81 kwa ajili ya ujenzi wa chuo hicho. Aidha, ujenzi wa Chuo hiki unatarajia kugharimu kiasi cha shilingi bilioni 1.6 kwa majengo yaliyopangwa kujengwa katika awamu ya kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itaendelea kupeleka fedha ili ujenzi wa chuo hiki uweze kukamilika na kuanza kutoa mafunzo kama ilivyopangwa. Ninakushukuru sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa James.

**MHE. ERIC J. SHIGONGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru sana kwa majibu mazuri na sahihi ya Serikali, lakini ninayo maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; kwa kuwa wananchi wa Buchosa wamejipanga kwa ajili ya kusoma katika chuo hiki na hawajawahi kuwa na chuo tangu uhuru wa nchi yetu: je, Serikali inaweza kutamka ni lini chuo hiki kitakamilika kwa mujibu wa mpango wake? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; kujenga chuo ni jambo moja lakini kuwa na wataalam wa kufundisha watu wetu ili wapate maarifa ya kukabiliana na dunia ni jambo la pili muhimu zaidi. Je, Serikali imejipangaje kwa mujibu wa mitaala na walimu ili kuweza kuwafundisha watoto wetu *digital economy* ili waweze kukabiliana na ulimwengu ujao? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kipekee nichukue fursa hii kwanza kumpongeza sana Mheshimiwa Shigongo amekuwa akikifuatilia chuo hiki kwa muda mrefu na mara kadhaa ameniomba niweze kufanya ziara katika eneo hili ili kuweza kuona ujenzi jinsi unavyoendelea. Nimwahidi tu Mheshimiwa Shigongo baada ya hizi Shughuli za Bunge tutapanga utaratibu namna gani tunaweza kwenda kwenye chuo hiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo haya sasa ninaomba nijibu maswali mawili ya Mheshimiwa Shigongo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la kwanza kuhusiana na suala la utekelezaji wa mradi kwamba lini utakamilika? Kulingana na programu tuliyokuwa nayo hivi sasa tunatarajia kukamilisha ujenzi ule katika mwezi Agosti, 2025 ili itakapofika mwezi wa Oktoba mafunzo yale ya muda mfupi yaweze kuanza kutolewa katika eneo hili au katika chuo hiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika eneo la pili, kuhusu mikakati ya Serikali ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, tunafahamu kwamba tunajenga vyuo hivi, vyuo 64 katika wilaya 64 na chuo kimoja cha Mkoa wa Songwe. Ni idadi kubwa ambayo haijawahi kujengwa tumpongeze sana Mheshimiwa Rais. Mikakati ya Serikali ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la kwanza, Chuo chetu cha Ualimu wa Ufundi pale Morogoro tumekiongezea majengo kwa maana idadi ya mabweni pamoja na madarasa na hivi sasa kinaweza kikachukua wanafunzi wa mwaka wa kwanza kwa pamoja zaidi ya 160 ambao watakuwa wanalala pale pale shuleni. Kwa hiyo, huo ni mkakati wa kwanza wa kuhakikisha kwamba tunakuwa na walimu wa kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la pili vyuo vyetu vya ufundi kwa maana ya Chuo chetu cha Mbeya – *MUSTS,* Chuo chetu cha

*DIT* pale Dar es Salaam na Chuo chetu cha *ATC* kule Arusha navyo vilevile vimeanzisha programu za ualimu wa ufundi ili ku-*catch up* kulingana na programu zitakazokuwa zinatolewa katika vyuo vyetu hivi vya *VETA*.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la tatu, tunakwenda kubadilisha vyuo vyetu viwili vya Mtwara kawaida na Mtwara Ufundi vinakuwa ni *branch* ya chuo chetu cha Mbeya ili kuhakikisha kwamba vyuo hivi vitazalisha walimu wa ufundi ili kuweza kuhakikisha kwamba vyuo vyetu hivi vinapata walimu wa kutosha. Ninakushukuru sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Chaya.

**MHE. DKT. PIUS S. CHAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Katika Wilaya ya Manyoni tuna Ujenzi wa Chuo cha *VETA*, ambacho Serikali imeshatoa takribani shilingi milioni 412. Sasa je, ni Serikali itakamilisha ujenzi wa chuo hicho cha Wilaya ya Manyoni cha *VETA?*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Chaya anajua na alikuja wiki iliyopita ofisini pale, tukakaa tukazungumza. Kwanza fedha iliyokwenda pale Manyoni ni shilingi milioni 932 karibu katika vyuo vyote vile 64. Kwa hiyo, nimhakikishie tu na hiki Chuo cha Manyoni nacho tutahakikisha itakapofika mwezi Agosti Mheshimiwa Chaya nikuondoe wasiwasi na hapa ni karibu kabisa tutahakikisha itakapofika mwezi Agosti chuo kile cha Manyoni nacho kimekamilika katika awamu hii ya kwanza. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Nusrat, jiandae Mheshimiwa Mkundi.

**MHE. NUSRAT S. HANJE:** Mheshimiwa Naibu Spika, sisi Wilaya ya Ikungi pale kuna Chuo cha *VETA*, lakini bado mazingira ya kujifunzia na kufundishia bado kuna changamoto si katika kozi

nyingi zinazotolewa, lakini bado tunahitaji miundombinu ya kujifunzia. Sasa ni kwa nini Serikali wakati inaweka mikakati ya kujenga vyuo isifungamanishe na kuweka miundombinu ya kujifunzia na kufundishia ili tutoe vijana kwenye vyuo vya ufundi ambao wameiva ili waingie kwenye uzalishaji moja kwa moja?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nikijibu swali dogo la Mheshimiwa Nusrat ni kweli tumejenga chuo katika Wilaya ya Ikungi ni katika ile awamu ya kwanza vyuo 25 vya wilaya na vile vinne vya mikoa. Nimwondoe wasiwasi Mheshimiwa Nusrat utekelezaji wa programu mbalimbali katika vyuo hivi unakwenda kwa awamu na unatarajia au unategemea sana upatikanaji wa vifaa. Kwa hiyo, katika bajeti yetu ya mwaka huu tumeweka zaidi ya shilingi bilioni 160 kwa ajili ya ununuzi wa vifaa katika vyuo vile 25 vya wilaya na vile vyuo vinne vya mikoa. Vifaa hivi vitakavyofika ina maana programu zile nyingine zote zitakwenda kufunguka na tutaanza kufundishwa katika vyuo hivi vyote. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Mkundi.

**MHE. JOSEPH M. MKUNDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru. Niipongeze Serikali imeweka nguvu kubwa sana kujenga Vyuo vya *VETA* karibu nchi nzima ikiwemo na Jimbo la Ukerewe, lakini bado kuna mwamko mdogo sana wa jamii kuona umuhimu wa vyuo hivi na kwa hiyo kupeleka watoto wao kupata mafunzo kwenye vyuo hivi. Nini mkakati wa Serikali kuiamsha jamii ione tija na umuhimu wa kupeleka vijana hawa kwenye vyuo hivi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nikijibu swali dogo la Mheshimiwa Mkundi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi mwenyewe nimeshawahi kwenda pale Ukerewe, anachokizungumza Mheshimiwa Mbunge

ni sahihi na hii imetokea sana maeneo ya visiwani hata kule kwangu Mafia, mwitikio ni mdogo sana kwa upande wa vijana wetu, lakini nini mkakati wa Serikali?

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na Bunge lako Tukufu. Tumefanya maboresho sana ya sera pamoja na mitaala yetu kuanzia shule za msingi. Kwa hiyo, katika mitaala mipya pamoja na sera mpya inasisitiza sana masuala ya elimu ya ufundi. Bila shaka katika vijana hawa tunaoanza kuwazalisha sasa hivi, kwa vile mkondo huu wa ufundi utakuwa sasa ni *formal* moja kwa moja kutokea shule shule zetu msingi, bila shaka umma wa Watanzania watakuwa wameelewa maana ya elimu ya ufundi, lakini vilevile watavutiwa na mazingira yale ya kwenda kupeleka watoto kwa ajili ya kujifunza maeneo haya ya ufundi. Ninakushukuru sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Sanga.

**MHE. DEO K. SANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru. Kwa kuwa Serikali imetupatia fedha za kujenga shule ya ufundi katika Jimbo la Makambako, shilingi milioni 585 ni lini Serikali itatuongezea fedha kwa ajili ya kukamilisha Shule ya Ufundi Makambako? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli tumepeleka fedha katika majimbo ambayo yalikuwa hayana Vyuo vya *VETA* ambayo tunakwenda kujenga shule za ufundi zaidi ya shule 103 na katika awamu ya kwanza tumepeleka zaidi ya shilingi milioni 528. Ninaomba nimwondoe hofu Mheshimiwa Sanga, awamu hii ya mwezi huu Aprili tutapeleka fedha awamu ya pili ambayo ni zaidi ya shilingi milioni 528 tena kwa sababu shule zile zinajengwa kwa zaidi ya shilingi bilioni 1.6.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaamini kabisa katika kipindi hiki kifupi tunafanya *evaluation* ya namna gani fedha zile zilitumika

zile za awamu ya kwanza na baada ya kujiridhisha kwamba fedha zote zimetumika, tunakwenda kutoa katika awamu ya pili ili kukamilisha majengo yale ya awamu ya pili. Ninakushukuru sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea Wizara ya Maliasili, Mheshimiwa Dkt. Ishengoma.

Na. 102

**Kutangaza Maporomoko ya Vinile Kuwa Kivutio cha Utalii**

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itatangaza Maporomoko ya Vinile yaliyopo Mvomero kuwa kivutio cha utalii?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Maporomoko ya Maji ya Hululu au Vinile yanapatikana katika Hifadhi ya Msitu wa Mazingira Asilia Uluguru iliyopo Mkoani Morogoro na unasimamiwa na Wakala wa Huduma za Misitu *(TFS)*. Maporomoko hayo yenye mtiririko wa maji mengi na safi mwaka mzima tayari yanatambuliwa kama moja ya vivutio vya utalii nchini kama kinavyobainishwa katika tovuti na majarida mbalimbali. Upekee wa Maporomoko hayo unashabihishwa pia na uwepo wa vivutio vingi katika safu za Milima ya Uluguru kama vile wanyama mbalimbali, ndege, miti jamii mbalimbali, maua na miinuko ya utalii wa kupanda milima.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika jitihada za Serikali kuyatangaza na kuyatumia maporomoko hayo kiutalii, Wizara kupitia Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania imetekeleza shughuli mbalimbali za kuboresha miundombinu ya kitalii na kutangaza Hifadhi hiyo ndani na nje ya nchi. Kazi zilizofanyika ni pamoja na matengenezo ya mara kwa mara ya barabara yenye urefu wa kilometa nane kutoka Kijiji cha Kibaoni kuelekea kwenye

Maporomoko, kujenga kambi ya watalii eneo la Bunduki, kujenga ngazi za kupanda kuelekea Maporomoko hayo, kutoa mafunzo kwa waongoza watalii wenyeji (*Local tour guides*) pamoja na kukarabati nyumba ya kupumzikia watalii. Jitihada hizo zimeendelea kuzaa matunda ambapo idadi ya watalii katika hifadhi hiyo imeongezeka kutoka watalii 290 katika mwaka 2021 hadi kufikia watalii 1,453 mwaka 2024.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Ishengoma.

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa nINamshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri sana, ila nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la kwanza mpaka sasa hivi ninavyoongea miundombinu ya barabara ya kufikia pale Vinile kwa kweli siyo mizuri. Hasa kuna mahali kuna mto ambapo inatakiwa kujengwa daraja kiasi kwa sababu siyo rafiki kwa watalii kuifikia hiyo Vinile kwa mara moja hasa kwa mwaka mzima. Je, Serikali ina mpango gani wa kutengeneza hizo njia zinazokwenda kwenye vivutio vya utalii ili viweze kufikika kwa urahisi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la pili; kuna mpango mkakati gani hasa wa kutangaza utalii wa Kanda wa Pwani kama unavyotangazwa utalii wa Kanda ya Kaskazini pamoja na Kanda ya Kusini kwa sababu ukanda wa Pwani una vivutio vingi hasa ukichukua Mkoa wa Pwani, Mkoa wa Tanga, Mkoa wa Morogoro, na Mikoa yote ya Kusini ina utalii mkubwa sana? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Ishengoma, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema kwenye jibu langu la msingi, Wizara inafanya kazi kubwa ya kuhakikisha inaboresha miundombinu ya kuelekea kwenye maporomoko haya na tayari tumeshajenga kilometa nane za barabara kwenye

eneo hilo. Japokuwa matengenezo haya yanahitajika kufanyika mara kwa mara kwa sababu ni eneo la kwenye miinuko, lakini tunafahamu kwamba kuna changamoto ya kivuko hili liko kwenye mipango yetu, ninaomba Mheshimiwa Mbunge awe na subira wakati tunatekeleza.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, utalii kwenye ukanda huu alioutaja tuna mkakati mahususi wa kutangaza utalii wa fukwe lakini vilevile na maeneo yote yalioko kwenye ukanda huu. Tayari kazi kubwa inafanyika, mwezi uliopita tulikuwa Berlin tukitangaza vivutio vyetu kwa nchi za Ukanda wa Ulaya ni imani yangu kwamba tutapata uwekezaji lakini vilevile tutapata watalii watakaokuja kwenye eneo. Vilevile, tunafanya kazi kubwa sana tangu kuanza kwa mwaka wa fedha huu mpaka mwezi huu Machi tayari meli karibu tisa za watalii kutoka nje zimeshafika kufanya shughuli za kiutalii katika nchi yetu.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Sophia.

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Katika Wilaya ya Rungwe kuna Maporomoko ya Kapologwe na Malasusa, lakini katika Daraja la Mungu. Serikali inasema nini kwa ajili ya kuweka uwekezaji pale maana ni pa chafu sana na hapana maendeleo yoyote? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeweka mikakati madhubuti ya kutangaza utalii katika ukanda wa nyanda za juu kusini na miongoni mwa maeneo ambayo yanatiliwa mkazo ni maeneo ya maporomoko na utalii wa misitu. Ninaomba Mheshimiwa Mbunge awe na imani kwamba jambo hili tunalifanyia kazi.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea Wizara ya Mawasiliano, Mheshimiwa Twaha.

Na. 103

**Uhitaji wa Mawasiliano Maeneo ya Delta – Kibiti**

**MHE. TWAHA A. MPEMBENWE** aliuliza:-

Je, upi mkakati wa Serikali kuhakikisha kuwa maeneo ya Delta Kibiti yanafikiwa na mawasiliano ya simu?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote *(UCSAF)* inatekeleza Mradi wa Tanzania ya Kidijitali *(DTP)* kwa lengo la kufikisha mawasiliano katika sehemu mbalimbali nchini ikiwemo Delta - Kibiti.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika awamu hii ya utekelezaji wa mradi huu, Kibiti imenufaika kwa kupata idadi ya minara saba ambapo Minara minne kati ya hiyo inajengwa katika eneo la Delta katika Kata za Msala, Maparoni, Salale na Kiongoroni, ambapo kukamilika kwa ujenzi wa minara hii kutaimarisha hali ya mawasiliano katika eneo la Delta. Kwa sasa utekelezaji wa ujenzi wa minara hii ambayo ni sehemu ya Mradi wa Ujenzi wa Minara 758 upo katika hatua mbalimbali za ujenzi na kwa mujibu wa mikataba, mradi huu unatarajiwa kukamilika ifikapo Mei, 2025. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Twaha.

**MHE. TWAHA A. MPEMBENWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru sana kunipatia nafasi. Kwanza kabisa ninaomba niipongeze Serikali kwa kazi kubwa na nzuri ambayo imefanya ya kupeleka mawasiliano katika Jimbo la Kibiti, eneo la Beta. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nina maswali mawili madogo ya nyongeza. Swali la kwanza; katika Kata ya Salale Kijiji cha Mfisini na Kiomboni wale wakandarasi walishafika muda mrefu, wameainisha yale maeneo ya kujenga minara, lakini mpaka leo bado hawajafika kule. Ninataka kujua, lini sasa wakandarasi wale wataanza ujenzi huo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; kwenye Kijiji cha Mchukwi pale kuna Hospitali ya Mchukwi hakuna kabisa mawasiliano. Nini sasa mkakati wa Serikali katika kuweza kuhakikisha pale panapelekwa mawasiliano? Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Awali ya yote nipende kupokea pongezi kwa Serikali. Kwa kweli tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais namna ambavyo amesimamia kidete kuhakikisha mawasiliano yanafika maeneo yote. Nimpongeze Mheshimiwa Mbunge kaka yangu Twaha kwa ufuatiliaji wake kama tulivyoongea hivi karibuni alivyotembelea Wizarani.

Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo haya ya visiwa kule Kiomboni na kile Kijiji kingine tayari wataalam wetu wanaendelea kuona namna njema ya kufikisha *signal* pale. Kama unavyofahamu maeneo yenye maji, ujenzi wa minara umekuwa wa usumbufu kidogo, lakini wataalam watahakikisha minara itajengwa eneo ambalo litaelekeza kuhakikisha *signal* zinafika katika maeneo yale ya visiwani.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo hili la Hospitali pia kama tulivyoongea Mheshimiwa na Twaha katika ufuatiliaji wake, Mheshimiwa Jerry Silaa ameshaagiza sana kuhakikisha kwamba, maeneo yote ambayo yanatoa huduma za kijamii, hospitali, shule, vyuo na masoko lazima uhakika wa mawasiliano uweze kuwepo. Hivyo nimtoe hofu katika hili pia tutasimamia. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Suma.

**MHE. SUMA I. FYANDOMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa swali dogo la nyongeza. Wilaya ya Kyela Kata ya Bujonde, Ikolo, Katumbasongwe na Ngonga mawasiliano yamekuwa ni shida sana kwa sababu hakuna mnara pale. Je, ni lini Serikali itakwenda kujenga mnara huo ili wananchi wale waweze kupata mawasiliano? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Suma Fyandomo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo haya ya Kyela ni juzi tu nimetoka kufanya ziara kwa kuhakikisha maeneo haya ya mpakani yote yanapata mawasiliano ya uhakika. Kata hizi zote alizozitaja zipo katika mpango wa kuhakikisha minara inajengwa kwa muda ambao wakandarasi wamesaini mikataba na maeneo yaliyoweza kufanyiwa tathmini, kadri tunavyopata fedha lazima tupeleke minara. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Michael.

**MHE. MICHAEL C. MWAKAMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, mara nyingi nimekuwa nikiuliza juu ya upatikanaji wa mawasiliano kwenye Kijiji cha Kimalamisale kule Kata ya Dutumi. Leo ninaomba Mheshimiwa Waziri uniambie lini utakuwa na nafasi mimi na wewe tufike pale pamoja, ili wananchi wakajiridhishe mnara utapatikana? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, nafasi yako.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mbunge wa Kibaha Vijijini tumeongea juzi na tumekubaliana baada ya Pasaka kwenye tarehe 24 au 25 mida ya mchana tutakwenda pale kuhakikisha yule mkandarasi kwanza aliyekuwa amesainishwa, tufahamu shida yake ipo wapi ili kuhakikisha mnara unajengwa na

wananchi wa Kimalamisale waweze kupata mawasiliano ya uhakika. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa, tunaendelea na Wizara ya Mambo ya Ndani, Mheshimiwa Omar Issa Kombo.

Na. 104

**Kujenga Ofisi ya NIDA Micheweni**

**MHE. OMAR ISSA KOMBO** aliuliza:-

Je, lini Serikali itajenga Ofisi ya *NIDA* katika Wilaya ya Micheweni?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa inaendelea na utekelezaji wa Mradi wa Vitambulisho vya Taifa awamu ya pili ambao unahusisha ujenzi wa Ofisi za Usajili katika Wilaya 31, ujenzi wa Jengo la Makao Makuu ya *NIDA* Jijini Dodoma na ujenzi wa Kituo cha Matengenezo ya Vifaa vya TEHAMA.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa utekelezaji wa mradi huo, upo katika hatua ya usanifu wa michoro ya majengo na miundombinu ya TEHAMA pamoja na utaratibu wa kumpata Mkandarasi. Aidha, ujenzi unatarajiwa kufanyika kwa miaka mitatu kuanzia Mwaka wa Fedha 2025/2026 na jumla ya shilingi 29,138,814,000 zimetengwa kwa ajili ya ujenzi wa majengo hayo ikiwemo na Ofisi ya *NIDA* Wilaya ya Micheweni. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kombo.

**MHE. OMAR ISSA KOMBO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu, lakini ninaomba niulize maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza; kati ya shilingi bilioni 29.1 alizozitaja tunapenda kufahamu; je, Wilaya ya Micheweni peke yake imetengewa kiasi gani cha fedha? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; je, Mheshimiwa Naibu Waziri haoni ipo haja ya kutembelea Wilaya ya Micheweni kwenda kujionea hali halisi ya Wilaya ya Micheweni jinsi Ofisi hii ambavyo ina ufinyu wa ofisi na wananchi wanapata tabu katika kufuata huduma hizi? Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Omar Issa Kombo, Mbunge wa Wingwi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kati ya fedha zilizotajwa shilingi bilioni 29.1, Wilaya ya Micheweni imepangiwa shilingi milioni 500, lakini kwa mwaka wa fedha 2026/2027 wataanza na shilingi milioni 170.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu swali la pili, kwenda kuona Ofisi ya Micheweni nipo tayari nitapanga na Mheshimiwa Mbunge katikati ya kipindi hiki cha Bunge la Bajeti twende tukaone hali halisi kule Micheweni.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mtemvu.

**MHE. ISSA J. MTEMVU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru kwa nafasi. Kwa kuwa uhitaji wa Vitambulisho vya *NIDA* kwa wananchi wetu imekuwa ni muhimu sana kutokana na uhitaji wa huduma nyingine, lakini ni ukweli katika maeneo ya majiji na miji mikubwa wananchi wanapanga foleni kutoka asubuhi hadi jioni kutafuta Vitambulisho vya *NIDA,* kwa sababu upatikanaji wake umekuwa *centrally* kwenye Ofisi za Wilaya. Je, Serikali mko tayari sasa kuongeza watumishi na kupeleka huduma hizi kwenye kata ili wananchi walio wengi wapate kule wanapotokea badala ya kutumia muda mrefu kule Wilayani?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Issa Mtemvu, Mbunge wa Kibamba kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli vitambulisho vya Taifa ni muhimu kwa ajili ya huduma za kijamii, kiuchumi pamoja na huduma nyingine. Tunajipanga kama *NIDA* kuhakikisha kwamba wananchi wetu wanapata vitambulisho katika maeneo ya karibu. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tunajipanga kama *NIDA* kuhakikisha kwamba, tunasogeza huduma hii kwa wananchi ili wapate vitambulisho vyao kwa muda bila kupoteza muda mwingi. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Maji. Mheshimiwa Kaiza kwa niaba yake Mheshimiwa Matiko.

Na. 105

**Gharama ya Uchimbaji Kisima**

**MHE. ESTHER N. MATIKO K.n.y. MHE. AGNESTA L. KAIZA** aliuliza:-

Je, kabla ya kuwa na mitambo ya uchimbaji wa Visima ya Serikali, gharama ya uchimbaji wa kisima ilikuwa kiasi gani ukilinganisha na gharama ya sasa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeendelea kuboresha eneo la utafutaji wa vyanzo vya maji chini na juu ya ardhi ili kuhakikisha wananchi wanapata huduma ya maji safi na salama kupitia miundombinu ya maji iliyopo na inayojengwa. Moja ya maboresho yaliyofanyika ni pamoja na ununuzi wa seti tano za ujenzi wa mabwawa na mitambo 25 ya uchimbaji wa visima.

Maboresho hayo yamesaidia kupunguza gharama za uchimbaji visima kutoka shilingi 210,000 kwa urefu wa kina cha mita moja mwaka 2021 na kufikia shilingi 150,000 kwa sasa. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Matiko.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa takwimu ambayo Serikali imetoa hapa ni dhahiri kwamba bado uchimbaji wa maji kwa visima ni ghali sana pamoja na kwamba ni mitambo ya Serikali, kwa sababu tuna *experience* kuchimbia hata kwa *private sector* inakuwa chini kwa hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa maswali yangu, swali la kwanza; kuna taasisi mbalimbali kwa mfano, vituo vya afya, zahanati na taasisi za shule zinakuwa hazina maji na unakuta kwa mfano wanafunzi wanatumia muda mrefu kwenda kutafuta maji. Ni kwa nini Serikali isingetoa kipaumbele kwa mitambo hii kuweza kuchimba visima kwenye taasisi pale ambapo maji hayajafika kwenye maeneo ambayo maji hayajafika?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; mitambo hii imewekezwa sana vijijini. Maeneo ya mijini kwa mfano, pale Tarime Mjini hatujapata huduma hii na unakuta labda kuna miradi ya kimkakati. Kwa hiyo, pale Tarime Mjini tuna Mradi wa maji kutoka *Lake Victoria*. Ninataka kujua kwa maeneo ambayo mitambo hii haifiki, Serikali ina mkakati gani kuhakikisha miradi ya maji ambayo imewekwa pale kama *Lake Victoria* kwenda Tarime unakamilika kwa wakati, ili Watanzania wale waweze kupata huduma ya maji?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Esther Matiko, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, gharama kama ambavyo nimejibu katika jibu langu la msingi kwa kweli zimepungua kwa kiwango

kikubwa kutoka shilingi 210,000 mwaka 2021 na kufika shilingi 150,000 mwaka 2025. Hapo unaona kabisa kwamba kuna punguzo kubwa sana ambalo linatokana na Serikali kuchukua hatua ya kununua mitambo yake yenyewe. Tunatambua kwamba ni lazima tuendelee kupunguza gharama, lakini tunafahamu pia yale ambayo yanaendelea kufanyika tayari yanaonesha kuna mabadiliko makubwa sana katika sekta hii ya uchimbaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la vituo vya afya na shule; ni dhamira na ni kipaumbele cha Serikali kuhakikisha kwamba, watoto wetu waliopo katika shule wanaweza ku-*access* maji katika wakati wowote. Pia, vituo vya afya haviwezi kuendeshwa bila kuwa na maji ya uhakika.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunachokifanya ni nini? Tunaendelea kushirikiana na wenzetu wa Ofisi ya Rais, TAMISEMI kuwa na mpango mzuri zaidi pale tunapojenga shule na vituo vya afya basi kuwe *package* ya moja kwa moja kuhakikisha kwamba kutakuwa na maji ya uhakika katika maeneo hayo ili wananchi waweze kupata huduma ya maji safi na salama shuleni pamoja na vituo vya afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo la Serikali kununua mitambo hii ni kuangalia namna ambavyo vijijini ilikuwa imeachwa mbali sana na upatikanaji wa huduma ya maji. Kwa sababu mijini tayari tuna miradi ya kimkakati kama ambavyo Mheshimiwa Mbunge ametaja. Mkakati wa Serikali ni kuhakikisha kwamba, tunaendelea kusukuma miradi hii ya kimkakati ikamilike kwa wakati ili wananchi wa mijini waendelee kupata huduma ya maji kutokana na vyanzo ambavyo Mwenyezi Mungu ametujaalia kuwa navyo hasa Ziwa Victoria ambapo ndio suluhisho linaloonekana katika Ukanda wa Ziwa. Kwa hiyo, nimtoe wasiwasi Mheshimiwa Mbunge Serikali tunaendelea kulifanyia kazi na tuna hakika kabisa miradi hii itakamilika na wananchi watapata huduma ya maji safi na salama.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Bulaya. Jiandae Mheshimiwa Jesca.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru kwa kunipatia nafasi niulize swali dogo la nyongeza. Mbali ya mkakati wa Serikali kununua hiyo mitambo na kuchimba visima, kuna miradi ambayo imeanzishwa ukiwepo mradi wa Nyabehu kupitia Ziwa Victoria, kutoka Nyabehu Kata ya Guta kuja Bunda Mjini. Vilevile, kuna changamoto ya miundombiunu kutoka Kata ya *Bunda Store* kwenda Mlima Kasakwa lile bomba kubwa ambayo inasababisha 45% ya maji ya ule mradi yanapotea. Tunahitaji *seven billion,* ili kupata hilo bomba kubwa kutoka *Bunda Store* kwenda Mlima Kasakwa ili wananchi sasa wa kata zote 14 wawe wana uhakika wa kupata maji safi na salama. Ni lini mtabadilisha hilo bomba kubwa ambalo linafanya maji ya mradi 45% yanapotea? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kujibu swali zuri kabisa la Mheshimiwa Ester Bulaya. Ni kweli kabisa tuna maeneo mbalimbali nchini ambayo yana changamoto ya miundombinu. Aidha, miundominu hiyo imechakaa au imewekwa katika namna ambayo inasababisha upotevu wa maji. Upotevu wa maji ni hasara kubwa kwa Serikali. Sisi Serikali tumeshaliona hilo ndio maana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, ameshatoa fedha za kuhakikisha kwamba tunaendelea kuboresha miundombinu ambayo imeshachakaa. Lengo ni kuokoa upotevu wa maji ambao unatutia hasara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimtoe wasiwasi Mheshimiwa Mbunge, katika eneo ambalo amelitaja ni moja ya maeneo ambayo tumeyatazama kuhakikisha kwamba fedha itakapopatikana mara moja tu, tunaipeleka kwa ajili ya kuhakikisha kwamba bomba hilo linaenda kufanyiwa ukarabati, ili wananchi wasiingie hasara ya kulipia maji ambayo hawayatumii. Lengo ni kwamba wapate maji kulingana na namna wanavyolipia, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Jesca.

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Moja ya mkakati wa kutusaidia sisi tulioko mijini kupekeka maji kwenye maeneo yenye sura za vijiji lakini yapo mijini, ilikuwa ni kuchimba visima vitano. Sasa, kuna eneo la Ugele na Mosi pale Iringa kutokana na jinsi lilivyo kuchimba kwa mitambo ya kawaida ilishindikana. Je, mpo tayari sasa kutuletea mitambo hiyo mikubwa, ili tuchimbe visima wananchi wale wapate maji? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nilipokee suala hilo kwa sababu lipo *specific* kwamba eneo hilo limekuwa na changamoto ya hii mitambo yetu ambayo imeshindwa basi tuweze kuona namna nyingine ambayo tunaweza tukakamilisha ile dhamira ya Serikali kuhakikisha kwamba tumechimba visima katika maeneo hayo na wananchi wa Mheshimiwa Jesca waweze kupata majisafi na salama. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, maswali yamekwisha. Wageni waliopo Bungeni asubuni hii.

Wageni waliokaa Jukwaa la Spika. Wageni wanne wa Mheshimiwa Hamisi Shabani Taletale, watoto wake kutoka Mkoani Morogoro ambao ni Ndugu Zahid Taletale, Ndugu Tale Taletale, Ndugu Tamir Taletale na Ndugu Tatiana Taletale. *(Makofi)*

Wageni wa Waheshimiwa Wabunge. Wageni 33 wa Mheshimiwa Innocent Bashungwa, Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi ambao ni Wajumbe wa *ATAPE SDA* kutoka Bukoba Mkoani Kagera, wakiongozwa na Mwenyekiti Ndugu Daniel Rwechungura. Karibuni. *(Makofi)*

Wageni wa Mheshimiwa Kenneth Nollo, rafiki yake Ndugu Brian Sinkara ambaye ni Mtumishi wa Mungu kutoka Jijini Arusha. Karibu. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Sylvia Sigula Ndugu, Salome Simwanza ambaye ni mpigakura wake kutoka Sumbawanga. *(Makofi)*

Wageni watatu wa Mheshimiwa Njalu Silanga ambao ni marafiki zake kutoka Mkoa wa Simiyu. *(Makofi)*

Wageni 65 wa Mheshimiwa Jesca Jonathani ambao wanafunzi 56 na walimu tisa kutoka Shule ya Sekondari ya *SCIM Polytechnic* ya Mkoani Iringa. Karibuni. *(Makofi)*

Wageni 47 wa Mheshimiwa Ally Juma Makoa ambao ni wanafunzi na walimu wa Shule ya Msingi Kondoa *Integrity* ya Kondoa, Mkoa wa Dodoma. *(Makofi)*

Wageni watano wa Mheshimiwa Jonas Van Zeeland ambao ni Viongozi wa CCM wa Kata ya Pemba wakiongozwa na Diwani Mheshimiwa Costar Rouben kutoka Wilaya ya Mvomero, Mkoa wa Morogoro. *(Makofi)*

Wageni watatu wa Mheshimiwa Stanslaus Shing'oma Mabula ambao ni Waadventista Wasabato kutoka Nyamagana Mkoani Mwanza. Karibuni. *(Makofi)*

Wageni watatu wa Mheshimiwa Nashon William ambao ni wapigakura kutoka Nguruka Mkoani Kigoma. *(Makofi)*

Wageni watatu wa Mheshimiwa Nusrat Shaaban Hanje ambao ni watoto wake kutoka Mkoani Sindiga. *(Makofi)*

Wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo. Tunao wanafunzi 60 ambao ni Wanachama wa Chama cha Skauti kutoka Shule ya Msingi Kibaha *Independent* na *Future Star*. *(Makofi)*

Tunao pia wanafunzi 65 wa Chama cha Skauti kutoka Shule ya Awali na Msingi *Mother of Mercy* iliyopo Wilaya ya Kinondoni Jijini Dar es Salaam. *(Makofi)*

Katibu.

**NDG. ATHUMANI HUSSEIN, *ndc* – KATIBU MEZANI:**

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**NAIBU SPIKA:** Majadiliano yanaendelea. Waheshimiwa Wabunge, tunaanza na mijadala ya Wizara hii ya TAMISEMI na tunaanza na Mheshimiwa Joseph Kizito.

**MHE. JOSEPH K. MHAGAMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru kwa kupata fursa hii asubuhi ya leo niweze kuchangia Hotuba ya Bajeti ya Mheshimiwa Babu yangu Mohamed Mchengerwa, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza niruhusu niungane na Waheshimiwa Wabunge ambao wamempongeza sana Mheshimiwa Rais kwa namna ambavyo amepeleka kipaumbele sana kwenye hii Ofisi ya TAMISEMI, kwa sababu amekusudia kuwafikia Watanzania walio chini kabisa ambao wanahitaji huduma zote muhimu zikiwemo afya, elimu na kadhalika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kama ambavyo Waheshimiwa Wabunge wamesema, mimi pia kwa niaba ya wananchi wa Madaba ninampongeza sana Mheshimiwa Rais na ninamshukuru sana kwa vipaumbele ambavyo ametupatia katika Jimbo letu la Madaba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niruhusu pia nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri na Naibu Mawaziri wa hii Ofisi, kwa sababu hawa watu ni wazalendo sana. Kazi na mafanikio makubwa ambayo tumeyapata kwenye halmashauri na majimbo yetu imetokana na uzalendo mkubwa ambao Mheshimiwa Waziri na

wasaidizi wake wanao kwa Watanzania. Kwa hiyo, tunamshukuru sana Mheshimiwa Waziri na timu yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimetoka kwenye ziara ya vijiji, ziara ya Kata zote za Madaba na nimebakiza vijiji vinne tu, ziara yangu ilikusudia kuona namna gani tunaweza kuendelea kuweka vipaumbele vya maendeleo ya wananchi kwa msukumo na kwa mahitaji ya wananchi wa Madaba. Wananchi wa Madaba walitamani kuona nini kwenye bajeti hii? Hilo ndilo jambo kubwa ambalo lilinifanya nifanye ziara.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la kwanza ambalo wananchi wa Mabada walitamani kuliona, ni kuona kwamba Serikali inaendela kutenga bajeti ya kutosha kwa ajili ya barabara za vijijini kupitia *TARURA* na ninawathibitishia wananchi wa Madaba na ninatumia fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Rais, kwamba Madaba tumetengewa fedha za kutosha kwa ajili ya ujenzi wa barabara na vipaumbele vyetu tutaendelea kuviweka kwenye barabara zinazoenda kwenye maeneo ya huduma muhimu, ikiwemo barabara ya Ngongongo ambayo itatuwezesha kufika kwenye hospitali yetu ya Wilaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ile tutaendelea kuijenga kwa lami na bajeti ipo, pia barabara zinazoelekea maeneo ya uzalishaji ikiwemo mashambani na kadhalika huko pia tumepata fedha za kutosha, ninaamini maeneo haya yenye changamoto ikiwemo Barabara ya Lifanzulu - Kijiji cha Kipingo itaweza kujengwa kwa ubora na barabara zetu za Ifinga na maeneo mengine zitaendelea kuimarishwa. Kwa hiyo, nilitamani niliseme ili wananchi wa Madaba waweze kujua ni eneo gani ambalo limepewa kipaumbele kwenye bajeti yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Madaba tunayo changamoto ya mapato ya ndani, hii inatokana na uchanga wa Halmashauri yetu. Tulianza na mapato ya ndani yasiyozidi shilingi milioni 900 kwa mwaka, lakini sasa tumeweza kufanya mara mbili zaidi, tumefika kama shilingi 1,900,000,000. Tumeendelea kupeleka vipaumbele kwenye miradi ya kimkakati ambayo itatusaidia kuongeza mapato kwa asilimia kubwa, mapato ambayo

yatatusaidia pia kuchangia maendeleo ya vijana, wanawake na watu wenye ulemavu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye eneo hili la miradi ya mkakati tumeweka kipaumbele kwenye kongani la viwanda ambalo litajengwa maeneo ya Kipingo ambapo kama tutafaulu itaweza kutoa ajira za moja kwa moja na zisizo za moja kwa moja zaidi ya laki tano, hizi ni ajira nyingi sana. Pia tunayo maeneo muhimu ya masoko ya bidhaa za mbao ambayo tunayajenga maeneo ya Wino, huko tunapeleka pia vipaumbele, lakini jambo ambalo nilitaka niliwekee mkazo leo ni mradi wetu wa kimkakati wa stendi ya Madaba.

Mheshimiwa Naibu Spika, utakumbuka kwa muda mrefu nimekuwa ninalalamika na kuililia Serikali kuhusiana na mradi huu, kwa sababu unaenda kuongeza mapato ya Halmashauri yetu kwa 100% au 200%, kwa maana ya kutoka shilingi bilioni 1.9 ambayo tunayo sasa, mpaka tutafika karibu shilingi bilioni nne za maingizo ya mapato ya ndani, mapato ambayo hayana masharti ambayo yatatuwezesha pia kuwasaidia vijana, wanawake na watu wenye ulemavu, kwa kupitia mikopo ya 10%, kwa hiyo, ninaishukuru Serikali kwenye eneo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza *TASAF* wametenga zaidi ya shilingi milioni 480 na tayari kazi imeanza kwa maana ya utafutaji wa mkandarasi na uandaaji wa eneo la ujenzi wa stendi. Pili, kwenye bajeti hii tuliomba shilingi bilioni tano na bilioni moja tayari imeshatengwa kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huu. Kwa hiyo, ninataka sasa nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri na Serikali hii kwa kutoa kipaumbele kwa wananchi wetu wa Madaba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mapato haya yanaenda kutatua changamoto kubwa sana ambayo tunayo kwa vijana wetu wa Madaba. Wakati ninafanya ziara nimekutana na makundi mbalimbali ya wanawake, nimekutana na makundi ya vijana. Vijana wengi vijana wa bodaboda wanalalamika kwamba hawapati mikopo, kwa mwaka huu ninashukuru kwa awamu hii tunayokwenda, maana yake kwenye bajeti hii imetengwa shilingi

bilioni 153 ambazo zitaenda kwa vijana wetu wa bodaboda, vikundi vya akinamama, maeneo yote ya Kata zetu za Madaba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto ambayo ninaiona ni maandalizi ya vijana hawa, tunamwomba Mheshimiwa Waziri waendelee kupeleka nguvu kwa hawa tunaowaita Maafisa Maendeleo ya Jamii, wengi '*wamejiziuka*' sana. Unaenda kwenye ziara vijana wanasema hatuna taarifa ya mikopo ya 10%. Vijana ambao wapo katika eneo la mjini kama Madaba na viunga vyake vyote, Waziri anapajua, kuna vijana ambao mpaka leo wameshindwa ku-*access* mikopo hii, siyo kwa sababu hawana sifa, ila kwa sababu baadhi ya watu ambao tumewapa jukumu hilo la kuwasimamia na kuwaandaa vijana hawa, hawafanyi hilo jukumu. Nimeenda kwenye Kata moja ninaambiwa vikundi 10 viliomba, vikundi viwili vimeandika andiko lao vizuri, vikundi nane vimeshindwa kuandika maandiko yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hawa wakulima, hawa wafugaji, hawa madereva wa bodaboda wanapata wapi ujuzi wa kuandika maandiko? Tumewaajiri Maafisa Maendeleo ya Jamii wafanye kazi na hivi vikundi vya kijamii, vikundi vya maendeleo, waviwezeshe, wavisaidie kuandika maandiko ya miradi yao. Mheshimiwa Waziri apeleke nguvu kwenye eneo hilo ili awajengee uwezo Maafisa Maendeleo ya Jamii kuweza kuvisaidia hivi vikundi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu ya maslahi ya muda, ninarudia kuishukuru Serikali na ninawajulisha wananchi wa Madaba kwamba, pia shule zetu zote zimepangiwa fedha, maboma yote yamepangiwa fedha, lakini pia miradi ya afya kwa maana ya hospitali yetu ya wilaya pamoja na zahanati na vituo vya afya, vyote vimepangiwa bajeti. Kwa hiyo, bajeti ya mwaka huu upande wa TAMISEMI imetupa kipaumbele kikubwa na tutapiga hatua kubwa sana kimaendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru kwa nafasi hii. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ally Mohamed Kassinge, wajiandae Mheshimiwa Njalu Daudi Silanga na Mheshimiwa Msongozi.

**MHE. ALLY M. KASSINGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru kwa nafasi. Baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu ninapeleka shukrani zangu za dhati kabisa kwa Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwani katika Jimbo letu la Kilwa Kusini kwenye Sekta ya Afya, Sekta ya Elimu, Sekta ya Barabara zinazosimamiwa na *TARURA*, kwa kweli Mheshimiwa Rais ametutendea haki sisi wananchi Kilwa Kusini na ifikapo Oktoba 2025 *Insha Allah* ataona shukrani zetu sisi wa Jimbo la Kilwa Kusini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya shukrani hizi, pia ninapeleka shukrani na pongezi kwa Wizara yetu ya TAMISEMI, kwani sisi Kilwa tulikuwa na changamoto kubwa ya miundombinu mibovu pale kwenye hospitali yetu ya Wilaya Kinyonga - Kivinje. Mheshimiwa Rais kupitia Ofisi yake ya TAMISEMI ametuletea fedha shilingi milioni 900 za ukarabati. Hivi tunavyozungumza tayari tuna miundombinu inayoridhisha katika jengo la *X-Rays*, jengo la maabara, jengo la kichomea taka, kwa kweli tunaishukuru sana Wizara yetu ya TAMISEMI. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kana kwamba haitoshi, tumeletewa fedha zaidi ya shilingi millioni 300 kwa ajili ya ujenzi wa jengo la *emergency* kwenye Hospitali yetu ya Wilaya, Kinyonga. Hivi tunavyozungumza tayari linafanya kazi, pongezi sana kwa Wizara yetu ya TAMISEMI. Kwa hiyo, pongezi hizi ziende kwa Waziri wetu wa TAMISEMI Ndugu yangu Mheshimiwa Mchengerwa, Naibu Waziri wake, Mheshimiwa Dkt. Dugange pamoja na dada yangu Mheshimiwa Zainab Katimba, pia Katibu Mkuu, Naibu Makatibu Wakuu, Wakurugenzi wote wa Wizara ya TAMISEMI na watumishi wote katika *level* ya Wizara, Mikoa na Halmashauri zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati tunakarabati na kuboresha sekta ya afya, ninaendelea kushukuru pia kwamba pale Kilwa

Kusini tumekamilisha ujenzi wa kituo cha afya cha Hoteli Tatu na kinafanya kazi, tunaishukuru sana TAMISEMI. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tulikuwa na maombi ya vituo vyetu vya afya vya kimkakati, kwenye Jimbo langu nilipendekeza Kata ya Likawage, tunaomba ile ahadi ya fedha za kuanzia shilingi milioni 300 kwa kila Jimbo kwenye vituo vya afya vya kimkakati ziharakishwe kupitia Ofisi ya Rais, TAMISEMI ili wananchi wetu wakaone utendaji kazi wa Serikali yao ambayo wanaiamini.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na yote hayo, tumeendelea kupata fedha kwa ajili ya ujenzi wa zahanati zetu. Tumekamilisha ujenzi wa zahanati Kisongo na inafanya kazi, tumepata fedha kwa ajili ya ujenzi wa zahanati kule Liwiti na ujenzi unaendelea. Tumepata fedha kwa ajili ya ujenzi wa zahanati kule Makangaga, ujenzi unaendelea. Haya yote ni matunda na kazi iliyotukuka ya Serikali yetu ya Awamu ya Sita chini ya Mheshimiwa Dkt. Samia.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika maeneo haya ninatoa rai na maombi kidogo kwenye Sekta hii ya Afya nikianzia na eneo la hospitali ya Wilaya pale Kinyonga, pamoja na yote hayo, lakini tunaomba kupitia bajeti ya TAMISEMI tujengewe uzio ili sasa mindombinu ile mizuri inayopendeza iwe katika uzio, wafanyakazi wawe katika mazingira bora, pia wagonjwa na wauguzi wawe katika maeneo ambayo kwa kweli yana staha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hayo, kumekuwa na changamoto kubwa ya watumishi. Katika hospitali yetu ya Wilaya ya Kinyonga tuna mahitaji ya watumishi 325, waliopo ni 118 tu. Hiyo ni chini ya 37% ya mahitaji yote. Tunaomba wakati tunatenga bajeti kwa ajili ya kutengeneza miundombinu ya afya, pia tukumbuke kwenda sambamba na kutenga bajeti ya kuwa na watumishi wa kutosha watakaohudumia vituo vyetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, upande wa elimu, ninaishukuru Wizara yangu ya TAMISEMI kwamba Jimbo langu la Kilwa Kusini tumepata sekondari mpya ya kisasa pale Ngome Sekondari, Kilwa Masoko. Pia, tunakamilisha Sekondari ya Mavuji katika Kata ya

Mandawa, pia, ujenzi wa sekondari nyingine ya kisasa unaendelea katika Kata ya Lihimalyao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika maeneo haya nizungumze kwa uchache tu kwamba pale Sekondari ya Mavuji, pamoja na kwamba ujenzi umekamilika kwa hatua zaidi ya 90% na kazi ya kusomesha vijana wetu imeanza, lakini shule hii bado haijasajiliwa. Ninaomba kupitia Ofisi ya Rais, TAMISEMI waharakishe kupata usajili wa shule yetu ya sekondari pale Mavuji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tulipata fedha za ukarabati wa shule za msingi ambazo zimechakaa, tunaishukuru sana Serikali yetu. Tulipata ukarabati wa Shule ya Msingi Masoko, sasa madarasa yanaridhisha. Tulipata fedha za ukarabati kwa ajili ya shule ya msingi pale Mirumba, sasa madarasa yanaridhisha. Tulipata fedha za ukarabati Shule ya Msingi Kiranjeranje, madarasa mazuri. Haya yote ni matunda ya Serikali yetu, kwa kweli sisi wananchi wa Kilwa tunajivunia sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba na ninatoa rai kupitia Ofisi ya Rais, TAMISEMI, kwamba iendelee kufanya tathmini ya shule zilizochakaa sana shule kongwe za msingi na za sekondari ili utaratibu huu wa kutenga fedha za ukarabati kila mwaka uendelee. Kwa bajeti hii ninaomba kwenye Jimbo langu la Kilwa Kusini waiangalie kwa karibu Shule ya Msingi Mnazi Mmoja pale Kilwa Masoko, lakini pia Shule ya Msingi Lihimalyao Kaskazini katika Kata ya Lihimalyao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, upande wa sekondari, ukifanya tathmini ya Wilaya ya Kilwa hususan Jimbo la Kilwa Kusini, Kata ya Kivinje Singino imekuwa ni kata ambayo ina wanafunzi wengi sana wa shule ya msingi ambao wanashindwa kupata ukaribu wa shule za sekondari. Kwa mfano, ukiangalia Kijiji cha Matandu peke yake, ni kijiji ambacho wanafunzi wanapata shida kwenda kusoma sekondari iliyopo kule Dodomezi. Wengine wanakwenda kule Mipingoni kule. Sasa hii kidogo imekuwa shida.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikaa na wananchi wenzangu wa Matandu, tumetenga eneo pale Matandu kwa ajili ya ujenzi wa

sekondari. Tunaomba kupitia utaratibu ule wa *SEQUIP* tuweze kupata fedha kwa ajili ya ujenzi wa sekondari Matandu, ili kupunguza adha ya wanafunzi wetu ambao wanatembea umbali mrefu na wakati mwingine wanalazimika kudandiadandia magari yasiyokuwa na uhakika kwenda kufuata elimu ya sekondari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie kwa uchache eneo la barabara, hususan kupitia sekta au idara yetu hii ya *TARURA*. Sisi Kilwa kama Wilaya, tunashukuru. Mwaka 2016/2017 bajeti yetu nzima ya Wilaya ilikuwa ni shilingi milioni 999 tu. Hivi leo tunazungumza, kupitia Mheshimiwa Rais wetu, bajeti yetu sasa hivi ya *TARURA* ni shilingi bilioni 4.4. Kupitia bajeti hii tumeweza kufungua barabara mpya, tumeweza kuweka kuweka lami sehemu ambazo zilikuwa hazina lami, angalau katika maeneo yetu ya miji na taa za barabarani, lakini pia tumeweza kuunganisha miundombinu katika maeneo ambayo barabara zilikuwa hazipitiki kipindi chote cha mwaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninatoa rai katika eneo hili la *TARURA* kwamba, pamoja na fedha ambazo tunatengewa kila mwaka kupitia tozo, kupitia *Road Fund* pamoja na maeneo mengine, tuwe na fedha za dharura. Wananchi wa Kilwa tuliathirika sana mwaka jana, sote ni mashahidi, barabara zetu zote ziliharibika kwa kiwango kikubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa dhati kabisa ninaishukuru Serikali yangu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania chini ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, ametupatia fedha za ukarabati wa miundombinu iliyoharibika, angalau kwa kuanzia sisi Kilwa Kusini tumepata shilingi milioni 200, tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais. Ninapendekeza kwamba, fedha hizi shilingi milioni 200 ziende kukarabati na kujenga barabara iliyoharibika sana ya kutoka Hoteli Tatu – Mkazambo – Mtangashari mpaka Pande, kule maeneo ya Malalani. Tukifanya hivi ninadhani tutakuwa tumetendea haki hizi fedha ambazo Serikali yetu imetutengea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, nina ombi mahsusi, sisi hatujaingia katika miradi ya kimkakati.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Kassinge muda wako umekwisha.

**MHE. ALLY M. KASSINGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa nafasi. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Njalu Daudi, jiandae na Mheshimiwa Msongozi.

**MHE. NJALU D. SILANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia hotuba hii kubwa nzuri, hotuba ambayo imebeba maudhui ya Watanzania kwa maana ya TAMISEMI, inayoshughulikia wananchi na matatizo yote ya nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa na nzuri ambayo ameifanya katika Serikali yake ya Awamu ya Sita. Jinsi gani alivyotiririsha fedha nyingi kwenye majimbo yetu na kwenye utawala wetu. Pia, ninampongeza sana Waziri wa TAMISEMI Mheshimiwa Mchengerwa na Wasaidizi wake, Mheshimiwa Dkt. Dugange pamoja na Mheshimiwa Zainab kwa kazi kubwa na ufuatiliaji mzuri wanaoufanya kwenye Majimbo yetu ambayo inapelekea kupunguza maswali mengi katika Bunge lako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee ninampongeza sana Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa wetu, Mkoa wa Simiyu, Mheshimiwa Kenan Kihongosi kwa kazi kubwa na nzuri anayoifanya katika Mkoa wetu wa Simiyu. Ninaamini kwamba Serikali ya Awamu ya Sita jinsi inavyofanya uteuzi wake katika maeneo yetu ni dhahiri kwamba vijana wa nchi hii wamepewa dhamana kubwa ya kuaminiwa. Kama hapo tunavyoona, vijana wanahudumu katika Ofisi ya Rais, TAMISEMI. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na pongezi hizo kubwa kwa watendaji wote, *TARURA* pamoja na sekta zote ambazo nimezitaja, sisi katika Wilaya yetu ya Itilima tunayo mambo makubwa ambayo wameyafanya kupitia Sekta ya Elimu, Sekta ya Afya, Sekta ya Maji, maana Wizara hii ni mtambuka inaingilia maeneo yote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ninapongeza kwa kutuletea fedha shilingi bilioni 1.5 katika Kata ya Mwamapalala ambapo shule hiyo ya Amali imeshakamilika. Imebakia *process* chache chache ili tukamilishe na vijana waanze kupata elimu nzuri katika maeneo yetu haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili, tumejenga barabara. Katika kila Wilaya na katika Mkoa kuna barabara za kiuchumi ambazo zinaunganisha kutoka eneo moja kwenda eneo lingine. Mheshimiwa Naibu Waziri atakuwa shahidi kwa sababu amewahi kukaa katika Mkoa wetu wa Simiyu. Tunazo *centre* kubwa, *centre* ya Migato – Longalombogo, barabara ile ilikatika uchumi wa wananchi katia maeneo hayo unakatika. Ukikatika mwananchi haamini yale makubwa yaliyofanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba daraja hili nilishawahi kulizungumzia kwenye swali la msingi, Mheshimiwa Naibu Waziri alinijibu Daraja la Gamaloha – Longalombogo. Ni vema nikapata majibu kwa ajili ya wananchi katika maeneo hayo kutusaidia katia eneo hilo husika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili, Serikali imefanya mambo makubwa sana lakini tunalo tatizo kubwa ambalo lazima litafutiwe jawabu. Tatizo hilo ni kada ya afya kwenye suala la Utumishi. Tunatambua Serikali imefanya kazi kubwa na nzuri sana kuendelea kuleta watumishi, lakini bado mahitaji ni makubwa. Ninafahamu Sekretarieti ya Utumishi imetangaza ajira katika Wilaya yetu ya Itilima, lakini kulingana na uchache wake ninamwomba Waziri mwenye dhamana, ikiwezekana mambo mengine haya ayakaimishe kwa *RAS* kwenye Mkoa husika ili mambo yafanyike. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunayo magari mengi yamenunuliwa na Serikali ya Awamu ya Sita, chini ya Dkt. Samia Suluhu Hassan, tuna watumishi wa Kata na Vijiji ajira bado. Sasa hivi ni zaidi ya mwaka mzima walishatoa matangazo, lakini bado Sekretarieti haijaja kuratibu. Ninamwomba tu Waziri mwenye dhamana ikimpendeza, basi akaimishe pale kwa *RAS* Mkoa wa Simiyu, *RAS* yule ni mwanamama mchapakazi, ikimpendeza basi atoe kibali ili mambo hayo yaweze kufanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ni, tuna shule kongwe, niipongeze sana Serikali ya Awamu ya Sita jinsi gani walivyotusaidia. Niombe katika shule ambazo ni kongwe za muda mrefu, kuna Shule ya Linalo, Shule ya Gangabileli na Shule ya Zanzui zina wanafunzi zaidi ya 2,300 na kitu, sasa kwenye eneo hilo moja tunaendelea kuwabana watoto wetu, darasa moja linakuwa na zaidi ya watoto, tumekuwa na changamoto kubwa ya madarasa mmetuletea, lakini ni vizuri mkajaribu kutuongezea fedha, ili kusudi tuweze kupanua katika eneo hilo husika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaendelea kufanya mambo makubwa sana, lakini TAMISEMI ndio uti wa mgongo wa nchi hii, miradi mingi mikubwa inayofanyika yote ipo ndani ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Ombi langu ni TAMISEMI pamoja na Wizara nyingine zote ndio sehemu mojawapo ya kuwaunganisha wananchi na vijana katika maeneo yetu, tunafahamu vijana wanamaliza vyuo vikuu, wanamaliza sekondari, *form five* na *form six,* tunalo tatizo kubwa sana la ajira; ombi langu kwa TAMISEMI ni tumefanya mambo makubwa, lakini yanahitaji sasa vijana hawa ambao tumewapa elimu tuwatafutie njia mbadala, wakimaliza shule waendelee kupata kipato na kujiajiri wenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninazungumza hivyo kwa sababu gani; Serikali ya Awamu ya Sita ilitengeneza mazao ya kimkakati. Tupongeze sana Wizara ya Kilimo, kazi kubwa waliyoifanya zaidi ya vijana 2,000 wamewaajiri, lakini vijana hawa ningeendelea kutoa ushauri TAMISEMI kwa sababu, ndio *overall* na ndiyo *in charge* na ndiyo wanafanya kazi kwenye maeneo husika, ikiwapendeza, wale vijana wawachukue waingie kwenye

utaratibu wa TAMISEMI chini ya Wakurugenzi kwenye Halmashauri zetu kwenye mazao haya ya kimkakati. Tukifanya hivyo, kwanza kutakuwa na uzalishaji mkubwa. Pili, tutaongeza ajira na tatu vijana wataendelea kujipanga kifikra na kujiajiri wenyewe na vilevile tuelekeze nguvu nyingi kwenye TAMISEMI kwenye suala la uzalishaji wa kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tutazungumza sana humu ndani kuhusu ajira. Wote sisi ni mashahidi, ajira za watu wa tano zikitoka wanajitokeza vijana zaidi ya 500 mpaka elfu moja na kitu kwa hiyo, lazima tuna tatizo. Ni nini kifanyike?

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya TAMISEMI ilianzisha mpango mzuri sana wa neno lilikuwa linaitwa *ODOP (One District One Product)*. Maana yake ni walitengeneza viwanda vidogovidogo, viwanda vile vitasaidia kuongeza ajira, vitasaidia vijana kupata ujuzi na mwisho wa siku tutakuwa na Taifa ambalo siyo tegemezi kwenye nchi, kwa ajili ya kupata ajira Serikalini. Kwa hiyo, niwaombe sana TAMISEMI wafunue, wapanuke, ili kusudi mambo yao yafanane na mahitaji halisi yalivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi ukilinganisha miaka ya zamani na miaka ya sasa, wasomi walikuwa ni wachache na wananchi walikuwa ni wachache. Kwa hiyo, kijana msomi akimaliza shule lazima apate ajira, lakini sasa kulingana na mazingira tuliyonayo lazima Serikali, kupitia TAMISEMI maana ndiyo wasimamizi na ndiyo wenye watu, wayachukue haya wayafanyie kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunafahamu jitihada ambazo zinazofanyika ni kubwa, lakini ombi, kwa sababu sisi kazi yetu ni kuishauri na kuisimamia Serikali, hasa tunawashauri katika misingi, katika mazao yote ya kimkakati waongeze na taasisi ambazo zinasimamia ili waungane kiwe kitu kimoja, yale yanayopatikana yaweze kusaidia ajira kwa vijana wetu. Tusipofanya hivyo, tutakuwa na wimbi la kila siku ambalo likijitokeza tu, ajira ndogo watu wanajaa zaidi ya maelfu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumekwenda tumejaribu, Mheshimiwa Waziri wa Utawala Bora, siku moja nilikuwa namtania kwa nini umeamua kuweka *division* ya *zero* kuingiza kwenye Jeshi la Polisi? Akasema ni kwa sababu, hawa waliosoma wapo wengi sana na wao wakajaa tu. Kwa hiyo, ni lazima tuendelee kubadilika, wasoma *degree* wameshajaa vijijini, wanahitaji ajira; sasa TAMISEMI mnayo kazi ya kufanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kingine pamoja na kwamba, tuna mahitaji ya watumishi katika maeneo yetu ni vyema, hasa kwenye kada ya afya tumejenga zahanati, tumeongezewa vituo vya afya, katika mipango ya Wizara inavyokwenda tutakuwa ni watu wa kuzungumza kila siku, lakini majawabu hatutayapata. Niombe ikiwezekana, tuna vijana ambao wamepata ajira kwenye maeneo, wakaimishe kupitia utaratibu wowote wa kiafya waendelee kujitolea kupata ajira kwenye maeneo yetu husika. Tukifanya hivyo, itakuwa imetusaidia sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho, nimpongeze sana Mtendaji wa *TARURA,* amekuwa mstari wa mbele. Ninavyoongea hivi sasa kuna barabara tuliomba kupandishwa, ninavyozungumza timu ipo Mkoani Simiyu, Wilayani Itilima, inazungukia kuhakiki kisha kuchukua hizo barabara. Barabara hizo ni ya kutoka Lugulu – Laini – Nyangokolwa na kuna Barabara inayotoka Gambasingu inakwenda kutokea Mwanza, Magu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hizi zote tukizifungua, tunafungua uchumi, tutapunguza gharama ya usafirishaji, lakini sisi kwa sababu ni wa kulima wa mazao barabara zile zitakapokuwa zimeimarika muda wote wananchi watafanya biashara. Wahitaji wengi wataenda, kwa maana hiyo mazao yatapanda bei katika maeneo husika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja na ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Msongozi, wajiandae Mheshimiwa Noah Saputu na Mheshimiwa Ally Makoa.

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana kwa kunipa fursa ili niwe miongoni mwa wachangiaji katika Bajeti hii ya Wizara ya TAMISEMI ya mwaka huu 2025/2026. Bajeti ambayo, kimsingi ni nzuri sana ya kupigiwa mfano, ni bajeti ambayo inagharimu pesa za Kitanzania zaidi ya shilingi trilioni 11.

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kazi nzuri ambayo anaifanya, kimsingi ametuheshimisha Watanzania ndani ya nchi, nje ya nchi na hata duniani kote, anastahili pongezi na heshima kubwa sana. Vilevile, ninaomba nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI, Manaibu wake, pamoja na Wakurugenzi wote kwa namna ambavyo wamekuwa wakifanya kazi. Kazi ambayo wanaifanya usiku na mchana na kwamba, TAMISEMI sasa imetulia, ipo vizuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mkuu wangu wa Mkoa wa Ruvuma, Kanali Ahmed Abbas, kwa kazi nzuri anayoifanya. Mkuu wa Mkoa huyu anafanya kazi nzuri sana na ndiyo maana mnaona Mkoa wetu wa Ruvuma sasa unaendelea kusonga mbele kimaendeleo. Tunamshukuru sana na Mungu aendelee kumpa maisha marefu, aendelee kuwatumikia Wanaruvuma kadiri ambavyo anafanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze pia, *RAS* ambaye ni dada yetu Mary Makondo, Wakuu wa Wilaya wote, Wilaya ya Nyasa, Mbinga, Songea Vijijini na Mjini, Namtumbo na Tunduru, wote wanafanya kazi nzuri sana. Kongole nyingi sana kwao na halikadhalika, kwa Wakurugenzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mkurugenzi wa *TARURA*. *CEO* wa *TARURA* anafanya kazi nzuri sana, hongera sana. Ukiona kila Mbunge anasimama hapa anakupongeza maana yake unafanya kazi nzuri sana na tunaomba watu kama hao, wazalendo, wanaofanya kazi nzuri namna hii katika nchi yetu, wakati mwingine tuwafikirie kuwapa zawadi ili waweze kuwa na moyo zaidi wa kuitumikia nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukarabati; ninapenda sana leo nizungumzie suala la ukarabati, hasa kwenye hospitali ya Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga, katika mkoa wangu wa Ruvuma. Hospitali hii inahitaji kuendelea kufanyiwa ukarabati, hospitali hii uchakavu wake ulikuwa ni mkubwa sana, kwa hiyo, ninaomba Ofisi ya Rais, TAMISEMI waendelee kupeleka pesa, kwa ajili ya kufanya ukarabati wa hospitali hii ya Mbinga. Halikadhalika yapo maboma ambayo yamejengwa na nguvu za wananchi, lakini bado hayajakamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunahitaji vilevile maboma kwenye zahanati, yamejengwa, lakini hayajaezekwa. Nitumie nafasi hii kukuomba sana Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI, ili uweze kupeleka pesa katika zahanati ya Ukimo katika Jimbo la Mbinga Mjini, Zahanati ya Rudisha, Zahanati ya Lifakara na Zahanati ya Malangali. Nimwombe sana Mbunge, zahanati hizi hali yake sio nzuri, tunaomba kwa namna yoyote ile watusaidie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze sana Mbunge wa Jimbo la Mbinga Mjini kwa namna ambavyo amekuwa akifanya kazi kwa umahiri mkubwa, amekuwa mfuatiliaji, haachi hata nafasi moja, naamini kabisa Manaibu Waziri wanamuona kila siku ofisini kwenu. Halikadhalika na mimi, winga machachari, ambaye ninafanya kazi kwa Mkoa wa Ruvuma pia, nimekuwa nikifuatilia kuhakikisha kwamba, nguvu ya pamoja itatoa msukumo kwa TAMISEMI kutuletea pesa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii pia, nizungumzie Kituo cha Afya Lilambo katika Manispaa ya Songea. Kituo cha afya cha Lilambo katika Manispaa ya Songea hakina uzio, lakini bado kuna maboma ambayo yanatakiwa yakamilishwe. Niombe sana mazingira ya kituo hicho, ina maana kwamba, usalama wa kituo cha afya chenyewe bado ni mdogo; inawezekana kabisa ukatokea hata wizi wa hapa na pale.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na afya ya mtu; ugonjwa wa mtu ni siri, siyo mgonjwa analetwa pale, mtaani kote wanajua leo fulani kapelekwa pale hospitali. Ninaomba nichukue nafasi hii kutoa msisitizo. Halikadhalika katika Kituo cha Afya cha

Kata ya Ruvuma katika Manispaa ya Songea, nacho pia, kinahitaji majengo mawili ya wodi ya wanaume na watoto, ambayo bado pesa haijapelekwa, kwa ajili ya ujenzi huo. Niombe sana, halikadhalika uzio unatakiwa katika hospitali hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nichukue nafasi hii kuwasemea Shule ya Msingi Matalawe, nao pia, wanahitajia uzio, kwa ajili ya usalama wa watoto. Watoto wamekuwa wakitoka hovyohovyo kiasi kwamba, watoto wale wamekuwa wanapata matatizo, pikipiki zinapita hapo, usalama wao ni mdogo. Kwa hiyo, ninaomba sana Serikali izingatie kwa sababu, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan amefanya kazi nzuri sana ya kuweka miundombinu mizuri kwenye elimu na kwenye afya kwa hiyo, ninaomba sana uboreshaji wa miundombinu hiyo, kwa maana ya kuweka uzio, ili kuwe na usalama zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii pia, kuzungumzia nyumba za walimu; kuna umuhimu sana wa kuweka nyumba za walimu. Walimu wengine wanatoka mbali na imekuwa ni kisingizio kwamba, natoka mbali, wakati mwingine wanachelewa kufika shuleni, kwa ajili ya kufanya majukumu yao. Kwa hiyo, niiombe sana Serikali iendelee kufanya maboresho kwa kuweka nyumba za walimu katika Mkoa mzima wa Ruvuma.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ninaomba nizungumzie miundombinu ya barabara. Nichukue nafasi hii kuishukuru sana Serikali kwamba, katika Wilaya ya Namtumbo tuliweza kupata kilometa 1.8 ninaishukuru sana Serikali; kilometa 1.8 ni ya lami katikati ya mji. Kwa hiyo, nichukue nafasi hii kuiomba Serikali iendelee kutupatia lami zaidi kwa sababu, Mji wetu wa Namtumbo ukipelekewa lami ina maana kwamba, katikati ya mji patapendeza zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba vilevile nichukue nafasi hii kuzungumzia suala la stendi hapohapo Namtumbo. Tunaomba tupatiwe pesa kwa ajili ya ujenzi wa stendi mpya ya kisasa, ili sasa na sisi Wananamtumbo tuwe wa kisasa. Ninataka niwaambie Wananamtumbo wenzangu wawe watulivu wakati Serikali inaendelea kuchakata mambo haya. Ninataka niseme tu

kwamba, Wananamtumbo tupo vizuri na tutaendelea kuiunga mkono Serikali, lakini pia, tunaomba kwa mambo hayo na vipaumbele hivi tulivyoweka watusaidie ili tuweze kusonga mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba sasa nizungumzie Barabara ya kilometa 10 ya kutoka Majengo mpaka Subira, yenye urefu wa kilometa 11 katika Manispaa ya Songea. Barabara hii imeshaanza kujengwa kilometa moja kutoka Majengo mpaka pale Kata ya Ruvuma, niombe sasa kuelekea kule Ruvuma juu na hata kuelekea Subira tupatiwe pesa, ili tuweze kujenga hii barabara kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni imani yangu kwamba, kaka yangu Mheshimiwa Seif anasikia kilio changu. Nimekuwa nikimpigia simu mara kwa mara kumwomba barabara hii, sasa ikajengwe kwa kiwango cha lami kwa sababu. Barabara hii ni ya kimkakati, inaunganishwa na Barabara ya Songea Vijijini inayoenda Likuyufusi - Mkenda. Barabara hii imebeba vijiji vingi ambavyo vinafanya kazi ya kufanya maendeleo, hasa katika shughuli za kilimo, ninaomba sana barabara hii iweze kujengwa kwa kiwango cha lami. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mbinga Mpepai; nizungumzie sasa Barabara ya Mbinga – Mpepai yenye urefu wa kilometa 42. Barabara hii imejengwa kwa kiwango cha changarawe, tunashukuru sana, lakini kwa sababu ya umuhimu wa barabara hii na kazi kubwa inayofanyika na wananchi katika uzalishaji na umeona nazungumzia sana kuhusiana na suala la barabara kwa sababu, Mkoa wa Ruvuma ni mkoa wa uzalishaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia…

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kengele.

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie…

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa kengele ya pili hiyo. Kengele ya pili, lakini umependeza sana leo. *(Makofi)*

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, achia kidogo. Nakushukuru sana na naunga mkono hoja. *(Makofi/Kicheko)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ally Makoa, wajiandae Mheshimiwa Subira Mgalu na Mheshimiwa Mwantatu Mbarak Khamis.

**MHE. ALLY J. MAKOA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru kwa kunipatia nafasi ili niweze kuchangia kwenye hoja hii ya Wizara ya TAMISEMI. Ninamshukuru sana Mwenyezi Mungu kutufikisha hapa, nadhani ndiyo Bunge letu la mwisho la awamu hii, tunamwomba atujalie uzima, *Inshallah,* tutaonana tena awamu inayofuata.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kazi kubwa ambazo amezifanya kwenye Taifa hili, hususan kwenye Jimbo la Kondoa Mjini ambalo wananchi waliniamini na kunipa ridhaa ya kuwasimamia. Tunampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa sababu, amefanya *wonders* kwenye Jimbo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Kondoa ni miongoni mwa wilaya kongwe sana kwenye Taifa hili na muda mrefu kwa kweli, wilaya ile ilikuwa imebaki nyuma sana. Leo katika kipindi cha Awamu ya Sita mambo yaliyofanyika ni makubwa sana, ambayo tunasema kweli, sasa tunaanza kuiona wilaya kongwe ikiwa na thamani kubwa. Kwa hiyo, tunampongeza, tunamwombea kila la heri na afya njema Mheshimiwa Rais ili mitano mengine ijayo aweze kabisa kumalizamaliza vile vichache ambavyo vimebaki, kwa ajili ya manufaa ya watu wa Kondoa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, miradi iliyokuja ni mingi kwa kweli, hata kuielezea hapa itachukua muda mrefu sana. Ninachokiomba ni kwamba, kuna *gaps* chache ambazo zimebaki

kwenye hizi bajeti zetu ambazo tunaendelea nazo, tunamalizia bajeti hii ambayo tunaendelea nayo sasa hivi, tumeitekeleza kwa kiwango kikubwa sana yamebaki maeneo machache kabisa, ambayo tunaamini mpaka miezi hii miwili ikamilike, tutakuwa tumekwenda kumalizia. Ninaishukuru Serikali, kwanza kwa kuendelea kukubali mipango yetu kama halmashauri na kama jimbo, ya kuendelea kuitengeneza Wilaya yetu ya Kondoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaishukuru Serikali, baada ya muda mrefu sana wa kuomba tupatiwe ujenzi wa soko, stendi pamoja na barabara zetu za mjini kuwekewa lami, sasa tunaona Serikali imekwishakubali na tayari wapo wale wahandisi washauri kwenye jimbo wakiendelea na zoezi la kufanya kazi ya kuandaa *documents,* kwa ajili ya kuanza ujenzi wa soko la kisasa katikati ya mji, ujenzi wa stendi, pamoja na lami na taa za barabarani. Tunaishukuru sana Serikali kwa kukubali mpango huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa naongea na Mheshimiwa Waziri mwaka jana, kwamba, Kondoa imekuwa ni Wilaya ya muda mrefu sana, tunatamani sasa ipande hadhi, tutoke kwenye Halmashauri ya Mji twende kwenye Manispaa na alinieleza vigezo hivyo na mimi nikasimamia hapo. Kwa maana hiyo, sasa kwa maandalizi ya miundombinu hii kwa kweli, ninaishukuru Serikali, naitakia kila la heri na ninaamini kwa uchapa kazi wa Mawaziri; Mheshimiwa Mchengerwa na Manaibu Waziri wote wawili, jambo hili litakamilika kwa ukamilifu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninajua TAMISEMI wanafanya kazi kubwa sana na ninajua mambo haya yatakwenda kwa sababu, kwa mara ya kwanza nimeona TAMISEMI wanatekeleza bajeti waliyopangiwa na Bunge kwa kiwango cha hali ya juu sana. Kwa hiyo, ninawatoa hofu Wanakondoa Mji, waamini kwamba, Serikali hii ipo kazini na Mbunge wao yupo kazini, sasa tuna miezi sita tu ya wale wakandarasi washauri kufanya kazi ya kuandaa hizo *documents,* ili soko letu la kisasa lijengwe pamoja na barabara zetu za lami, kilometa saba na nusu na taa za barabarani. Kwa maana hiyo, mji ule sasa utapendeza na tutaendelea kuujenga upate hadhi, ili tuweze kuongezea kuupandisha hadhi kutoka halmashauri ya mji kwenda kwenye manispaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaishukuru Serikali kwa sababu, imekubali kuupanga vizuri mji wetu. Leo ule mji mvua ikinyesha maji huwa yanajaa barabarani na barabara zinageuka kuwa mito, sasa Serikali imekubali na tayari imeshawaleta wakandarasi washauri, kwa ajili ya kujenga mitaro mizuri kwenye barabara za mji, ambayo itakuwa na sifa ya kukusanya maji yote katika mji na kuyapeleka korongoni na hivyo kutunza barabara na hadhi ya mji.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaishukuru sana Serikali kwa kukubali kufanya uboreshaji wa barabara zetu za katikati ya mji. Tunaipongeza na tunaishukuru Serikali pia, kule Kingale tumeshaanza kujenga barabara kutia mitaro na kuimarisha barabara zetu. Kingale ni mji mkubwa ambao kwa kweli na wenyewe umekuwa ni wa muda mrefu. Tunatamani baada ya kuimarisha barabara kwa kutengeneza mitaro vizuri basi ninaamini tutaelekea kule kwenye barabara nyeusi za lami kwenye mitaa yetu ya halmashauri ya Mji. Kwa hiyo, ninashukuru sana kwa hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa afya, Serikali imefanya mambo makubwa sana. Mpaka hivi ninapozungumza tayari tuna vituo vya afya vitatu na tunakwenda kujenga kituo cha afya hicho cha mkakati ambacho tunaamini Mheshimiwa Waziri amesema mwisho wa mwezi huu atatuwekea fedha kwa ajili ya kujenga kituo cha afya hicho ambacho cha ni kimkakati na ambacho kitajengwa ndani ya Kata ya Kondoa Mjini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa maana hiyo, ninaiomba Serikali sasa, kile Kituo cha Afya cha Kolo kimaliziwe ile miundombinu ambayo bado haijakamilika; na kile Kituo cha Afya ya Mongoroma kule Serya kimaliziwe miundombinu ile ambayo bado haijakamilika na Kituo cha Afya cha Kingale nacho kimaliziwe miundombinu ili kiweze kutoa huduma ya afya vizuri kabisa kwa ajili ya kuwahudumia wananchi wa Jimbo la Kondoa Mjini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye upande wa elimu tumefanya vizuri sana, tunaishukuru Serikali. Tumekwishajenga

sekondari mpya mbili na tayari tumeanza ujenzi wa sekondari ya amali; *no,* tumejenga sekondari tatu mpya na sasa tunaendelea na ujenzi wa sekondari ya nne ya amali ambayo inajengwa kule Kingale. Kiukweli Serikali imefanya mambo makubwa na tunaishukuru. Tunaiomba sasa zile fedha ambazo bado hazijapelekwa basi zipelekwe ili tukamalizie ujenzi wa sekondari hii. Kwenye shule ya msingi tumebahatika kupata shule ya msingi mpya moja, lakini tumeboresha shule zetu zote za msingi kwa kujenga miundombinu ya kisasa sana, pongezi kubwa kwa Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba sasa Serikali kupitia TAMISEMI, kuna shule shikizi; unajua watoto wetu wadogo wanasoma wanatembea umbali mrefu sana. Kwa hiyo wananchi na Mbunge wao tuliamua kuanza kujenga shule shikizi ambazo kwa kweli mpaka sasa hivi tumefikia ujenzi wa takribani madarasa mawili mawili kwenye Shule Shikizi ya Usia, Shule Shikizi ya Kingale Chini, Shule Shikizi ya Serya na Shule Shikizi ya Tekule. Tumefikia ujenzi wa madarasa mawili mawili kwa sababu watoto wanatembea zaidi ya kilometa 10 kwenda kutafuta shule za misingi. Kwa hiyo, tukajipanga na wananchi tukamua tuanze kuwajengea shule kwenye mitaa yao. Kwa hiyo, tunaiomba Serikali kwa nguvu ile ile ambayo imeifanya katika miaka ya nyuma ku-*support* hizi nguvu za wananchi watuletee fedha sasa kwa ajili ya kuziimarisha hizi shule shikizi ili nazo zisajiliwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika awamu hii ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan tumeweza kusajili shule za msingi mpya tatu. Kwa hiyo tumeweza kuwaokoa wanafunzi ambao walikuwa wanakwenda kusoma mbali. Tunaishukuru sana Serikali kukubali kutusajilia hizo shule mpya tatu; ni jambo kubwa sana, Mungu awabariki Mheshimiwa Rais, Waziri pamoja na Manaibu Mawaziri wa TAMISEMI, bila kumsahau Mtendaji Mkuu wa TAMISEMI na Maafisa wote. Kazi zenu ni nzuri na Mungu atawabariki sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ombi la kipekee kabisa ninawaomba sasa Mawaziri watusaidie kutujengea Shule ya Msingi ya Mtaa wa Bolisa. Ule Mtaa wa Bolisa hauna shule ya

msingi, watoto wanatoka Mtaa wa Bolisa wanakwenda kusoma Mtaa wa Poisi. Hata hivyo watoto wanaosoma kule ni wengi. Kwa maana hiyo, ili kuwasaidia watoto wetu hawa tunaomba sasa, ombi maalum kabisa, tujengewe na shule ya msingi kwenye huu Mtaa wa Bolisa. Wazee wa Bolisa, akinamama na watoto watawashukuru sana kwa sababu wamekuwa wakiitafuta shule hii ya msingi kwa muda mrefu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa, hii Kata ya Bolisa ilikuwa ni kisiwa, ilikuwa na madaraja matatu yanahitajika yajengwe. TAMISEMI wametufanyia jambo kubwa sana, Mungu awabariki sana. Wananchi walikuwa wanatamani daraja lijengwe moja baada ya lingine kila mwaka; kwa maana hiyo tungetumia miaka mitatu kujenga haya madaraja. Kwa ufanisi mkubwa TAMISEMI wametusaidia, wameyajenga madaraja yote matatu. Leo akinamama wale walikuwa wanavuka maji kwa kunyanyua nguo zao juu sasa hawatanyanyua tena. Walikuwa wanavua viatu ili…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante.

**MHE. ALLY J. MAKOA**: Mheshimiwa Naibu Spika ninakushuru na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa nilimruka Mheshimiwa Noah. Mheshimiwa Noah, halafu baadaye atakuja Mheshimiwa Mgalu.

**MHE. NOAH L. S. MOLLEL:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia. Kwanza kabisa nianze kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema yeye ambaye ametupa uzima kwa siku ya leo na hata siku zilizopita. Pia, nianze kwa kumshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na Mheshimiwa Spika, Waziri Mkuu na Serikali nzima kwa jumla pamoja na Waziri wa TAMISEMI kwa jinsi ambavyo wanatekeleza majukumu yao, na Serikali nzima kwa ujumla wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hotuba yangu itajikita katika maeneo makuu mawili ambayo ni eneo la yaliyotekelezwa na eneo la yatakayotekelezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi hiki Serikali ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan imeweza kututekelezea miradi katika upande wa Barabara, hasa katika upande wa madaraja yaliyochukuliwa na mafuriko. Madaraja hayo ni Kiutu, Kiranyi, Seriani, Mnadani, Mwandeti na Bwawani; ni madaraja makubwa ambayo yaligharimu siyo chini ya zaidi ya shilingi bilioni 1.5. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika barabara zetu za Jimbo la Arumeru Magharibi, kuna changamoto kwa sababu jimbo langu lipo kwenye mwanguko wa milima, hivyo barabara nyingi ni mbovu. Barabara ya Malalua – Nduruma – Bwawani hali yake ni mbaya, pia Ngulelo – Sokoni II hali ya barabara ni mbaya, Kimandolu – Nyiresi – Sanawari – Oldonyosambu – Gomba *Estate* – Msitu wa Mbogo – Likamba – Mussa – Monduli – Kisongo – Mussa - Oljorobusi – Mateves – Likamba – Losikito – Lemanyata – Olkokola – Lemohoja – Olkejulenderit Tangasikiriet – Lengijave – Loyongo – Engalaoni – Kilima Moto – Mwandeti – Engalaoni na Barabara ya Olokii – Shambarai Burka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Ilani ya Chama Cha Mapinduzi katika Ibara ya 57, imeelekeza Serikali kutekeleza suala la miundombinu ili iweze kukaa vizuri. Barabara ni siasa na siasa ni barabara. Katika jimbo langu wananchi wanalalamika na tumekuwa tukipata sana adha kubwa tukiwa katika ziara mbalimbali. Hivyo, ninaomba Waziri wa TAMISEMI, Katibu Mkuu na Wizara nzima kwa ujumla wake waweze kutukumbuka, kwa sababu kwa kweli hali ya barabara katika Jimbo letu la Arumeru Magharibi siyo nzuri kama ambavyo nimetaja. Nimekuwa nikiwasiliana na Mawaziri, Manaibu Mawaziri, kuwatumia na meseji na *clips* mbalimbali ambazo wananchi wanalalamika wakidai barabara. Kazi nzuri imefanyika sana na Serikali yetu ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, hivyo kitu hiki kidogo kisituharibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, *TARURA* wanafanya kazi nzuri sana. Pamoja na kwamba hali ya fedha ni tata kidogo, lakini hicho wanachokipata wanafanya vizuri zaidi. Nimpongeze Ndugu Seff kwa sababu kila wakimpigia simu changamoto ya barabara amekuwa akitusaidia. Ninaomba sasa TAMISEMI itusaidie kuwaruhusu *TARURA* kwenye jimbo langu waweze kutangaza zile 40% za barabara ambazo zimebaki. Kwa sababu barabara nilizozitaja kama zikitangazwa hizo 40% hali itakuwa nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa afya kazi kubwa imefanyika. Tumejengewa vituo vya afya takriban vitano ambavyo ni Engalaoni, Oldonyosambu, Olorieni, Bwawani na Mateves. Hospitali ya Wilaya imeboreshwa kwa kuleta shilingi milioni 900 ambayo imejenga jengo ya *OPD,* jengo la maabara, jengo ya *mortuary* na jengo la *X-ray,* shilingi bilioni 900 hizo zimetekeleza kazi vizuri zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, maombi katika eneo hili. Hospitali hiyo haina wodi ya wazazi, haina wodi ya wanaume na pia haina wodi ya watoto. Hivyo tunaomba na jengo dhararu; kwa sababu hospitali ipo karibu na barabara ya Namanga, hilo jengo la dharura ni muhimu zaidi. Pia tunaomba umaliziaji wa maboma kwa sababu maboma mengi bado yapo hivyo tunaomba sana ili tuweze kumaliza maboma hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa elimu, tumepata shule tatu za sekondari. Tunashukuru sana Serikali ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, tumejengewa Sekondari ya Kiutu, Sekondari ya Moivo na Sekondari ya Ng'orilukul, zote zinagharimu zaidi ya shilingi bilioni 1.5. Shukurani hizo tunampa Mheshimiwa Rais na Serikali yake na kumpongeza kwa dhati kabisa kwa sababu imekuwa ikiwahudumia wananchi wa sehemu kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba basi kwa upande wa elimu kuwe na ukarabati wa shule kongwe. Kuna shule kongwe katika Jimbo la Arumeru Magharibi ambazo zimechakaa mno. Niombe basi katika ukarabati zikumbukwe za Shule za Sambasha ambayo imekuwa ni chakavu sana Kiseriani na Nduruma katika shule mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaendelea kumtia Mheshimiwa Rais moyo na kumpongeza kwa kazi kubwa anayoifanya kwa sababu anastahili. Hivi karibuni kumekuwepo na baadhi ya watu wakisema Bunge linampongeza Mheshimiwa Rais na wao hawaelewi kwamba kwa nini, wanampongeza. Hata nyuki wana malkia wao, nyuki wanapokuwa na malkia wanamtunza na kumlinda ili kuhakikisha kwamba ile jamii ya nyuki inaendelea kustawi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hata sisi leo kama Wabunge lazima tumlinde Mheshimiwa Rais wetu na kumtetea na kumjengea ujasiri wa kuweza kutuhudumia. Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ni malkia wetu ambaye tunaendelea kumtetea na kumtia moyo ili aweze kutuhudumia vizuri na kuhudumia Taifa letu vizuri. Kiongozi akiishi kwa wasiwasi hawezi kufanya majukumu yake vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna nchi ambazo zimekuwa na malkia wao na wamekuwa wakiwalinda. Kwa mfano *Queen* Elizabeth wa Uingereza, Cleopatra wa Misri, *Queen* Nzinga wa Angola, Angela Merkel, Indira Gandhi wa India, na Ellen Sirleaf wa Liberia.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninayasema haya kwa sababu kumekuwepo na watu baadhi wanasema kwa nini, mnapongeza Mheshimiwa Rais. Kuna kila sababu ya kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa sababu anafanya kazi na ameonesha kwamba anaweza na ameweza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi karibuni pia nimemsikia mwanazuoni mmoja ambaye ni mtu wa thiolojia akisema wanasema tu Mheshimiwa Rais amefanya lakini je, ngoja tuwasubiri sasa na wao watuambie hao Wabunge wamefanya nini. Ninachotaka kusema ni kwamba, hakuna Ilani, Ilani ni moja tu; Ilani inayotekeleza na Mheshimiwa Rais, Ilani inayotekeleza na Waheshimiwa Wabunge ni Ilani moja tu. Sisi kwenda kuelezea kwamba kimefanyika nini na ni nani amefanya ni wajibu wetu kama wanasiasa ambao tuna uwezo wa kueleza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Waziri Mkuu anayeitwa Winston Churchill ambaye aliwahi kusema; ninaomba kunukuu, "*A Politian needs the ability to foretell what is going to happen tomorrow next week, next month and next year and to have the ability afterward to explain why it don't happen.* Kwa hiyo, ninachotaka kumaanisha hapa nini, ninataka kusema ni kwamba kuendelea kuelezea kuhusu Mheshimiwa Rais amefanya nini ni wajibu wetu na ni jukumu letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo, niiombe Serikali, Mheshimiwa Mchengerwa ananisikia na Manaibu wako, Mheshimiwa Waziri Mkuu ananisikia na Serikali nzima kwa ujumla. Ninaomba chonde chonde, mambo mengi yamefanyika kwenye Jimbo la Arumeru Magharibi, lakini kinachoniletea changamoto kwa sasa ni jambo moja tu barabara, barabara, barabara.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba sana na niseme kwamba ninaunga mkono hoja na niombe sana anikumbuke kwa sababu hali yangu ni tete. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Mgalu, wajiandae Mheshimiwa Mwantatu Khamis na Mheshimiwa Leah Komanya.

**MHE. SUBIRA K. MGALU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia bajeti ya Ofisi hii ya Rais, TAMISEMI. Kwanza, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupa afya njema inayotuwezesha leo kukutana humu Bungeni. Pili, nimshukuru Mwenyezi Mungu pia kwa kuniwezesha kuchangia Ofisi ya Rais, TAMISEMI nikiamini ikiwa ni bajeti ya mwisho kwa muhula huu wa Bunge la Kumi na Mbili. Mimi nimekuwa nikiichangia Wizara hii kwa sababu Wizara hii imefanya kazi nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kumpongeza sana Rais, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, nimpongeze kaka yangu Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Mchengerwa, Mheshimiwa Naibu Waziri mdogo wangu Mheshimiwa Zainab, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara hii pamoja na watendaji wote wa ngazi za Mikoa, Mkuu wangu wa Mkoa Alhaji

Kunenge, Katibu Tawala wetu Wakuu wa Wilaya wote wa Mkoa wa Pwani, Wakurugenzi wote Mabaraza ya Madiwani kwa kazi nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nianze kwa kunukuu, nukuu ya Mheshimiwa Waziri Mchengerwa kwenye bajeti hii ukurasa wa 139; kwamba TAMISEMI haitafuti sifa ya kisiasa tunatafuta suluhisho sahihi kwa maisha ya Mtanzania wa kawaida; mwisho wa kunukuu. Ninaungana na nukuu ya Mheshimiwa Waziri na nimpongeze kwa kazi nzuri ya kutafuta masuluhisho ya changamoto za wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa Mkoa wetu wa Pwani kipekee nimpongeze kupitia taasisi yake ya Mfuko wa Barabara *TARURA* kwa kazi nzuri iliyofanya, hasa kwenye maeneo yenye changamoto kubwa. Maeneo ya visiwani wamejenga Daraja la Mbuchi, haijapata kutokea, zaidi ya shilingi bilioni saba. Leo Mwanarufiji, Mwanakibiti anatoka Dar es Salaam moja kwa moja mpaka Mbuchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna kazi inayoendelea ya ujenzi wa Daraja la Bibi Titi Mohamed kwa ajili ya kudhibiti mafuriko ya Muhoro. Tangu tupate uhuru haijapata kutokea; daraja ya shilingi bilioni 11. Kuna daraja la Mbambe daraja shilingi bilioni 24 linajengwa. Kwenye Wilaya ya Rufiji kuna kazi nzuri haijapata kutokea ya kutatua suluhisho yanatukabili kwenye miundombinu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kana kwamba haitoshi, bajeti ya Wizara hii kutoka shilingi trilioni saba mwaka 2020/2021 mpaka shilingi trilioni 11 inayoombwa leo. Haijapata kutokea, ni historia katika bajeti zote za Wizara hii. Ni jambo kubwa la kuonesha utayari wa Mheshimiwa Rais wa kutatua changamoto za wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kana kwamba haitoshi ninampongeza Mheshimiwa Waziri, ameweza kusimamia bajeti kubwa ya Wizara hii ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI. Kwa mfano, mwaka huu 2023/2024, Taarifa ya CAG imeonesha kwamba

halmashauri zote 184 zimepata hati zinazoridhisha, hakuna hati yenye shaka hata moja. Kwa hiyo ni wazi inaonesha kwamba wamesimamia vizuri matumizi na mapato ya Wizara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kana kwamba haitoshi, mimi binafsi nimeshiriki ziara ya UWT Taifa chini Mama Mary Chatanda na Mama Shomary tumezunguka Kata 1,058. Hakuna Kata wala Kijiji ambako hatukuona miradi ya maendeleo. Tumeona miradi 1,130 yenye thamani ya shilingi trilioni 1.2. Yote hayo yanaonesha namna gani TAMISEMI wamejipanga katika kushughulikia changamoto za wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo ninataka nieleze tu changamoto moja tu; nimwombe Mheshimiwa Waziri; kwanza Mkoa wetu wa Pwani tunashukuru kupata Manispaa; haijapata kutokea. Tuna makao makuu leo yenye Manispaa ya Kibaha; ahsante sana. Tunashukuru kwa Halmashauri ya Mji wa Rufiji.  Ahsante sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niombe kwenye miundombinu, ninataka nimwombe aangalie jitihada za wananchi. Ipo Kata yetu ya Mapinga, Bagamoyo yenye wananchi takribani 40,000 lakini ipo vitongoji. Kwa mfano, Kiembeni, Kiharaka, Tungutungu, Kwa Kibosha, Kimele Changwafedha; hivi vitongoji mara zote vinachanga michango ya wananchi kwa ajili ya ukarabati wa miundombinu. Tumeona wananchi wakichangia ukarabati au ujenzi wa madarasa, ujenzi wa maboma ya maabara; na kipekee kwa wananchi hawa ni kwamba wanachangia ukarabati wa miundombinu. Tulipata kuchangia na hata Mbunge wa Jimbo letu la Bagamoyo aliomba Barabara ile ya Mingoi – Kiembeni ipandishe hadhi kwenda *TANROADS. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba *Engineer* Seff ambaye tumempongeza kwa kazi nzuri anayofanya, nimwombe kwa zile fedha za dharura kuweza kuwasaidia wananchi hawa kwa kadri wanavyoendelea na jitihada za kujichangisha kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya barabara na lile daraja ambalo linaunganisha au linaunganisha Mkoa wa Dar es Salaam na Wilaya ya Bagamoyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo tunashukuru kwa shilingi bilioni 32 za ukarabati na ujenzi wa miundombinu ya elimu. Tunashukuru shule ya wavulana ya shilingi bilioni 4,000,000,000 inayojengwa Mkuranga. Tunashukuru shule ya wasichana ya Bibi Titi Mohamed iliyojengwa Rufiji. Tunashukuru shule nne za amali zilizojengwa Halmashauri ya Rufiji, Halmashauri ya Bagamoyo, Halmashauri ya Chalinze na Halmashauri ya Mafia. Ni kwa mara ya kwanza zinajengwa Shule za Mafunzo ya Amali ili kusaidia vijana wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninataka niseme kwamba tunapompongeza Mheshimiwa Rais, tuna kila sababu kwa sababu Mheshimiwa Rais ndiye Amri Jeshi Mkuu. Mheshimiwa Rais kupitia Baraza lake la Mawaziri ndiye anayeidhinisha fedha anayeelekeza maono yake. Tumeona Awamu ya Sita imeelekeza maoni yake katika kutatua changamoto za wananchi. Tunamshukuru na kumpongeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, chanda chema huvikwa pete. Amevunja rekodi ya kutenga fedha Wizara hii ya TAMISEMI. Amevunja rekodi ya Serikali kupeleka fedha za maendeleo kutoka 60% mwaka wa fedha 2019/2020 ya fedha za maendeleo zinazotengwa kupelekwa kwenye Halmashauri za Serikali za mitaa mpaka 95% kwa mwaka wa fedha 2023/2024; ni hatua kubwa ya maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mpaka sasa Mkoa wetu wa Pwani kwenye fedha za maendeleo tumepitishiwa shilingi bilioni 51 mwaka wa fedha unaoendelea na tulikwishakupokea 85% mpaka mwezi Aprili. Ni wazi kwamba kazi hii nzuri maana yake kuna kutenga fedha, lakini kuna kuzipelekea fedha kwenye miradi ya maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninataka nimalizie kwa kusema, kwa kweli namba hazidanganyi. Fedha zinazopelekwa halmashauri zetu, Wizara yako imepata hati safi, taasisi zinazosimamia zimepata hati safi, haijawahi kutokea; na zinafanya kazi iliyokusudiwa kwa sababu tunaziona, vituo vya afya tumeviona, shule nyingi tumeziona, yote hayo ni rekodi

zilizowekwa na Serikali ya Awamu ya Sita kwa mara ya kwanza imefanya kazi nzuri, ya kupigiwa mfano na haina mashaka yoyote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wanaoshangaa kwa nini tunampongeza Mheshimiwa Rais; tunampongeza kwa maono yake, kwa utayari wake, kwa sababu baadhi ya fedha zilizofanya maendeleo ni zile ambazo amezitafuta kupitia diplomasia yake. Hizi shule zilizojengwa kwa *Boost,* zilizojengwa kwa amali, zilizojengwa kwa fedha mbalimbali, ni kutokana na jitihada zake kuongezea kwenye mapato ya ndani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninamshukuru Mheshimiwa Waziri, amefanya kazi nzuri, miongoni mwa Mawaziri wa TAMISEMI waliopambana yeye ni mmojawapo; na ameweka rekodi ya kufuatilia, kusimamia na kuhakikisha matokeo chanya yanapatikana. Ninawapongeza na ninawashukuru sana. Sisi wametupa ajenda; alisema hatutafuti umaarufu wa kisiasa, lakini utekelezaji huu wa Ilani ambao ameuchambua vizuri ametupa nafasi sisi wawakilishi tumejivunia, tumefanya kazi na tumetembelea miradi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi binafsi ninamshukuru Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi yake nzuri, imeniwezesha kutembea nchi nzima, kupata miradi mingi, kuona na kuamini; na pia ambayo nitatumia kusimama kwenye majukwaa kumwombea kura za kishindo Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan na mgombea mwenza Dkt. Emmanuel Nchimbi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli Serikali imetenda, ni Serikali ya vitendo na *data* tunazo. Tukutane *site* kwa kazi inayoendelea. Ahsante sana kwa nafasi uliyonipa. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Sasa ninamwita Mheshimiwa Mwantatu Mbarak Khamis, jiandae Mheshimiwa Komanya.

**MHE. MWANTATU MBARAK KHAMIS:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii ili kuweza kuchangia bajeti hii ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI kwa mwaka wa fedha 2025/2026.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote kwanza ninachukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake nzuri ambayo imeeleza mambo ya msingi ambayo yanaenda kutekelezwa kwa lengo la kuwaletea Watanzania maendeleo. Aidha, ninawapongeza wasaidizi wa Mheshimiwa Waziri wakiwemo Manaibu Waziri, Katibu Mkuu na wasaidizi wake pamoja na watendaji wake wote wa Ofisi ya Rais, TAMISEMI. Bila kuwasahau Waheshimiwa Wakuu wa Mikoa, Waheshimiwa Wakuu wa Wilaya pamoja na Wakurugenzi wa Halmashauri ambao wamekuwa wakifanya kazi kubwa ya kuhakikisha wanasimamia miradi inayotekelezwa kwa kuhakikisha fedha ambazo zinapelekwa katika halmashauri zinatumika kama ilivyokusudiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee kabisa ninampongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa aliyoifanya na ya mfano ya kutekeleza Ilani na kuleta maendeleo makubwa Tanzania. Vilevile, kwa kuhakikisha huduma muhimu zinawafikia wananchi; na kuhakikisha kwamba katika Awamu hii ya Sita amani na utulivu ndiyo jambo la msingi ambalo litatawala katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi mwenyewe nikiwa Mjumbe wa Kamati ya TAMISEMI, nimeshuhudia mambo mengi ambayo yametekelezwa kwa kipindi hiki, lakini mambo yenyewe katika Hotuba ya Mheshimiwa Waziri ameyaeleza. Tumetembelea miradi mbalimbali kupitia Kamati na tumeshuhudia miundombinu mizuri ya afya, elimu, barabara pamoja na kuona utekelezaji wa fedha za mikopo isiyo na riba ya 10%. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaanza kwa kuzungumzia miundombinu ya afya. Mheshimiwa Rais Samia ameweza kupeleka fedha nyingi katika halmashauri kama ambavyo Waheshimiwa Wabunge ambao wanatokea katika halmashauri

hizo wameeleza. Fedha hizi zimekwenda kuondoa changamoto ambazo wananchi walikuwa wakizipata kwa kufuata huduma ya afya katika maeneo ya mbali na makazi yao. Kuimarika kwa huduma hizi zimekwenda kupunguza ama kuondoa kabisa changamoto walizokuwa wakipata akinamama wakati wanapoenda kujifungua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa akinamama wameondokana na ile kadhia ya kujifungulia njiani kutokana na kuboreshwa huduma hizi za afya katika vijiji na halmashauri zetu. Pamoja na utekelezaji huo mkubwa ambao umefanyika, lakini bado kupitia bajeti hii Mheshimiwa Rais ameweza kutenga fedha kwa ajili ya kujenga hospitali za halmashauri, vituo vya afya na zahanati, lakini pia inakwenda sambamba na miundombinu ya kuhakikisha huduma hizi zinatolewa kwa ufanisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hayo yote, pamoja na miundombinu mizuri ambayo imewekwa, ninawaomba watumishi wa huduma za afya watoe huduma nzuri kwa wananchi ili lile lengo la Mheshimiwa Rais liweze kutimia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu mwingine nitagusia suala zima la elimu. Kupitia Kamati ya TAMISEMI nimeshuhudia miradi mingi ya ujenzi wa shule za msingi na sekondari zikiwemo shule za sekondari za wasichana. Ujenzi wa shule hizi unalenga kuhakikisha ufaulu wa wanafunzi unaongezeka, lakini pia kuhakikisha wanafunzi wa kike wanafaulu vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na bajeti ambayo imekwenda kujenga shule, lakini bado fedha nyingine zimepelekwa katika bajeti hii ambayo tunaijadili ambayo inaenda kujenga vyumba vya madarasa, shule mpya nyingine zitajengwa, mabweni na mabwalo, lakini pia zinakwenda kuimarisha mfumo wa TEHAMA kwa shule mbalimbali zilizopo katika halmashauri. Kutokana na uwekezaji mkubwa uliofanywa na Mheshimiwa Rais katika Sekta hii ya Elimu, ninawaomba wazazi na walimu kila mmoja atimize wajibu wake ili lengo lililokusudiwa liweze kufikiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nikizungumzia Sekta ya Miundombinu ya barabara, ninaungana na Waheshimiwa waliotangulia kwa kuipongeza *TARURA*. Kwa kweli *TARURA* imefanya kazi kubwa sana na kutokana na changamoto iliyojitokeza kwa kweli miundombinu mingi imeharibika, lakini Serikali haikuishia hapo ilitoa fedha ya dharura shilingi bilioni 84.35 kwa lengo la kufidia ile athari iliyojitokeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee kabisa ninachukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mchengerwa kwa ubunifu wake wa kuhakikisha barabara za vijijini zinaendelezwa. Mpango wa hati fungani ambao ameubuni Mheshimiwa Waziri ni mpango mzuri ambao unaenda kuwakomboa wakandarasi wenyeji kwa sababu walikuwa na changamoto kubwa ya upatikanaji wa fedha, lakini kupitia mpango huu wa hati fungani wataweza kupata fedha kupitia benki na wataweza kutekeleza majukumu ya kiusahihi kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie mikopo ya 10%, mikopo ya 10% imetekelezwa lakini bado ina changamoto kama walivyoendelea kuzungumza Waheshimiwa waliotangulia. Nikizungumzia 10% ninazungumzia wanawake asilimia nne, vijana asilimia nne, asilimia mbili inaenda kwa watu wenye ulemavu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto iliyopo, bado watu wenye ulemavu hawajapata huduma hii kama inavyostahiki. Kuna baadhi ya halmashauri hawakuthubutu hata kukopesha mtu mmoja mwenye ulemavu. Kwa kweli hii inasikitisha, sitaki kuamini kwamba katika halmashauri hakuna mtu mwenye ulemavu ambaye ana uhitaji wa mikopo hii. Kwa hiyo, ninaomba sana Wakurugenzi wa Halmashauri wakalifanye vyema suala hili ili na wao waweze kufaidi matunda ambayo yanaletwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa, ninawaomba Watanzania wenzangu kutokana na kazi kubwa zilizofanywa na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt.

Samia Suluhu Hassan, ninawaomba tena tuthamini kazi kubwa ya mfano…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa ahsante kwa mchango mzuri.

**MHE. MWANTATU MBARAK KHAMIS:** …iliyotekelezwa na Rais. Wananchi wamuunge mkono Mheshimiwa Dkt. Samia Oktoba, 2025 kwa kumpa kura za heshima ili aweze kumaliza majukumu yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Komanya, wajiandae, Mheshimiwa Ndulane na Mheshimiwa Rweikiza.

**MHE. LEAH J. KOMANYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru kwa kunipatia nafasi hii ili niungane na wenzangu kuunga mkono hoja iliyopo mbele yetu nikimpongeza Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI pamoja na Manaibu wake kwa kazi nzuri wanazozifanya pamoja na watendaji wote wa Wizara ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba niungane na wenzangu kumpongeza Mheshimiwa Rais wetu kwa kazi nzuri aliyoifanya ya kutuletea maendeleo katika nchi yetu lakini pia hususan katika Jimbo la Meatu. Kazi kubwa sana imefanyika na wananchi wa Jimbo la Meatu wamemwelewa Mheshimiwa Rais. Nitoe mfano mdogo tu, katika uhamasishaji wake wa matumizi ya gesi, Jimbo la Meatu mwitikio umeonekana ni mkubwa kutokana na majiko ya ruzuku yaliyoletwa. Kulikuwa kuna foleni kubwa ambayo sijawahi kuishuhudia wakihitaji kununua majiko ya gesi yenye ruzuku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyoshauri kwenye swali dogo, kaya nyingi zinahitaji majiko haya, lakini majiko haya yalipokuja yaligawiwa kwa ku-*base* na namba ya *NIDA* ambapo ilisababisha familia moja kupata jiko zaidi ya moja, lakini kaya

nyingi zilikosa. Kama tutatumia Wenyeviti wetu wa Vitongoji kugawa majiko haya kwa kupitia kaya, kaya nyingi zitanufaika kwa matumizi ya gesi na wananchi wengi watanufaika sana. Hii imekuwa ni kero na hoja ninapokwenda kwenye mikutano ya hadhara, katika kata mbalimbali; wanahitaji wapelekewe majiko ya gesi ya ruzuku yanayotolewa na mama yetu, Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nikijikita kwenye bajeti iliyopo mbele yetu, kazi nzuri imefanyika kwa upande wa barabara. Kabla ya *TARURA* kuboresha tozo, Jimbo la Meatu lilikuwa linapokea shilingi 500,000,000 tu kwa mwaka kwa ajili ya ukarabati wa barabara ambayo ilikuwa ni 30% ya Mfuko wa Barabara. Nimpongeze mama yetu Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kwa kuridhia kutoa tozo kwenye mafuta ambapo tuliongezwa shilingi 1,500,000,000 barabara nyingi zimefunguliwa katika Jimbo la Meatu, madaraja madogo madogo yamejengwa na kupunguza adha iliyokuwa inawakabili wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nishukuru kwa bajeti tuliyoipitisha ya ziada ya shilingi bilioni 945, tayari fedha zimeanza kupelekwa *TARURA*, wakandarasi wetu wameanza kulipwa angalau wameanza kuendelea na kazi na wamerudi *site* kwa ajili ya kuendelea. Ninaomba niwahakikishie wananchi wa Meatu barabara nilizoziahidi kupitia *TARURA* zitafunguliwa na kwenye maeneo korofi zinaendelea kukarabatiwa, tayari wakandarasi wapo *site*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimwombe Waziri Mheshimiwa Mchengerwa, tunayo ahadi yetu ya Daraja la Mto Mwamanongu ya shilingi bilioni 7,500,000,000 ambayo ilishafanyiwa upembuzi yakinifu, kama alivyoniahidi hivi karibuni kwamba atatupatia fedha ili ujenzi uanze. Nimwombe mtani wangu, nimeshamweleza mengi kuhusu Jimbo langu, sitakuwa na deni tena kwenye upande wa barabara, sitamwomba kitu kingine, ninaomba atusaidie sasa fedha kidogo lile daraja lianze kujengwa. Ninashukuru hadhi za barabara zinaendelea kupandishwa, ninavyoongea wataalam wapo *site* kutoka Wizara ya

Miundombinu wanafuatilia upandishaji hadhi wa barabara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nikienda Sekta ya Elimu, tumepata kituo cha ufundi cha *VETA* ambacho ujenzi wake ulikuwa umesimama, lakini kupitia fedha za nyongeza za bajeti tayari ujenzi unaendelea na utakamilika hivi karibuni. Tumepokea shilingi 1,600,000,000 kwa ujenzi wa awamu ya kwanza ambao utakamilika na wanafunzi wataanza. Niombe tu *ALAF* watupelekee mabati kwa sababu ndiyo wanaotuchalewesha kwa sababu ninafahamu wameshalipwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati awamu ya sita inaingia madarakani, Jimbo la Meatu lilikuwa lina shule za kidato cha tano mbili ambazo hazikuwa zimeboreshwa. Ninavyoongea sasa hivi tunaenda kupata shule tano zenye hadhi ya kidato cha tano na sita zikiwa zimeboreshwa. Ninaomba, Shule ya Lyusa ambayo tumepelekewa madarasa ya kidato cha tano na sita, tupelekewe mabweni kwa sababu tunategemea ongezeko la ufaulu kwa 100%, kwa hiyo wanafunzi wengi watatakiwa kwenda katika shule zetu hizi ambazo tumezifungua kuwa za *A-level*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tumejenga shule sita mpya za sekondari katika Jimbo la Meatu, shule nne zikiwa za fedha za *SEQUIP*, shule mbili zikiwa za michango ya jamii pamoja na wawekezaji. Niombe, shule ya kwanza na ya pili tulijenga kwa *Force Account,* shule hizo zilienda vizuri. Jimbo la Meatu shule yetu ilikuwa ya pili katika Kanda ya Ziwa kuwa ya ubora; na Shule ya Mwanhuzi hivyo hivyo. Tulipoingia kwa mkandarasi zile shule mbili za sasa hivi, mambo mabaya yalitokea, tukavunja mkataba, tukamweka *local* fundi, sasa hivi kazi inaenda vizuri; lakini Waziri atusaidie, yule mkandarasi tuliyemtoa tunamdai shilingi milioni 82 atatukwamisha kukamilisha hizi shule mbili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini tunaomba hizi shule nyingine katika Kata ya Mjini Mwanhuzi kwa sababu kuna ongezeko la udahili wa wanafunzi. Kwa hiyo, kutakuwa na msongamano mkubwa katika Kata ya Mwanhuzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tumepokea pia fedha kwa ajili ya Shule mpya ya Msingi ya Bomani, tukapunguza msongamano uliokuwepo katika Shule ya Msingi Mwanhuzi; lakini tuna upungufu wa walimu na nyumba za walimu. Tuna maboma ya shule za msingi 90 ambayo hayajakamilishwa; kwa sekondari hatudai maboma yoyote kwa vyumba vya madarasa. Kwa hiyo, fedha za maboma kwa Jimbo la Meatu upande wa elimu zielekezwe katika maboma ya shule za msingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, upande wa afya kazi nzuri imefanyika. Tunalo ongezeko la upatikanaji wa dawa, mwezi uliopita 96% ya upatikanaji wa dawa katika Jimbo la Meatu. Huu ni ukweli usiopingika, hata ukiwafuata wauza dawa kwenye *pharmacy* zetu, wengi wanakiri biashara yao imeshuka kutokana na Serikali kupeleka dawa katika hospitali zake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tumepunguza vifo vitokanavyo na uzazi, tulikuwa tuna vifo vitatu hadi vitano, sasa hivi tuna kifo kimoja kwa robo au hakuna na vifo vingine vinatokea kwenye jamii. Kazi nzuri ya kupunguza vifo vitokanavyo na uzazi imefanywa na Mheshimiwa Mama Samia, tumepokea *ambulance* mbili katika wilaya yetu, Hospitali ya Wilaya ya Meatu. Tumepokea shilingi milioni 900 kwa kuanza ujenzi wa hospitali ya wilaya, kwa sababu hospitali tuliyokuwa tunaitumia ilikuwa ni ya hadhi ya Kituo cha Afya cha Mwanhuzi. Ila nikuombe Mheshimiwa Waziri kwenye mwaka huu wa fedha, hatujatengewa fedha yoyote…*(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Leah ahsante kwa mchango mzuri. Mheshimiwa Ndulane, wajiandae Mheshimiwa Rweikiza na Mheshimiwa Minza Simon.

**MHE. FRANCIS K. NDULANE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika Bajeti ya Wizara ya TAMISEMI siku ya leo.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, napenda kumshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa anayoifanya ya kuisimamia nchi na kuhakikisha kwamba miradi mbalimbali inatekelezwa kwa ufanisi mkubwa hasa ile ambayo inalenga katika kutatua changamoto au huduma za kijamii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeona miradi mingi ya afya, elimu, kilimo, mifugo na mingineyo imefanyika katika majimbo yetu nchi nzima na ambayo imekwenda kwa ufanisi mkubwa na kutatua kero na changamoto mbalimbali ambazo zilikuwepo nyuma miaka minne iliyopita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, nachukua nafasi hii kumpongeza na kumshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu ambaye jana alituongoza kuweza kutembelea katika barabara yetu inayotokea Kibiti – Lindi mpaka Mingoyo. Kwa hakika ziara ya jana ilikuwa na mafanikio makubwa, ambapo Mheshimiwa Waziri Mkuu wetu alitoa miongozo na maelekezo ya namna ambavyo Serikali inashughulikia changamoto ya barabara hiyo pale Somanga, Matandu na Njia Nne. Tunamshukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, napenda kuwapongeza Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI, Mheshimiwa Mchengerwa; Naibu Waziri, Mheshimiwa Dkt. Dugange; na Naibu Waziri, Mheshimiwa Zainab Katimba kwa kazi kubwa ambayo wanafanya katika kuhakikisha kwamba wanaisimamia Wizara hii kwa ufanisi mkubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, leo nina mambo mawili ya kuzungumza. Jambo la kwanza ni suala la barabara za vijijini. Jimbo letu la Kilwa Kaskazini, Jimbo la Kilwa Kusini na Jimbo la Rufiji, ni miongoni mwa majimbo ambayo yameathiriwa kwa kiasi kikubwa na mvua za *El-Nino* na Kimbunga Hidaya mwaka 2024 na hivyo imesababisha miundombinu ya barabara kuwa katika hali mbaya sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, yale maji ambayo yanaonekana kila mara yanakata barabara zetu za pale Somanga – Njia Nne,

hii ndiyo niliyoizungumzia ya Kibiti kwenda mpaka Lindi – Mingoyo, yanatokana na maji ambayo yanatoka kwenye Pori la Akiba la Selous pamoja na kwenye Milima ya Matumbi, ambayo yamekuwa yakitiririka mara kwa mara na kila siku yamekuwa yakiathiri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, huko yanakotoka yanapita kwenye vijiji zaidi ya 100 vilivyopo hapo katikati na hivyo kufanya barabara za huko ndani zote kuwa hazipitiki kabisa. Hadi kufikia mwishoni mwa mwaka huu, hali ilikuwa mbaya zaidi na nililazimika kuwasiliana na wewe Mheshimiwa Waziri, kuomba msaada wa fedha za kutosha ili zile barabara muhimu angalau ziweze kufunguliwa. Pia, miradi mingine ya ujenzi wa shule, ujenzi wa madarasa, iliyokuwa imekwama ya ujenzi wa shule, madarasa...

**MHE. MAIMUNA A. PATHAN:** Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa.

**MHE. FRANCIS K. NDULANE:** ...ujenzi wa visima vya maji na kadhalika iweze kushughulikiwa. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ndulane, kuna taarifa.

**MHE. FRANCIS K. NDULANE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

**TAARIFA**

**MHE. MAIMUNA A. PATHAN:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpa taarifa mzungumzaji wa sasa, kila mwaka maji yanapindukia kwa juu ya ile barabara. *Solution* ya pale ni kuweka daraja ambalo litainuka juu, liwe kama *flyover*. Wakituwekea hivyo, ndiyo itakuwa *solution* kwa barabara ya Kusini, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Haya, kwenye *CV* tutaongeza *engineering*. Mheshimiwa Ndulane.

**MHE. FRANCIS K. NDULANE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naipokea taarifa yake kwa mikono miwili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, barabara zote ndani ya Jimbo la Kilwa Kaskazini, Rufiji na kule Kilwa Kusini zina hali mbaya sana. Namshukuru Mheshimiwa Waziri, tuliona matunda yalipatikana kwenye mawasiliano yetu. Baadhi ya barabara zetu zilipata wakandarasi, lakini wakandarasi wale wameshindwa kuanza kazi. Wengi wamekuwa na manung'uniko ya kuonesha kwamba hawajalipwa pesa za kazi ambazo walifanya siku za nyuma. Kwa hiyo, imewafanya washindwe kuendelea kufanya kazi hizi ambazo wamepewa sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya kutoka Njinjo kwenda Kandawale mpaka Ngarambe, tayari mkandarasi ameshapatikana, lakini hajaenda kazini kwa sababu anaidai Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara kutoka Kandawale kwenda mpaka Nasaya na ile ya kutoka Kipatimu kwenda Miangalaya mpaka Mtende na Jimbo jirani maarufu la Rufiji, haijaanza kushughulikiwa japokuwa mkandarasi ameshapatikana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, kuna barabara ya kutoka pale Mingumbi kwenda mpaka Chapita, imeshatengenezwa kwa kiasi fulani, lakini kiasi kingine mkandarasi yuko kazini lakini hajaendelea na kazi kwa sababu anaidai Serikali. Kwa hiyo, naiomba Serikali iharakishe malipo ili hawa wakandarasi waweze kuendelea na kazi na kurudisha barabara katika hali ya kawaida na hatimaye wananchi waweze kupata nafuu kutokana na mihangaiko wanayoipata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, pale kwenye Kijiji cha Mwengei, tumeletewa fedha zaidi ya shilingi milioni 83 kwa ajili ya kujenga matundu ya vyoo na madarasa, lakini barabara haipitiki. Kwa hiyo, gari zinashindwa kuingia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukienda Kibata na Mwenge pia kuna miradi ya maji imekwama kwa sababu gari za kuchimba visima zimeshindwa kufika huko kwa sababu barabara ni mbaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, ninapenda kusema, Mheshimiwa Waziri baada ya kuwa umetuhakikishia kwamba pesa zitakuja na baadhi ya wakandarasi wameshapatikana na wamekuwa *employed,* bado kuna baadhi ya maeneo kwa mfano ile Barabara ya Kipatimu – Miangalaya bado haijapata mkandarasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi juzi tulishauriana na wataalamu wa *TARURA* waweze kuomba maombi maalum ili ku-*rescue situation* iliyopo ili hiyo miradi mingine ambayo imekwama iweze kuendelea mbele. Wameomba shilingi milioni 200. Mheshimiwa Waziri, nakuomba katika zile fedha za *emergency* ambazo tulitenga mwaka jana zaidi ya shilingi bilioni 400, utumegee hiyo shilingi milioni 200 ili tukakamilishe ile barabara katika kipindi hiki kifupi kijacho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hiyo barabara pia ina umuhimu mkubwa kwa Watu wa Wilaya ya Rufiji, kwa sababu ikitoka Kipatimu inapita mpaka Mwenge inakwenda Miangalaya inakwenda mpaka kule Nambunju, Mbwala mpaka inatokea kule. Kwa hiyo, naomba hayo tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la mwisho kabisa, Wilaya yetu ya Kilwa ni miongoni mwa Wilaya kubwa sana katika eneo lake, lakini ina jiografia mbaya sana. Wilaya yetu ya Kilwa ni kubwa kuliko Mkoa mzima wa Dar es Salaam na Wilaya yetu ya Kilwa inafanana na Mkoa mzima wa Kilimanjaro. Kwa hiyo, nakuomba niwasilishe ombi maalum la wananchi wa Wilaya ya Kilwa kwa sababu wanateseka sana katika shughuli za kiutawala. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri atufikirie kuigawa Wilaya ya Kilwa kuwa katika halmashauri mbili. Halmashauri moja iwe ndani ya mipaka ya Kilwa Kaskazini na

halmashauri nyingine iwe ndani ya mipaka ya Kilwa Kusini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nina imani mgawanyiko huu ukifanikiwa, basi tutapiga hatua kubwa za maendeleo kama ilivyo dhamira ya dhati aliyonayo Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nashukuru kwa kunipa nafasi. Ahsante sana na ninaunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya Mheshimiwa Rais kumwaga *flyover* Dar es Salaam, kila jimbo, na kila mkoa wanataka *flyover*. Nawahakikishia zinakuja kwenu. *(Makofi/Kicheko)*

Tunaendelea na Mheshimiwa Rweikiza, Mheshimiwa Minza, na Mheshimiwa Zaytun wajiandae.

**MHE. DKT. JASSON S. RWEIKIZA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia kwenye Bajeti hii ya TAMISEMI. Kipekee namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupa afya hadi muda huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee pia namshukuru na kumpongeza sana Mheshimiwa Jemedari wetu, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi nzuri sana anayoifanya ya kuiendeleza nchi yetu na kutupa maendeleo makubwa pamoja na wasaidizi wake, Mheshimiwa Makamu wa Rais, Mheshimiwa Waziri Mkuu, Waheshimiwa Mawaziri na viongozi wengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Mchengerwa, Waziri wa TAMISEMI, Naibu Mawaziri, Mheshimiwa Dkt. Festo Dugange na Mheshimiwa Zainab Katimba kwa kazi kubwa wanayoifanya katika Wizara hii ya TAMISEMI. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, TAMISEMI ndiyo uhai wa nchi yetu kwa sababu inasimamia mambo mengi sana ambayo yote yanakwenda vizuri. Ndiyo maana nawapongeza hawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye Jimbo langu la Bukoba Vijijini tumepata miradi mingi sana ambayo imefanyika ya TAMISEMI na mingine isiyo ya TAMISEMI. Kwa mfano, barabara nyingi zimejengwa na nyingine zimefanyiwa ukarabati ambao umefanya ziweze kutumika.

Mheshimiwa Naibu Spika, jimbo hili na maeneo ya Mkoa wa Kagera tuna mvua nyingi sana. Kwa hiyo, barabara zinaharibika mara kwa mara, na muda mwingi zinakuwa na mashimo, hazipitiki vizuri, lakini *TARURA* ambayo iko chini ya TAMISEMI, wako makini muda wote kuzifanyia ukarabati ili zirudie hali yake ya kupitika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, Maeneo ya Rugaze mwaka 2023 ilijifunga kabisa, wakaikarabati vizuri na madaraja na kalavati, leo ni barabara nzuri. Pia maeneo ya pale Kata ya Rukoma, ilijifunga hivyo hivyo kwa matope, lakini wameikarabati na leo inafanya kazi vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la Katokoro, Kata ya Katoro kwenda Kata ya Kyamulaile, pale kuna barabara ya miaka mingi lakini kilometa tano hivi au nne palijaa maji kama mita mbili kwenda juu ikawa haipitiki. Hata hivyo, TAMISEMI kwa kuwatumia *TARURA* wakaikarabati. Nilikwenda kwa *Engineer* Seff ambaye kila mtu anamsema hapa akatusaidia kuikarabati mara moja, na leo inapitika vizuri japo ni kwa taabu kidogo kwa sababu ya mvua lakini inapitika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo mengine, Barabara ya Kyabaramba kwenda Izimbya, ilijaa maji ikajifunga kwa muda mrefu, wakajenga madaraja pale na sasa inapitika. Barabara ya Kutoka Ibwera kwenda Butakya ilikuwa imeharibika sana, lakini wameikarabati sasa hivi nayo inapitika vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kwa kweli tuna kila sababu ya kumshukuru Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa anayoifanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha Mheshimiwa Dkt. Samia, jimboni kwangu tumepata zahanati 19 mpya ambazo zimefunguliwa na zinafanya kazi. Vituo vya afya vipya vinne vimefunguliwa na vinafanya kazi. Hospitali moja ya Wilaya pale Bujunangoma imefunguliwa na inafanya kazi; na siyo kufunguliwa tu, hata watumishi, madaktari na wauguzi wengine wameletwa. Vilevile, vifaatiba vimeletwa, vipo, na vinafanya kazi. Pia, dawa zinapatikana bila shida yoyote. Kwa kweli huduma imekuwa bora sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, upande wa elimu, tumepata shule 10 mpya. Tuna Shule ya msingi moja pale Kanazi B na shule tisa za sekondari ambazo zinafanya kazi. Ni nzuri na ambazo zimejengwa kisasa mpaka maktaba zipo, maabara tatu, madarasa ya TEHAMA na vifaa vingine ambavyo ni vya kisasa kabisa vipo kwenye shule hizi. Pia, kuna shule za msingi nyingine kama nne zilizokuwa chakavu sana zimekarabatiwa, zimekuwa mpya na zinafanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tumejenga madarasa mapya 117. Tumejenga matundu ya vyoo 342 na hii ilikuwa ni kero kubwa. Miaka ya nyuma kuna shule moja ilifungwa kwa sababu ya kutokuwa na vyoo, lakini leo hiyo ni historia, tumejenga vyoo 342. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tumejenga shule zaidi ya sita za Kidato cha Tano na sita ambazo zipo pale na zinaendelea. Kuna mengine ambayo ni ya nje ya TAMISEMI lakini Serikali ni moja. Kwa mfano, ndani ya jimbo langu kuna miradi ya maji 46 ya maji safi na salama na ya kutosha ambayo inahudumia vijiji 57. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, umeme umefungwa katika vijiji vyote japo siyo wa TAMISEMI, ni wa nje ya TAMISEMI, lakini Mheshimiwa Rais Samia amesimamia jambo hili na limekwenda vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tumepata *ambulance* mbili mwaka huu ambazo tumezipeleka katika vituo vya afya hapo Katoro na sehemu nyingine na zinafanya kazi vizuri uhitaji unapotokea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeweza kujengewa ofisi mpya ya Makao Makuu ya Halmashauri. Zamani tulikuwa bado tupo Bukoba Mjini ambao ni Manispaa, lakini leo tumehamia kwetu. Jengo limekamilika, ni zuri na kubwa ambalo lina kumbi za Madiwani kufanya vikao vyao, kuna ofisi za Watendaji na watu kupata huduma. Haya ni mambo mazuri. Miradi yote hiyo niliyoisema imegharimu shilingi bilioni 403. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, kuna miradi mingine ambayo inaendelea na inafanyiwa kazi na mingine imekamilika nje ya hizo fedha. Kwa mfano, Chuo cha *VETA;* Kagera hatukuwa na Chuo cha *VETA* cha hadhi ya mkoa, lakini leo kipo. Kwa kweli kina hadhi ya Kimataifa. Ni kizuri sana, alikifungua Mheshimiwa Rais Samia mwezi Oktoba, 2022. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, leo tunajengewa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Tawi la Bukoba. Ujenzi unaendelea kwa shilingi bilioni 22. Vilevile, Bandari ya Kemondo imekamilika kwa 100% na itasaidia sana kuboresha huduma ya usafiri kwa wananchi kwa bei rahisi, usalama wa kusafirisha mazao kama kahawa, ndizi na kadhalika kwenda katika maeneo mengine. Kwa hiyo, kwa kweli tuna kila sababu ya kumshukuru Mheshimiwa Rais Samia kwa kazi nzuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na shukurani hizo, kuna msemo kwamba, kushukuru ni kuomba tena. Pale kwenye Tarafa ya Bugabo, Kata ya Rubafu, kuna kivuko cha kwenda Uganda kilianza kujengwa kama miaka kumi na zaidi huko nyuma. Ni jirani sana kutoka pale kwenda Uganda. Walijenga pale jengo la uhamiaji, jengo la *customs* na sehemu ya *ferry* na meli kuweka nanga pale baadaye wakaacha na leo ni miaka zaidi ya 10.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kile kivuko kijengwe ili tupate *ferry* nzuri pale ya kuvusha watu kwenda Uganda kwa

sababu ni jirani sana kutoka pale, badala ya barabara ambayo inazunguka kupita Bukoba huku kwenda Uganda ambayo ni ndefu sana. Pale itasaidia kuongeza huduma kwa wananchi kwa sababu Uganda na sisi ni ndugu; tuweze kuungana moja kwa moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, kuna suala la utalii wa kimatibabu *(medical tourism)*. Pale Rubafu jirani na Kata ya Kishanje, kuna kituo cha afya kizuri sana. Kama nilivyosema, kina waganga, vifaatiba na mambo mengine. Kwa hiyo, kile kivuko kijengwe ili huduma ziweze kutolewa pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la mwisho...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Malizia.

**MHE. DKT. JASSON S. RWEIKIZA:** Mheshimiwa Naibu Spika, namalizia. Barabara ya Katokoro niliyoisema kwamba ilijengwa, leo tena imeharibika sana kwa sababu ya mvua nyingi nilizozisema. Naomba ifanyiwe ukarabati tena, *TARURA* itusaidie ile barabara ijengwe ili ifanye kazi vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Tunaendelea na Mheshimiwa Minza, Mheshimiwa Swai na Mheshimiwa Zedi wajiandae. *(Makofi)*

**MHE. MINZA S. MJIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuweza kuchangia katika Wizara hii. Namshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kunipa kibali leo kuweza kusimama katika Bunge lako hili Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, napenda kumshukuru sana Mheshimiwa Rais wetu Mama Samia, Mama yetu, anafanya kazi kubwa sana. Sote tunaona na sote ni mashahidi kwamba hakuna sehemu ambayo hajafanya kazi. Mama amegusa kote, abarikiwe sana. Naendelea kumwombea

kwa Mwenyezi Mungu amsaidie apate afya njema na aendelee kufanya kazi vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru sana na kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mchengerwa. Mheshimiwa Waziri wetu, ahsante kwa kazi nzuri unazofanya. Tunakuona unavyoshughulika katika halmashauri mbalimbali, unatupatia pesa na unaleta maendeleo katika nchi yetu. Ahsante kwa kumsaidia mama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitakuwa mchoyo wa fadhila nisipowashukuru Naibu Mawazi hawa wawili. Nawashukuru sana Mheshimiwa Dkt. Dugange pamoja na Mheshimiwa Katimba. Ni Mawaziri ambao wanafanya kazi kwa uadilifu na ni watu ambao ni wasikivu pia. Nashukuru sana kwamba, hata tunapowaona hawa Naibu Mawaziri, wanatusikiliza na wanatekeleza kile ambacho tunawaomba. Nashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda niingie katika Mkoa wangu wa Simiyu. Mkoa wa Simiyu kwa kweli ni mkoa ambao umeleta maendeleo sana, lakini yamepitia kwa Mama yetu Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan. Mama Samia ameukumbuka Mkoa wetu wa Simiyu. Mkoa wa Simiyu kwa sasa una maendeleo makubwa. Tunafanya kazi nyingi na barabara ni nyingi za kutosha, nashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, niingie katika upande wa maji. Katika Mkoa wetu wa Simiyu, tunashukuru kwa kupata mradi mkubwa wa wilaya zote tano. Hongera sana Mama Samia kwa kutupatia mradi huu mkubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niingie katika wilaya zangu za Mkoa wa Simiyu. Katika Mkoa wa Simiyu tuna wilaya tano lakini Wilaya ya Meatu inaongoza kwa ukame wa maji. Ninalisema hili jambo kila siku. Meatu tuna shida ya maji sana. Mheshimiwa Waziri tunaomba muiangalie sana Wilaya ya Meatu. Maji yetu tunayokunywa siyo safi na wala siyo salama, lakini tunaishi tu kwa kudra za Mwenyezi Mungu. Tunaomba maji ya huo mradi ambao

unaletwa katika Mkoa wa Simiyu, basi tupate maji hayo haraka ili watu wa Wilaya ya Meatu tuishi vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuingia katika upande wa barabara. Mkoa wa Simiyu tumepata pesa nyingi sana katika majimbo yetu yote na barabara zetu zilikuwa ni nzuri na tumefanya kazi vizuri. Tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais wetu. Changamoto ni moja, mvua hizi ambazo zimenyesha na pamekuwa na mashimo mengi, makorongo na madaraja mengi yamekatika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tunaomba sana *TARURA* mtuangalie sana. Kwa kweli barabara ni shida na watu wengi wanashindwa kufanya hata biashara zao vizuri kwa sababu barabara nyingi zimekatika na madaraja mengi yamekatika. Kwa hiyo, ule mtandao siyo mzuri. Tunaomba TAMISEMI itusaidie. Pia, tunashukuru imepeleka fedha, sasa wanaendelea. Ahsanteni kwa hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naingia upande wa elimu. Tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais wetu, ametujengea shule ya watoto wa kike. Watoto wana shule nzuri katika Mkoa wa Simiyu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda niongelee jambo lingine kwamba, tumepata madarasa mengi sana na tunamshukuru mama yetu, lakini kuna shule ambazo ni kongwe. Kuna Shule ya Nhobola A, Nhobola B, Mwagindu na kuna Inalo. Shule hizi zimekuwa ni za muda mrefu na ni chakavu kabisa. Tunaomba basi zitengewe fedha na zijengwe kwa ajili ya kuimarisha elimu katika Mkoa wetu wa Simiyu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwamba tumepata vituo vya afya vingi na zahanati nyingi katika Sekta ya Afya. Tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais wetu kwa kutuletea fedha nyingi katika Mkoa wa Simiyu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, kuna maboma ya vituo vya afya 13 katika Mkoa wa Simiyu ambayo hayajakamilika. Vilevile,

kuna zahanati 32 ambazo hazijakamilika. Hivi vituo vya afya pamoja na zahanati zimejengwa kwa nguvu za wananchi. Tunaiomba Serikali itie mkono ili maboma haya yaweze kukamilika na nguvu za wananchi ziweze kuonekana kwamba zimefanya kazi pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru pia kwamba katika kupata vituo vya afya, hospitali na zahanati, vifo vya mama na mtoto vimepungua kabisa, na havitapungua tu, lakini baadaye itakwenda kuwa historia kwamba vitakwisha na hakitaonekana hata kifo kimoja kulingana na kwamba vituo vya afya vimekuwa vingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, napenda kusema kwamba, katika watumishi wa afya katika Mkoa wa Simiyu, hapa asubuhi nimeuliza swali la nyongeza, Mkoa wa Simiyu ni miongoni mwa Mikoa 10 ambayo ina upungufu wa watumishi wa afya. tunaiomba Serikali iangalie sana huu Mkoa wa Simiyu. Unaweza ukakuta kituo cha afya kimoja, kuna wafanyakazi wawili au mmoja kitu ambacho haiwezekani kabisa katika utendaji, tunaiomba Serikali ituletee watumishi wengi katika vituo vyetu vya afya ili wagonjwa waweze kupata huduma zinazostahili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, upande wa watumishi katika elimu, kama nilivyosema kwamba tunashukuru tumejengewa shule nyingi, lakini tuna upungufu mkubwa wa walimu. Unakuta darasa moja lina watoto 180 ama watoto 150, lakini mwalimu anayefundisha ni mmoja, walimu watatu, walimu wanne, kwa kweli hiyo haipendezi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Shule za Sekondari zimejengwa nyingi kama nilivyosema, lakini tatizo kubwa ni walimu. Hakuna walimu, walimu hawatoshi, watoto hawafundishwi masomo mengi kwa sababu walimu hawatoshi. Mheshimiwa Waziri Mchengerwa tunakuomba uangalie sana tupate hao walimu ambao wanaweza wakafanya kazi vizuri sana katika Mkoa wetu wa Simiyu.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nimshukuru sana Waziri kwa ajili ya kazi nzuri ambazo zimeendelea kufanyika katika Mkoa wa Simiyu. Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Swai, atafuatiwa na Mheshimiwa Zedi.

**MHE. ZAYTUN S. SWAI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa hii nafasi nami niweze kuchangia bajeti ya Wizara ya TAMISEMI.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, nampongeza sana na kumshukuru sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kutuletea maendeleo Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo, nawapongeza sana Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI na Manaibu wake wote kwa kuwa wasikivu muda wote na kutekeleza haya maono mazuri ya Mheshimiwa Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwanza kwa kuishukuru sana Serikali ya Chama cha Mapinduzi chini ya Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kutuletea maendeleo Watanzania. Katika Mkoa wangu wa Arusha, tumepokea takribani shilingi trilioni tatu ambazo zimepelekwa katika miradi mbalimbali ya maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia kwenye sekta ya afya, tumepokea zaidi ya shilingi bilioni 50 ambazo zimeenda kwenye uboreshaji wa miundombinu ya afya, shilingi bilioni 10 zimeenda kwenye vifaatiba, zaidi ya shilingi bilioni 35 zimeenda kwenye ujenzi wa zahanati mpya 49 kwenye Halmashauri zote za Mkoa wa Arusha.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile tumepata zaidi ya vituo 26 vya afya kwenye Halmashauri zote na tumepata fedha kwa ajili ya ujenzi wa hospitali saba za Wilaya. Sambamba na hilo,

tumepokea fedha kwa ajili ya ukarabati na ununuzi wa vifaatiba katika hospitali yetu ya Rufaa ya Mount Meru. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hapo awali wananchi wengi wa Mkoa wa Arusha na maeneo jirani walikuwa wanalazimika kwenda mpaka nchi jirani kwa ajili ya kupata huduma ya afya lakini leo hii hospitali yetu ya Rufaa ya *Mount Meru* kwa kweli ina vifaa vyote na wananchi kwa kweli wanaridhika na huduma wanazozipata pale. Uboreshaji huo wa sekta ya afya umeleta mafanikio mengi na tumejionea kwa macho.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeona ongezeko la upatikanaji wa dawa na vilevile tumeona ongezeko la akina mama wanaokwenda kujifungua katika vituo vya afya. Hilo limeleta maendeleo makubwa na tumeona vifo vya mama na mtoto vimeweza kupungua kwa kiasi kikubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeona vifo vya mama na mtoto vimepungua kutoka vifo 556 hadi vifo 104 kwa kila vizazi hai 100,000. Kipekee kabisa nampongeza Mheshimiwa Rais kwa kuendelea kujali maisha ya Watanzania. Sisi wananchi wa Mkoa wa Arusha tunasema hatutamwacha na tunasema tunasonga na mama hadi mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hii sekta ya elimu, Mkoa wangu wa Arusha umepokea zaidi ya shilingi bilioni 210 ambazo zote zimepelekwa kuongeza idadi ya shule za msingi, madarasa, miundombinu ya mabweni, vyoo pamoja na mambo mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hilo, ikiwemo ujenzi wa shule ya wasichana ya Longido Samia *Girls* ambayo inafundisha wanafunzi wetu wasichana masomo ya sayansi, hii itasababisha kuongezeka kwa idadi ya wanafunzi wasichana wanaosoma masomo haya ya sayansi. Nampongeza sana Mheshimiwa Rais na ninaendelea kumshukuru sana Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kujali masuala ya elimu hususan elimu ya mtoto wa kike. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hotuba yake, Mheshimiwa Waziri hapa amesema kwamba, maendeleo ya kweli hayawezi kupatikana kama hatutaweza kuwekeza katika masuala ya afya, elimu na ustawi wa jamii. Kwenye hotuba yake hapa amedhihirisha dhahiri kwamba hotuba hii ya mwaka 2025/2026 ya Wizara hii ya TAMISEMI inaenda kuakisi malengo mazuri na malengo haya ya kimaendeleo ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niongelee suala la mikopo ya 10% ya Halmashauri. Naishukuru sana Serikali ya Chama cha Mapinduzi, katika Mkoa wangu wa Arusha katika mwaka huu wa fedha tumeweza kutenga zaidi ya shilingi bilioni 11 ambazo zimeenda kutolewa katika makundi mbalimbali ya akina mama, vijana na watu wenye ulemavu. Katika hili suala kuna changamoto moja kubwa. Bado suala la elimu ya utoaji wa mikopo halijaweza kuwafikia wananchi wengi hususan wananchi wa vijijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, binafsi nimefanya ziara katika Kata zote za Mkoa wa Arusha na nikienda maeneo ya vijijini, wengi bado wanalalamika hawana ufahamu juu ya utolewaji wa hii mikopo ya Halmashauri. Kwa hiyo, naomba kama kweli Wizara ina dhamira njema ya wananchi waweze kunufaika na hii mikopo, basi waweze kuwahamasisha Maafisa Maendeleo ya Jamii wetu waweze kwenda ngazi za chini kabisa waweze kutoa elimu ya hii mikopo ili basi wananchi wetu wote waweze kunufaika na haya masuala ya mikopo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu mwingine, bado Wilaya ya Ngorongoro wanampenda sana Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan na wanamshukuru sana kwa maendeleo yote anayowaletea. Kuna suala moja katika Tarafa ya Ngorongoro, bado huduma za kijamii hazipelekwi kule kwenye shule zetu, hususan Shule ya Ngorongoro *Girls* na shule nyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna miundombinu ya majitaka ambayo ni vyoo, pia kuna uchakavu sana wa majengo. Naomba Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI alichukulie hili suala kwa

umuhimu wake na aielekeze Serikali basi iweze kupeleka miundombinu kwenye shule zile za wananchi waliobaki kwenye Tarafa ya Ngorongoro. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kusema hayo machache, naomba niendelee kumshukuru sana Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kutuletea maendeleo Watanzania, wananchi wa Arusha tunasema tunasonga mbele na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni waliopo Bungeni asubuhi hii.

Wapo Wageni watano wa Mheshimiwa Mohamed Omary Mchengerwa, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, jamaa zake kutoka Jijini Dar es Salaam, karibuni. *(Makofi)*

Wageni 61 wa Mheshimiwa Minza Simon Mjika waumini wenzake wa Kanisa la Mshikamano *SDA* na Kanisa la Tumaini *SDA* kutoka Meatu, Mkoani Shinyanga, karibuni. *(Makofi)*

Wageni 21 wa Mheshimiwa Dkt. Medard Matogolo Kalemani, ambao ni Waimbaji wa Kwaya wa Chato kutoka Mkoani Geita, karibuni. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Anatropia Lwehikila, Ndugu Julian Samwel Mdigi, ambaye ni rafiki yake na mfanyabiashara kutoka Johannesburg, Afrika Kusini. *(Makofi)*

Wageni 38 wa Mheshimiwa Mwita Mwikwabe Waitara, ambao ni Wajasiriamali Wasabato kutoka Tarime, Mkoani Mara. *(Makofi)*

Pia tunao wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo. Wanafunzi 80 na walimu wanne wanachama wa Chama cha Skauti kutoka Shule ya Msingi Milestone, Jijini Dar es Salaam, karibuni. *(Makofi)*

Wanafunzi 56 na walimu watatu kutoka Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Mkwawa, Mkoa wa Iringa. *(Makofi)*

Wanafunzi 80 wa Chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo cha Jijini Dodoma. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Mheshimiwa Zedi, jiandae Mheshimiwa Janeth Massaburi.

**MHE. SELEMANI J. ZEDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii ili nami niweze kuchangia hii hotuba ya bajeti ya TAMISEMI iliyo mbele yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, kwa dhati kabisa ya moyo wangu niungane na Waheshimiwa Wabunge waliotangulia kumshukuru kwa dhati Mheshimiwa Rais wetu wa Awamu ya Sita Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa upendeleo mkubwa sana ambao ametupatia Jimbo la Bukene. Nasema upendeleo kwa sababu kwa miaka yote ambayo nimekuwa Mbunge, sijawahi kupata fedha nyingi za maendeleo kama ambavyo nimepata kipindi hiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia napongeze umakini na uchapakazi wa Waziri na Naibu Mawaziri wa hii Wizara ya TAMISEMI. Kwa kweli ni Mawaziri na Manaibu Waziri ambao ni wasikivu, wako makini na unapopeleka hoja zako kwao wanakusikiliza, wanafuatilia na wanakupa *feedback*. Kwa hiyo, nikupongeze sana Mheshimiwa Mchengerwa, lakini pia Naibu Mawaziri Waziri wako ambao pia wako makini; Dkt. Festo Dugange na Mheshimiwa Zainab Katimba, kwa kweli mnatupatia ushirikiano mzuri sana Waheshimiwa Wabunge na tunawashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijasahau, nichukue fursa hii kusema, pamoja na kwamba tunapata fedha nyingi sana za miradi ya maendeleo, lakini matokeo chanya ya hizi fedha yanatokana na usimamizi mzuri sana wa Serikali ya Mkoa na Serikali ya Wilaya ya Nzega.

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue fursa hii kabisa na kwa niaba ya Wabunge wenzangu wa Mkoa wa Tabora, kumpongeza Mkuu wetu wa Mkoa wa Tabora Ndugu Chacha Matiko kwa usimamizi mkubwa na mzuri sana wa hizi fedha ambazo zinashuka chini. Pia nampongeza Mkuu wetu wa Wilaya Ndugu Naitapwaki Tukai. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kipekee nimpongeze Mkurugenzi wa Halmashauri ya Nzega *DC*, *Engineer* Apolinary ambaye kwa kipindi kifupi alichokuwepo ameonyesha na ameleta mabadiliko makubwa. Wakati huyu Mkurugenzi wa Nzega *DC*, *Engineer* Apolinary anaanza ukurugenzi Nzega, mapato yetu ya ndani kwa mwaka yalikuwa ni shilingi 1,800,000,000, lakini kwa kipindi cha miaka miwili aliyokuwepo ameweza kusaidiana na Waheshimiwa Madiwani nasi kupandisha mapato ya ndani kutoka shilingi 1,800,000,000 na sasa hivi tunafunga mwaka tukiwa na mapato ya ndani ya shilingi 3,700,000,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ni ongezeko la karibia 100%. Kwa hiyo, kwa dhati kabisa mimi na mwenzangu Mheshimiwa Dkt. Hamisi Kigwangalla tunapongeza sana uchapakazi mzuri wa Mkurugenzi wetu wa Nzega *DC*, *Engineer* Apolinary. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tumepata mafanikio mengi, nitajaribu kuyasema machache, lakini pia nitasema changamoto ambazo bado tunaomba Serikali yetu iweze kutuunga mkono tuweze kupata mafanikio.

Mheshimiwa Naibu Spika, upande wa sekta ya afya, Jimbo la Bukene kwa kipindi hiki tumeboresha sana. Tumeweza kufungua zahanati mpya tano ambazo hazikuwepo kabisa. Tumeweza kufungua zahanati ya Kijiji cha Bulyambi, tumejenga, tumekamilisha na imeanza kutoa huduma kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia zahanati ya Kijiji cha Mogwa tumejenga, tumekamilisha na imeanza kutoa huduma. Zahanati ya Kijiji cha Buhulyu, tumejenga tumekamilisha na wananchi

wanaanza kupata dawa pale. Zahanati ya Ilagaja na zahanati ya Iboja hizi zote hazikuwepo lakini majengo yamekamilika na huduma zimeanza kutolewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo ambalo naomba TAMISEMI watusaidie ni kwamba hizi zahanati zote zina *Clinical Officer* mmoja mmoja tu. Kwa hiyo, unakuta huyo huyo ndio anamsikiliza mgonjwa, huyo huyo ndiye anaenda kumchoma sindano, huyo huyo ndiye anatoa dawa. Yuko mmoja tu pekee yake hakuna manesi. Kuna uhaba mkubwa sana wa watumishi, hivyo tunakamilisha zahanati, tunazifungua, lakini watumishi wanakuwa wachache sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba sana hizi zahanati mpya za Gulyambi, Mogwa, Buhulyu, Ilagaja na Ihoja, zipate angalau manesi wawili wawili kuweza kuwasaidia hawa *Clinical Officers* ambao wako pale ambao wanafanya shughuli zote pekee yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ni kuhusu kituo cha afya cha Itobo. Jimbo langu lina vituo vya afya viwili, kituo cha afya cha Bukene na kituo cha afya cha Itobo, kila Tarafa kituo cha afya kimoja. Sasa kituo cha afya cha Itobo tumeweza kukiboresha sana. Tulipatiwa shilingi milioni 800 ambazo tumejenga jengo la mama na mtoto jipya; tumejenga maabara, tumejenga chumba cha *X-Ray*, tumenunua *X- Ray machine* mpya ya shilingi milioni 180, lakini tumepatiwa na gari la wagonjwa. Kwa hiyo, tuliahidi kuboresha afya na tumeboresha afya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa alikuja Jimboni kwangu na akazindua hiki kituo cha afya kwa maana ya kutembelea haya majengo mapya ambayo tumeyaboresha.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kituo cha Afya cha Bukeni ni cha zamani sana, tangu wakati wa mkoloni, lakini nashukuru sana kwenye orodha ya vituo vipya vya afya vya kila Jimbo katika

Jimbo langu, tutapata hizo fedha kwa ajili ya kituo kipya cha afya katika Tarafa ya Bukene ambayo inahudumia Kata tisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ni matumaini yangu kwamba hizi fedha zitatoka muda siyo mrefu ili ujenzi wa kituo kipya cha afya cha kisasa katika Kata ya Bukene ambacho kitahudumia Tarafa tisa kiweze kuanza kufanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine kubwa ambalo mabadiliko makubwa sana yametokea, ni eneo la elimu. Pale kwenye Jimbo langu la Bukene ndiyo kuna shule ya kwanza ya Kidato cha Tano na Sita cha Serikali ndani ya Wilaya nzima ya Nzega inaitwa Kili Sekondari. Kwa kipindi kirefu shule hii ilikuwa inadahili wasichana wa Kidato cha Tano na Sita 150 tu kwa mwaka. Mheshimiwa Rais wetu wa Awamu ya Sita kwa nia na dhamira ya dhati ya kuongeza elimu kwa wasichana, watoto wetu wa kike ametupatia shilingi milioni 800 ambapo tumejenga madarasa 10 na mabweni manne, Sasa hivi badala ya kupokea wasichana 150 kwa mwaka, tunapokea wasichana 475 kwa mwaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue fursa hii kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Bukene kumshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa nia ya dhati ya kusaidia wasichana wetu waweze kupata elimu.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Zedi, malizia.

**MHE. SELEMANI J. ZEDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa nafasi hii, kazi kubwa imefanyika, na nina uhakika uchaguzi ujao Mheshimiwa Rais kwa Jimbo la Bukene anakwenda kupata kura nyingi sana za kishindo na Chama cha Mapinduzi kinakwenda kushinda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Janeth Massaburi, Mheshimiwa Magessa, halafu Mheshimiwa Zeeland jiandae.

**MHE. TUMAINI B. MAGESSA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa nafasi nzuri uliyonipatia ya kundelea kuchangia leo tena kwenye Wizara hii ya TAMISEMI, hotuba hii nzuri iliyotolewa na Mheshimiwa Mchengerwa, Waziri wa Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa ambayo tunaiona kwenye hotuba hii au kwenye hii bajeti kwa kuruhusu fedha nyingi katika bajeti iliyopita na kama rasilimali, zikaenda kufanyiwa utekelezaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Mawaziri wawili, wataalam wa Wizara hii kwa uratibu mzuri wa rasilimali ambazo zimeruhusiwa na kuyaona yale ambayo tunayaona kwenye hotuba hii ambayo inaonesha kwamba kumekuwa na matokeo chanya katika kila ambacho kimeenda kutekelezwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukipitia tu ukurasa wa tisa wa Hotuba ya Bajeti hii, utagundua kwamba, mwaka 2020/2021 Wizara hii ilipata takribani shilingi trilioni 7.01, lakini bajeti iliyopita tulikuwa tayari tumekwenda kwenye shilingi trilioni 10.03 na leo maombi yaliyopo ni shilingi trilioni 11 kama na saba hivi, kwa hiyo, inaonesha kuna ongezeko.

Mheshimiwa Naibu Spika, yapo mahitaji yanaongezeka, lakini vilevile ubunifu wa hao ambao ndio wataalamu, inatuonyesha Mheshimiwa Waziri sasa anahitaji fedha nyingi zaidi kuhakikisha kwamba Watanzania wanapata maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Rais na Mheshimiwa Waziri kwa kazi kubwa katika sekta ya elimu. Nilikuwa napitia ukurasa wa 12, inaonekana wazi ukiangalia vyumba vya madarasa tu vina ongezeko la takribani 32.69%, shule za msingi ukiangalia utaona zina ongezeko la 9.63%, shule za sekondari zina ongezeko la 26.68% na nyumba za walimu zimeongezeka kwa takribani 3.5%; maktaba, maabara na

mabweni vyote vinaonekana vimeongezeka. Kwa hiyo, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri kwamba, kuna kazi kubwa imefanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hayo, hata ukarabati, zipo shule nyingi sasa zimekarabatiwa. Zipo sekondari takribani 74 na shule za msingi 794 zimepitiwa kufanyiwa ukarabati. Ni wazi kwamba, zipo shule nyingi sana zilikuwa zimechakaa. Kwa hiyo, utaratibu huu unaofanywa na Wizara, unafanya shule zile ambazo zinaonekana, hali yake siyo nzuri sana, zinaendelea kukarabatiwa mwaka hadi mwaka, kurudia katika hali yake ili tuendelee kutoa elimu iliyo bora.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jimboni Busanda ukiangalia shule za msingi ambazo zimeongezeka, zipo takribani 18 na shule za sekondari takribani 20 kwa miaka hii minne ambayo Mheshimiwa Rais amekuwepo madarakani. Natoa pongezi kubwa kwa sababu kuna mambo makubwa nimeyaona yakitokea katika maeneo yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile fedha za *TARURA* ambazo zilikuwa takribani shilingi trilioni moja sasa zinakwenda kuwa shilingi trilioni karibu 4.5. Naamini kabisa kuna kazi kubwa inakwenda kufanyika kwenye maeneo tuliyonayo. Mvua kubwa zinaendelea kunyesha Kanda ya Ziwa na hivyo, barabara nyingi ziliharibiwa na mvua ya kuanzia mwaka jana na mvua ya mwaka huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni ombi langu kwamba, fedha zile ambazo tulizitenga mwaka 2024 na hizi ambazo zitatengwa mwaka huu, 2025, basi ziende kuhakikisha miundombinu ile inatengenezwa, kuhakikisha kwamba, barabara zinarudishwa kwenye hali yake ili wananchi waweze kupata huduma iliyo bora zaidi. Naamini haya yakifanyika, tutakuwa kwenye nafasi nzuri sana ya wananchi wetu kufanya shughuli kutoka sehemu moja kwenda nyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la afya. Tunaona kabisa wazi kuna vituo vingi vimejengwa. Ukiangalia, kama nchi, kuna ongezeko kubwa la vituo vya afya, lakini kama Jimbo kwa maana

ya Busanda, zipo fedha ziliahidiwa pale Rwamgasa kwamba, zitakwenda kwa ajili ya kuhakikisha kituo cha afya kinajengwa na kukamilika. Nafikiri kwamba, zimekwenda, lakini bado inahitaji kuziongeza ili tuweze kujenga pale kituo cha kimkakati ambacho tuliandika, nafikiri mwaka 2024. Naamini kwamba, fedha zake zitakuwa zinakwenda na kama zitakwenda kwa wakati, basi tutahakikisha wananchi wetu wanaweza kuhudumiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kiuhalisia, sisi tuna hospitali ambayo ina hadhi ya Wilaya, lakini bahati mbaya ni kwamba, barabara za kwenda kwenye hospitali hii ambazo zinatakiwa zijengwe na *TARURA,* nyingi hazipitiki. Kwa hiyo, wagonjwa tulionao wanaotakiwa kwenda pale wanakwenda kwa matatizo kwa sababu, hospitali ipo, lakini barabara zile za kwenda kufika eneo lile hazipitiki. Ni ombi langu tu kwamba, barabara hizi zifanyiwe kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Rais na niwe wazi tu kwamba, uratibu katika mkoa wetu chini ya Mheshimiwa Shigela, unafanyika vizuri na vilevile katika wilaya yetu chini ya Mheshimiwa Komba vilevile unafanyika vizuri. Uratibu unaofanyika na Mkurugenzi wetu, Karia, unafanyika vizuri, ndiyo sababu unaona miradi mingi inafanyiwa utekelezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi langu ni kwamba, wawezeshwe ili kuhakikisha haya tunayoyasema yanaweza kufanyiwa kazi. Kwa mfano, changamoto ambayo tunaisema kwenye afya, nikiangalia tu kwenye kumbukumbu zangu, kuna Kituo cha Chankorongo, Kitigili, Nyakafuro, Butobera, Iririka, Nderema, Rwamwizo na Mwenegeza. Haya ni maboma ambayo yapo, yanahitaji kumaliziwa. Yapo na mengine mengi, haya ambayo nimeyataja ni machache. Kama tukipata fedha za kutosha, haya maboma ya afya yataweza kufanyiwa kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, shule chakavu ambazo nilizitaja mwanzo, kwa mfano, tuna Shule ya Kabugozo, Shule ya Lulama na Shule ya Rubanda, hali yake siyo nzuri sana. Zipo shule zimefanyiwa kazi kwa maana ya nchi, lakini zipo shule chakavu Jimboni Busanda, ni vizuri sana zikaguswa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hilo, naomba tu wataalamu wetu na viongozi wetu, kwa maana ya Mkuu wa Wilaya, nimekuwa nafuatilia, nimetembelea mara moja, mara mbili, ile nyumba anayokaa, sasa ni ombi langu, TAMISEMI iweke bajeti ya kutosha kuhakikisha kwamba kuna ujenzi wa nyumba mpya unafanyika pale.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi ni wachimba dhahabu, unaweza ukajua Mkuu wa Wilaya anatakiwa kuwa na nyumba gani, kwa wachimba dhahabu? Sasa Serikali ihakikishe inampa hadhi hiyo, kwamba, nyumba anayoishi iwe na hadhi hiyo, hata wanapokwenda kumtembelea wajue kabisa huyu ni Mkuu wa Wilaya ya Wachimba dhahabu. Naamini kabisa haya yakifanyika kila mtu atakuwa *comfortable* kwenye maeneo yetu na kazi itafanyika vizuri zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja. Ahsante sana kwa kunisikiliza.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Jonas, jiandae Mheshimiwa Mwijage.

**MHE. JONAS V. ZEELAND:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi. Nianze nami kwa kumshukuru na kumpongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa na nzuri ambazo anazifanya katika nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri, Waheshimiwa Naibu Mawaziri na timu nzima ya TAMISEMI kwa kazi kubwa na nzuri sana ambazo wanazifanya. Huko nje baadhi ya wananchi wachache wanasema kwamba, Waheshimiwa Wabunge kazi yao kubwa ni kusifiasifia tu, tunasifia kwa sababu, kuna vitu ambavyo vimefanyika ndiyo maana inasababisha sisi Waheshimiwa Wabunge kusifia.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nimefundishwa kwamba, unapoomba jambo, ukipewa, ukishukuru, unaweka nafasi ya kuomba tena. Yapo mambo mengi ambayo tuliyaomba sisi watu wa Mvomero, Mheshimiwa Rais amesikia kilio chetu, ametupa

fedha nyingi za miradi. Ndiyo maana leo, tuna kila sababu na kila Mheshimiwa Mbunge ameguswa kwa namna moja ama nyingine kwenye jimbo lake, tunashukuru.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme machache kabla sijaleta maombi kwa Mheshimiwa Waziri, ili watu waelewe kwa nini tunashukuru. Yapo machache ambayo nitayasema kati ya mengi, ambayo yamefanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye eneo la elimu tulikuwa na upungufu mkubwa sana wa vyumba vya madarasa kwenye shule zetu za msingi, lakini kwa kipindi cha Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, mpaka sasa hivi ametupa fedha ya kujenga vyumba vya elimu ya msingi 128, haijawahi kutokea. Katupa fedha, tumejenga shule mbili mpya za msingi ambapo, hakuna mwananchi aliyechangishwa hata shilingi 100.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye eneo la elimu ya sekondari kila mwisho wa mwaka ama mwanzoni mwa mwaka, watendaji wetu walikuwa wanakimbizana na wananchi kuwachangisha fedha kwa ajili ya kujenga vyumba vya sekondari. Katika kipindi cha Mheshimiwa Rais hakuna mwananchi yeyote katika Jimbo la Mvomero, ambaye alichangishwa na watendaji wetu kwa ajili ya ujenzi wa vyumba vya sekondari. Ametupatia vyumba vya sekondari 174 ambavyo sasa hivi watoto wetu wanasoma kwenye vyumba vizuri, vyumba vya mfano.

Mheshimiwa Naibu Spika, tulikuwa na upungufu wa sekondari sita za kata, leo ninapozungumza hapa, katika kipindi cha Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, tumeshajenga. Katupatia fedha tumejenga sekondari tano za Kata ya Homboza; tumejenga sekondari Lubungo, tumejenga sekondari Msogozi, tumejenga sekondari Mkindo, tumejenga sekondari Kweuma, bado Kata moja tu ya Kikeo na nina imani katika bajeti ijayo tutakwenda kumalizia kata iliyobakia. Tumeshapata fedha, kwa ajili ya kujenga Sekondari ya Amali, fedha zimeshaingia zaidi ya shilingi milioni 500, muda wowote kazi itaanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumepandisha hadhi sekondari zetu tano kuwa sekondari za *advance*. Tarafa nzima ya Mgeta yenye kata saba haikuwa na sekondari ya *advance*, sekondari inajengwa. Tumepandisha hadhi sekondari yetu pale Mgeta, pale Doma tunajenga sekondari ya *advance* katika Kata ya Doma na pia, Mvomero tunajenga sekondari ya *advance*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sungaji na Kweuma hivi vitu tulikuwa tunavililia miaka nenda miaka rudi. Katika kipindi cha Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, haya mambo tumeyaona.

Mheshimiwa Naibu Spika, niende kwenye eneo la afya. Kwa kifupi tu yapo mengi yamefanyika, lakini nasema machache. Tumemaliza zahanati zilizoanzishwa na nguvu za wananchi. Zipo zahanati ambazo zilijengwa na wananchi kwa miaka mingi na wananchi walishakata tamaa ya kujitolea kuanzisha ujenzi wa kitu chochote kwa sababu, kuna majengo ambayo waliyaanzisha, yalikaa muda mrefu hayakumaliziwa. Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, ametupa shilingi milioni 650 tumekwenda kumalizia zahanati 13 ambazo zilianzishwa na nguvu ya wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumejenga vituo viwili, kuna *ambulance* mbili tumezipokea na vifaatiba, ambapo haijawahi kutokea kupokea vifaatiba kwa pamoja vyenye thamani ya zaidi ya shilingi bilioni moja na milioni mia moja. Tumevipokea na vimegawiwa huko kwenye vituo vyetu vya afya na kwenye zahanati zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, yapo mengi, lakini kwa sababu ya muda niombe, sasa nina jambo moja tu, naomba Mheshimiwa Waziri na timu yako mnisaidie kutokana na mvua kubwa zilizonyesha mwaka jana, na ambazo zinaendelea kunyesha sasa hivi zimesababisha barabara zetu nyingi kufa na jiografia yetu ya Mvomero siyo rafiki sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye *ceiling* ya bajeti wamewekewa ukomo wa shilingi bilioni mbili na milioni mia nne, ni

fedha ndogo ukilinganisha na jiografia yetu. Tuna barabara zenye urefu wa kilomita 1,300, hii shilingi bilioni 2.4, ni hela ndogo sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi jimbo letu zaidi ya 80% ni wakulima. Tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, katika hii miaka yake mitano tulipata, nje ya bajeti, zaidi ya shilingi bilioni 3.8, tulikwenda kufungua barabara ambazo zilikuwa zinaunganisha kata kwa kata, lakini pia, barabara ambazo zilikuwa zinaunganisha wilaya kwa Wilaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni Barabara ya Maskati kutoka Kibaoni kwenda Maskati. Hii barabara tuliifungua, Barabara ya Ndole – Kinda, Barabara ya Muhonda – Kweuma, Barabara ya Mkindo – Mndela, Barabara ya Jandila – Chenzema, Barabara ya Tembomchafu – Gonja, Tembomchafu kwenda Pandambili na Pandambili – Dibuluma na Dakawa kwenda Kibaoni kupitia Milaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hizi fedha tulizozipata katika miaka iliyopita, nje ya bajeti, tulitengeneza hizi barabara, lakini kwa mvua zilizonyesha mwaka 2024 na zinazoendelea kunyesha sasa, hizi barabara zimeharibika. Vile vile tuna barabara ambazo zinapitika kwa shida sana. Naomba niziseme hapa, na nina imani katika bajeti hii mtakwenda kuzipa kipaumbele hizi barabara. Mfano Barabara ya Difinga kwenda Dihinda, Barabara ya Mzia kwenda Njeula, Barabara ya Turiani – Digomadigalama, Barabara ya Wami – Dakawa, Barabara ya Milama – Kibaoni, Barabara ya Homboza Masalawe – Luwale.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii ni njia mpya, tunataka tuifungue Barabara ya Kibaoni – Bunduki, Barabara ya Langali – Bumu – Mwalazi – Msungi, Barabara ya Kibaoni – Kuyu, Barabara ya Nyandila – Muhale – Lukunguni, Barabara ya Mzumbe – Tangeni Mnyanza, Barabara ya Mkukuyuni – Vitonga, Barabara ya Melela – Magali Yowe, Barabara ya Vivuwe – Mlaguzi, Barabara ya Dunduma – Kisala na Barabara ya Melela – Mela.

Mheshimiwa Naibu Spika, hizi barabara ndiko wanakokaa wakulima wetu. Kama hizi barabara zitatengenezwa, tutakwenda

kuwasaidia wakulima wetu na tutakwenda kuinua uchumi wa watu wa Mvomero. Mimi namwamini sana *Engineer* Seff, ametusaidia sana Wilaya ya Mvomero, na hizi barabara nina imani katika bajeti ijayo zitakwenda kutengenezwa kwa kiwango ambacho kitakwenda kuwasaidia wananchi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalize tu la mwisho. Sisi Watu wa Mvomero, kila mtu kwa imani yake, tunamwombea sana Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, Mwenyezi Mungu ampe maisha marefu aendelee kututumikia Watanzania. Pili, nataka niseme hapa, tunakwenda kumpa zawadi ya kumpa kura nyingi katika uchaguzi wa mwezi Oktoba, haijawahi kutokea.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nakushukuru sana, naunga mkono hoja. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Mwijage, na baada yake atachangia Mheshimiwa Mafue, Mheshimiwa Gulamali na Mheshimiwa Waitara, wajiandae.

**MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipatia fursa ya kuchangia Bajeti ya TAMISEMI. Napenda kunukuu shughuli zote za maendeleo na ustawi wa wananchi zilizo nyingi, kama siyo zote, ambazo zinafanyika TAMISEMI. Kwa hiyo, nichukue fursa hii kuzungumza bajeti ya wananchi wa Tanzania wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati nachangia Bajeti ya Ofisi wa Waziri Mkuu, nilikuja na dhana ya *springboard*. Kupitia dhana hiyo, nilipitia kazi zote tulizofanya kwenye miaka mitano, na hususan miaka minne ya Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan. Sasa nakuja na dhana mpya ya kushukuru.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikiazima maneno ya Mtumishi wa Mungu, Mwalimu wangu Dkt. Father Kamugisha, anasema anayeshukuru anakumbuka. Ukimwona mtu anashukuru, anakumbuka. Yaani ukizungumza kwa Kiingereza, inaeleweka vizuri, yaani asiyeshukuru hana *memory,* lakini anayeshukuru anakumbuka. Asiyeshukuru hana *memory.*

Mheshimiwa Naibu Spika, anayeshukuru anathamini. Yaani anayeshukuru kile ulichompa, anakithamini, yaani asiyeshukuru ina maana hathamini. Ni kama kiumbe, kama kuku, unampa pilau, halafu anakula, halafu anaparuaparua, huyo hathamini. Anayeshukuru anaomba tena.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimetumwa na wananchi wa Rutoro kuja kushukuru, nimetuwa na wananchi wa Muleba kuja kushukuru, nimetumwa na wananchi wa Ibuga kuja kushukuru, nimetumwa na Jimbo la Muleba Kaskazini, nimetuwa na Wilaya ya Muleba, nimetumwa na Mkoa wa Kagera kuja kushukuru.

Mheshimiwa Naibu Spika, hizi habari mnazosema, narudia tena kwa mara ya tatu, sisi tumeshamaliza. Tarakimu yetu ni 1,560,000. Hata ukimpigia simu Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa kwamba kura za Kagera ni ngapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, katika 1,560,000 kura za Mama, yeye anaongeza *plus.* Hiyo ndiyo kushukuru.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa niende kwenye kuchangia bajeti hii. Naanza kuchangia kwenye sekta za kiuzalishaji. Kama nilivyoungumza mwanzo, TAMISEMI ndiyo kila kitu katika maendeleo na ustawi; lakini maendeleo na ustawi ni lazima uendane na uzalishaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawapongeza TAMISEMI, wameanzisha huu mchakato wa kwenda kuwasaidia wananchi, kuwawezesha wananchi, na nimeona hata kwenye vipaumbele vya Wizara, mwaka huu unaokuja 2025/2026 tunakwenda kuwawezesha wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nikupe ushauri. Ili uwawezeshe wananchi wa Tanzania, kama dhamira ya Mheshimiwa Rais ilivyo, kutoka hatua hii kwenda hatua nzuri kubwa, lazima tuhakikishe kwamba, tunatenga rasilimali za kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mchengerwa shilingi bilioni 123 ulizotenga tutatofautiana, lakini napenda nitoe ushauri mwingine, hawa ustawi wa jamii, lazima tuwape watu wa kuwasaidia, lazima utengeneze timu ya kuweza kuwasaidia hawa watu kwenda ku-*coach*, kwenda kushawishi, na ikibidi kwenda kuminya, yaani wasikudanganye Mheshimiwa Mchengerwa, watu wengine kuja kuwatoa kwenye hatua hii waliyopo kwenda hatua nzuri, ni lazima uwaminye.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata mtoto unapomwekea chakula hawezi kula, inabidi umminye kusudi aweze kula. Naomba katika upande wa ile 4:4:2 pamoja na vyanzo mlivyozungumza, kwanza vyanzo vya ndani, sijui marejesho, havitoshi. Fikiria katika shilingi bilioni 200 za mwaka huu, 2025 tunaomaliza, shilingi 123 za mwaka kesho, 2026, tukichukua shilingi trilioni moja tukawaweka watu hawa hapa; nenda katika ma-*shelf* yako Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakumbuka niliandika jarida linalohusu ujenzi wa uchumi wa viwanda katika Serikali za Mitaa, Waziri akalisome jarida hilo. Nakumbuka mtangulizi wake, Mheshimiwa Jafo, aliwahi kuamuru viwanda 100 vitengenezwe. Wakati mimi ninahubiri vyerehani vinne, yeye akasema vitengenezwe viwanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, namkumbuka Mheshimiwa Magessa, ilibidi niwapandishe ndege hawa nikawapeleka China. Badala ya kuwafundisha viwanda. Wachina, Mungu atawaona, wakawafundisha Kichina hao watu. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja yangu ni kwamba, wapeni watu zana. Wilaya ya Muleba, namshukuru Mkurugenzi, Muleba sasa hivi wanakwenda kuwapa watu vitu *tangible,* yaani unampa shughuli, anaanza na shughuli.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo tulilonalo, wengi waliopewa mikopo hii, wanakwenda kwenye uchuuzi. Uchuuzi hauwezi kubadilisha maisha ya mtu. Soma taarifa za Dangote, kwamba *it is manufacturing* inaweza kumbadilisha mtu, lakini uchuuzi ni wa

kwako. Leo unachuuza, kama hali yako siyo nzuri mkeo au mwanao hawezi kukusaidia, lakini *production;* kama una ng'ombe wa maziwa, usipokamua wewe, mwanao atakamua.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri, na Mheshimiwa Waziri Mchengerwa amwulize Mkurugenzi wa Muleba, nimezungumza naye sana, tumeelewana, tunakwenda kwenye *production*. Amwulize kwamba, wanafanyaje *production*? Ampe mara mbili ya kile ambacho amepanga kwa sababu rasilimali zake siyo kubwa za kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumze kuhusu wakandarasi. Wakandarasi. Ili wakandarasi waendelee, wanahitaji mkono wa Serikali. Jana mchangiaji mmoja hapa, Profesa alizungumza akasema *cashflow* ndilo tatizo. Wakandarasi hawalipwi. *The role of the government,* uje na nguvu. Pamoja na zile *bonds* alizoanzisha Mheshimiwa Rais, tuwape fedha ili wasiogope kufanya ukandarasi, tuwalee. Kwa ile fedha wanayoipata hata tatizo letu la kazi na ajira tutakuwa tumelimaliza. Unafundisha watu sayansi wawe ma-*engineer,* sasa kama ukandarasi haulipi, atakwendaje kufanya u-*engineer?* Utamkuta anapiga debe.

Mheshimiwa Naibu Spika, hilo ataliweza, lakini nimu-*inject* pale ili tuwasidie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine gumu ni kuhusu wafanyakazi. Nimepitia makabrasha mengi ya halmashauri na nimewasikiliza watu wengi; ana wafanyakazi wangapi kwenye elimu, afya, na ujenzi? Je, anahitaji wangapi? Je, wale wanaopungua Tanzania wapo? Je anashindwa nini kuwaajiri wote?

Mheshimiwa Naibu Spika, zipo sababu za msingi za kuzuia kuwaajiri. Sasa tukae hapa kama Bunge, Watanzania wote waseme na tuweze kuajiri kulingana na mahitaji na vile vikwazo tuweze kuviondoa. Nashauri hilo tulijadili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, twende kwenye bajeti yake. Katika bajeti naomba amwulize Mkurugenzi wake wa afya, ampe

*imprest* aende kwenye jimbo langu ambako kuna zahanati zangu; Zahanati za Kitua, Ruanga, Burembo, Buhaya, Nyakahama, Ngenge, Kabhare, Makongora, Kinagi na Iroba. Amtume Mkurugenzi wake aende aniambie ni kwa nini zile zahanati hazijaanza? Nimweleze Ndugu yangu Mheshimiwa Mchengerwa, ukiweza kunisaidia kupiga hatua moja, maisha yangu yatakuwa yanaendelea kusonga mbele. Nisaidie, uende utusaidie kwenye suala hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie kuhusu suala la vituo vya afya. Namshukuru sana, na nimeongea na naibu wake. Kituo cha mkakati cha Ngenge kinasubiriwa. Kimsingi sitaki kuzungumza zaidi kwa sababu tulizungumza kwa kina mpaka yeye akawa haamini…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa, malizia.

**MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE:** … amepanga zahanati mpya za kuongezea, hizo zahanati nilizomweleza azikamilishe.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo machache ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, Mheshimiwa Mafuwe, jiandaeni Mheshimiwa Gulamali, na Mheshimiwa Waitara.

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, wanafunzi wa Yesu, wengine wanamwita Nabii Issa, walimwambia Mwalimu, tufundishe kuomba. Akawaambia mnaposali semeni hivi, "Baba yetu uliye Mbinguni, jina lako litukuzwe, ufalme wako uje, mapenzi yako yatimizwe, utupe leo"; maana yake nini? Unatambua, unasifia kisha ndipo unapeleka hoja yako, kwamba utupe leo mkate, utupe leo riziki. Vivyo hivyo nami kama walivyofundishwa wanafunzi wa Yesu, nitakwenda kwa *style* hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza sana na kumshukuru Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa sana anayoifanya katika Jimbo la Hai. Hili juzi nilisema siyo maneno yangu, nimetumwa na watu wa Hai na ninatenda haki kwa kumshukuru Mheshimiwa Rais na nina hakika mwezi Oktoba tunakwenda kumlipa kura za kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri, tumefanya naye kazi kwa ukaribu sana. Mimi ni Mjumbe wa Kamati ya TAMISEMI, kwa kweli wanaomwita mtu kazi, kwa kweli ni mtu kazi. Mimi ninampongeza kwa kazi anayoifanya. Kule Hai tunampongeza kwa sababu hakuishia na kazi za Serikali tu, hata za kijamii. Amekuja kwenye harambee kwenye Usharika wa Hongo, juzi amekuja pale kwenye Msikiti wa Kilashini, ameshirikiana nasi, yeye na Naibu Waziri. Tunawapongeza na kuwashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nawapongeza Naibu Mawaziri bingwa sana, ndugu yangu Mheshimiwa Dkt. Festo na dada yangu Mheshimiwa Zainab Katimba, wanafanya kazi kubwa na nzuri sana. Nampongeza Katibu Mkuu Ndunguru, anafanya kazi nzuri sana na Naibu Makatibu Wakuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia unikubalie niwapongeze Waheshimiwa Wakuu wa Mikoa. Tumetembea takribani mikoa yote ya nchi hii na tumeona kazi kubwa wanayoifanya, wakiongozwa na Mkuu wa Mkoa bingwa kabisa, Mheshimiwa Nurdin Babu, Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, anatusimamia, anafanya ziara. Kwa kweli niseme, Mheshimiwa Rais ametupatia Mkuu wa Mkoa mzuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nawapongeza Makatibu Tawala wakitanguliwa na Katibu Tawala wa Mkoa wa Kilimanjaro kwa namna ambavyo wanaratibu kazi zao. Pia Wakuu wa Wilaya wakitanguliwa na ndugu yangu Hassan Bomboko Mkuu wa Wilaya ya Hai, anafanya kazi nzuri. Nikiwa huku nina amani kwa sababu yeye kule anaendelea na ziara, anamsemea Mheshimiwa Rais, na anamsemea Mheshimiwa Mbunge pia, Makatibu Tawala

wakiongozwa na Sospeter, Katibu Tawala wa Hai pamoja na Wakurugenzi wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa kwa Wakurugenzi niseme kidogo. Kwenye Kamati yetu tumekuwa wakali sana, na tumekuwa wakali kwa Wakurugenzi ili watekeleze majukumu yao. Leo kila anayesimama anashangilia humu, anasema vituo vya afya vimejengwa, zahanati zimejengwa, shule zimejengwa, ni kwa sababu hawa Wakurugenzi wapo.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo nawapongeza, na ninawapongeza Wakurugenzi wote Tanzania kwa binafsi, siyo kwa sababu ya taasisi zao, wao wenyewe. Tukumbuke Wakurugenzi nao ni watu, na kwa kweli wanapokea maagizo kila mahali, huku kuna Mkuu wa Mkoa, huku kuna Mkuu wa Wilaya, huku kuna Mkurugenzi, yaani kila mahali wanapigwa kama mpira wa kona; lakini mwisho wa siku wameweza kutoa matokeo ambayo tunayazungumza.

Mheshimiwa Naibu Spika, na mnajua, Wakurugenzi wengi Tanzania ukifuatilia utakuta kama hana kisukari, basi ana *pressure*. Ni kwa nini amepata magonjwa haya? Ni kwa sababu ya kuhangaika na matatizo ya wananchi. Kwa hiyo, nawapongeza Wakurugenzi wote Tanzania wakitanguliwa na Mhinga, Mkurugenzi wa Wilaya ya Hai kwa kazi kubwa wanayoifanya; pamoja na Watendaji wote wa Serikali, ngazi za Mitaa, Kata na Watendaji wote wa Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, nampongeza sana Mtendaji Mkuu wa *TARURA,* tumefanya naye kazi, kwa kweli *Engineer* Seff ni mtu muungwana na rahimu sana. Ameambukiza tabia yake hii kwa Watendaji wake mpaka ngazi ya mwisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, kule kwangu Hai tuna *Engineer* Kuya anafanya kazi mchana na usiku, wanafanya kazi kubwa sana. Hiyo ni sambamba na kupongeza hii *Samia Bond.* Huu ubunifu ambao Mheshimiwa Rais amekujanao ni kitu kizuri sana. Nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa kusimamia vizuri. *Samia Bond* itaondoa changamto na matatizo ya wakandarasi nchini,

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile nawapongeza Watanzania kundi kubwa limejitokeza kuwekeza. Malengo yalikuwa ni shilingi bilioni 150, lakini ime-*shift* hadi shilingi bilioni mia tatu na ushei; hayo ni mafanikio makubwa sana. Kubwa, kuna kundi kubwa sana la wakandarasi wanawake ambao wamejitokeza na wamechukua hisa kule, na wanafanya kazi. Niseme kwamba wakandarasi wachangamkie fedha hizi kwenye *Samia Bond* ili kuondoa matatizo yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa sasa tuna fedha kwenye *Samia Bond*, na jana Mheshimiwa Waziri wa Fedha ameniambia kwamba fedha zimepelekwa, nami nimekiri, kwamba jana fedha zimeingia kwa ajili ya ujenzi wa barabara kipande cha kuanzia Narumu kwenda Madaraja Mawili, mkandarasi ameshalipwa, nawapongeza sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba, na Mheshimiwa Waziri anisikilize vizuri. Tuna barabara ya Makoa kwenda Mferejini. kilometa 18. Kipande cha kuanzia pale Narumu ndicho hiki ambacho nimesema amelipwa jana, lakini kuna kipande cha kuanzia Makoa kwenda kwa Mengi, kwenye lile bonde kuna changamoto. Mheshimiwa Naibu Waziri alitembelea pale na aliliona eneo hili. Namwomba Mheshimiwa Waziri ahangaike na mkandarasi huyu ili hiki kipande kiweze kujengwa. Hii barabara ni muhimu sana, na ni barabara yetu ya kimkakati kwenye uchumi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunayo barabara nyingine, hii barabara ya Bomang'ombe, Chekimaji - *TPC*, siyo barabara ya Shaashisha na wala siyo barabara ya Hai, hii ni barabara ya Mkoa wa Kilimanjaro. Kwenye *RCC* waliipitisha kama barabara ya Mkoa kwa sababu hii ndiyo inayotoka Bomang'ombe inakwenda kutokea Moshi Mjini. Kwenye Daraja la Kikafu kukitokea shida, hakuna njia nyingine, kwa hiyo, hii pia ni barabara ya kiusalama, na Mkuu wa Mkoa yupo pale juu anajua hii kwamba ni barabara ya mkoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, wametupatia kilometa 3.5 kati ya kilometa 25. Nimwombe Mheshimiwa Waziri, hili yeye analiweza. Barabara ninayozungumza, ya Bomang'ombe – Chekimaji – *TPC* yenye urefu wa kilometa 25 wametupatia kilometa 3.5 tu, hizi ni chache mno ilhali hii ni barabara ya mkoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, zipo barabara nyingine nitazitaja kwa haraka haraka. Hizi Mheshimiwa Waziri aziweke kwenye begi lake na atembee nazo, ni barabara zetu za kimkakati. Barabara ya Sadala – Jiweni, hapa nimeshaahidiwa, ni barabara yenye kilometa 36. Ile barabara ifike Jiweni, ijengwe kwa kiwango cha lami na taa juu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nyingine ni Barabara za Sadala – Longoi, Lundugai – Tindigani; Mferejini kwa Tito, Mkalama Kikafuchini solu – Sawe, Kikafuchini – Miembeni, Somari – Tindigani, Kawaya – Kikuletwa, na Chilinjoro – Mijengweni ni barabara zetu ambazo zikijengwa na zikapitika tutaweza kushiriki kuchangia kwenye pato la Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana, tuna vivuko vingi. Najua kwamba kule Matiku mkandarasi tayari yuko *site,* Mkwarungo mkandarasi yuko *site,* Bonza mkandarasi yupo *site*, na Sawe mkandarasi yuko *site*. Naomba atusaidie Marire, Kikafu, Weruweru, kule Makoo pamoja na KKKT Geza viweze kujengwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ambalo naomba ni kuhusu shule chakavu. Nimempelekea andiko, shule 77, na ninashukuru ameanza kutupatia fedha, lakini bado aongeze *speed*. Hivi karibuni hapa Shule ya Mkwasaringe choo kimezama. Kwa hiyo, sasa hivi tupo tunahangaika kuhamisha wanafunzi kwenda shule nyingine. Kwa karne hii siyo sawa, na Halmashauri ya Hai hata ukisema watumie fedha za mapato ya ndani hawawezi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri yetu imehangaika, shule zetu nyingi zimejengwa miaka ya nyuma, kwa hiyo, unakuta uharibifu na uchakavu ni mkubwa sana. Kwa hiyo, naomba

watupatie fedha ya dharura ili zikasaidie kuokoa choo cha Mkwasaringe na vyoo vingine katika shule ambazo zimeharibika.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, tumeleta maombi maalum kwa ajali ya ujenzi wa shule za sekondari, Shule ya Sufi na Gezaulole, naomba fedha hizi zije kwa haraka.

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie kwenye eneo la posho za Wenyeviti wa Vijiji…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa, malizia.

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** …. niombe, wameweka kwenye bajeti lakini wakikishe Wenyeviti wanapewa posho zao za madaraka.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja na ninakushukuru sana, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Gulamali, jiandae Mheshimiwa Waitara na Mheshimiwa Kanyasu.

**MHE. SEIF K. S. GULAMALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipata nafasi ya kuweza kuchangia kwenye Wizara hii ya Mheshimiwa Mchengerwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napenda kutumia nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa aliyoifanya ndani ya muda mfupi, hongera sana kwake.

Mheshimiwa Naibu Spika, tangu alivyoingia Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, sisi katika hii Wizara ya Mheshimiwa Mchengerwa ndiyo Wizara ambayo inagusa wananchi kwa zaidi ya 90%, kwa sababu ndiyo Wizara ambayo inahudumia masuala ya afya, elimu, inahudumia mikopo, barabara za vijijini na wakulima.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kwa kipindi chake Mheshimiwa Rais, fedha alizozileta tunaweza tukasema hazina kipimo, kwa kuwa imeleta mabadiliko makubwa ndani ya majimbo yetu. Hii inathibitika, kwa kuwa Waheshimiwa Wabunge wote hapa ndani kila anayesimama anapongeza. Nami nasema hongera sana Mheshimiwa Rais, kazi hii ni kubwa, na nina hakika unahitaji kupewa miaka mingine mitano kwa kura nyingi sana; na tunaamini utazipata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka niseme tu, pale alipo Mheshimiwa Mchengerwa, alipopewa ile nafasi ame-*fit* na anafaa; yaani ameitendea haki. Kwa bahati nzuri Mheshimiwa Mchengerwa amekuwa anafanya kazi; kila Wizara alizokuwepo wanaofanya kazi naye hawatamani aondoke kwenye Wizara hizo, na akiondolewa watumishi na walio chini ya hiyo Wizara, wanasikitika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mchengerwa amekuwa Wizara ya Maliasili na Utalii, watu walilalamika; alikuwa Wizara ya Masuala ya Michezo, watu walilalamika alipohamishwa; na leo yupo katika Wizara hii ya TAMISEMI. Ama hakika tunaona mabadiliko makubwa. Mheshimiwa Mchengerwa chapa kazi, tunakuombea kwa Mungu, tunaamini *future* ipo kwako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kingine, nimpongeze pamoja na Naibu Mawaziri wake, Mheshimiwa Katimba pamoja na Mheshimiwa Dkt. Festo, ni Naibu Mawaziri ambao wamemsaidia vizuri sana Mheshimiwa Waziri. Wachape kazi, ama hakika wao ni mawaziri ambao ni wasikivu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya pongezi hizo, nianze kwa kusema, kwanza napongeza upande wa *TARURA* kwa fedha nyingi ambazo wametupatia ndani ya muda mfupi. Niweze kusema, wakati wa miaka mitano nyuma tulikuwa tukipewa fedha za barabara ndani ya majimbo yetu. Katika Wilaya yetu ya Igunga tulikuwa tunapokea shilingi bilioni moja tunagawana Wabunge wawili. Tangu alipoingia Mama Samia, mwaka wa

kwanza alitupatia shilingi bilioni nne tukagawana Wabunge kila mmoja akachukua shilingi bilioni mbili.

Mheshimiwa Naibu Spika, pongezi nyingi sana kwa Mheshimiwa Rais pamoja na Wizara, wametupatia fedha ambazo zimefanya mabadiliko. Ndani ya jimbo langu nimeweza kutengeneza mpaka barabara za mitaa katika Miji ya Simbo, Nkinga, Ziba, Ibologelo, pamoja na Choma; na tunaendelea kutengeneza barabara za mitaa kwa kadri ambavyo watakuwa wanatupatia fedha kwenye maeneo mengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeweza kufungua barabara ambazo zilikuwa hazijawahi kufunguliwa tangu dunia imeumbwa. Tumeweza kutengeneza barabara katika maeneo mbalimbali ya jimbo letu na kuziboresha. Tumetengeneza barabara ya Ibologelo kwenda Choma kupitia Mchinje, barabara ya kutoka Nyandekwa kwenda Ntigu mpaka Ulaya, barabara ya kutoka Nkinga kwenda Ikungwipina, barabara ya kutoka Simbo kwenda Usoya mpaka Bwekela, ni fedha nyingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile tumejenga madaraja makubwa kule Muwinamu katika Kijiji cha Bwekela, tumejenga madaraja ya Manonga kule Mondo na Choma. Pia tunajenga daraja lingine katika Mto Manonga pale Mwashiku. Tunawapongeza sana, kazi kubwa imefanyika katika upande wa barabara kwa fedha hizi ambazo wametupatia.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, naomba, katika zile asilimia za barabara ambazo walikuwa wametupatia, zimepungua 40%. Naomba watupatie hizi 40% ili tuweze kujenga barabara ya kutoka Mwisi kwenda Busomeke mpaka Mizazi, ndizo fedha ambazo zimebaki. Pia nimeomba watupatie fedha nyingine za kujenga barabara kutoka Chagutwa Majengo kwenda Igumo mpaka Chapela kutokea Mpogoro. Ni kati ya maeneo machache kabisa ambayo hayajatengenezewa barabara kwa muda mrefu. Tunaomba watupatie fedha hizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba, kuna wakandarasi walikuwa wanafanya kazi katika barabara hizi nilizozitaja. Kuna Mkandarasi anaitwa Wembere, kuna Mkandarasi anaitwa Mashiri, kuna Mkandarasi anaitwa Gradiator, na kuna Mkandarasi anaitwa Mnazareti. Hawa ni wakandarasi ambao wamefanya kazi na wengine wameishia njiani, bado hawajamaliza. Naomba wapewe fedha ili waweze kukamilisha barabara hizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kutoka upande wa *TARURA*, nizungumzie sasa upande wa vituo vya afya. Nawapongeza sana Serikali, wametupatia Kituo cha Afya cha Ziba. Sasa tunaomba fedha ili tumalizie kile Kituo cha Afya cha Ziba. Tumeona wametupatia magari ya kubebea wagonjwa katika Kituo cha Afya cha Choma.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia wametupatia gari kwa ajili ya Hospitali ya Rufaa ya Nkinga, na wametupatia gari kwenye Kituo cha Afya cha Simbo. Naomba tunamalizie kutoa gari la wagonjwa kwenye Kituo cha Afya cha Ziba. Mheshimiwa Waziri achukue hilo, tunaomba gari Kituo cha Afya cha Ziba ambacho wametupatia fedha, tunakwenda kukamilisha muda siyo mrefu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba zile fedha ambazo walituambia ni kwa ajili ya vituo vya afya vipya, kwa mfano, Kituo cha Afya cha Uswaya nilichokiandika, fedha hizo ambazo naomba, hata shilingi milioni 250, ili tuanze ujenzi wa kituo hicho cha afya. N,jua kwamba kuna fedha nyingine zinakwenda kwenye hospitali yetu ya Kituo cha Afya cha Choma; huku tuna upungufu wa shilingi milioni kama mia tano, ambazo wametuwekea kwenye zile fedha za Benki ya Dunia nazo tunaomba tuzipate.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo naweza kulichangia ni kuhusu elimu. Najua muda wetu siyo rafiki, lakini kwanza tunawashukuru sana, wameleta mabadiliko makubwa sana kwenye sekta ya elimu nchi nzima, likiwemo Jimbo langu la Manonga, hongera sana, wamefanya kazi nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeweza kujenga shule nyingi za sekondari kwenye maeneo ambayo hakukuwa na shule za sekondari. Pale Itigu tumejenga Seif Gulamali, tumejenga Bulangamilwa, tumejenga kule wanapaita Tambarale. Sasa tumeanza ujenzi wa shule ya amali pale Choma ya takribani shilingi bilioni tatu, hongera sana, kazi kubwa wameifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tunaomba watupatie fedha za ujenzi wa mabweni kwenye Shule ya Sekondari ya Simbo, Shule ya Sekondari Nkinga, na Shule ya Sekondari ya Manonga ili tuweze kuzifungua na kuweza kuanzisha shule za Kidato cha Tano na Sita.

Mheshimiwa Naibu Spika, naamini Mheshimiwa Waziri atalipokea ombi hili kwa sababu yeye ni moja kati ya Mawaziri wanaofanya kazi na wanaosikiliza. Ninaamini wamepokea na tutapata fedha angalau katika hiki kipindi ambacho tunamalizia bajeti. Najua atanipa zile fedha zilizobakia, zinazoitwa bakaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda tu kusema kwamba, pamoja na kazi hii nzuri ambayo wameifanya ama hakika maendeleo yameonekana. Hata kwenye zahanati wametupatia fedha ambazo zimetuwezesha kujenga zahanati nyingi sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali hii ya Mama Samia imetupatia fedha, tumeweza kujenga Zahanati za Chapela, Mwamala, Nguriti, Itale, Ntigu, Matinje, Mondo, Imalilo na Zahanati ambayo tunakwenda kuijenga sasa hivi, ya Mwamloli. Naomba sasa Mheshimiwa Waziri atupatie fedha za ujenzi wa Zahanati za Bulangamilwa, Kalemela, Bungingija pamoja na Mwina ili kuhakikisha kwamba tunakamilisha hizi kero za wananchi ambao tunawahudumia sisi wawakilishi tunaokuja humu Bungeni kuwaombea fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja ya bajeti ya Mheshimiwa Waziri. Ametoka kwenye shilingi trilioni sita, na sasa amepeleka bajeti yake kwenye shilingi trilioni kumi. Mimi kama Mbunge ninayewakilisha wananchi wa Jimbo la Manonga,

naunga mkono hoja yake ya bajeti ya shilingi trilioni kumi. Ninaamini bajeti hii…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Haya, ahsante.

**MHE. SEIF K. S. GULAMALI:** …itakwenda kutatua kero za wananchi wa Jimbo la Manonga na watu wa Wilaya nzima ya Igunga, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Waitara, jiandae Mheshimiwa Kanyasu, na Mheshimiwa Kapinga.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa nafasi. Namshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa fedha nyingi ambazo ameleta katika Jimbo la Tarime Vijijini. Vilevile, nilikuwa na mambo mengi kule Mkoa wa Mara, lakini namshukuru Mheshimiwa Rais, ameleta Mkuu wa Mkoa jembe kweli kweli, Kanali Mtambi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi Mkoa wa Mara umetulia chini ya kiongozi huyo ambaye ametoa ushirikiano mkubwa na anafanya ziara katika maeneo mbalimbali na kutatua changamoto za wananchi wetu. Vilevile, namshukuru pia Mheshimiwa Rais kutuletea *DC* Meja Gowele ambaye anafanya kazi ya kusikiliza wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hawa viongozi wawili wanafanya kazi zaidi hata ya raia wa kawaida. Kumbe siyo wanajeshi wote wanafanya kazi kwa mabavu. Wakati mwingine kuna watu wazuri kama hawa ambao wamekuja Mara. Namwomba Mheshimiwa Rais waendelee kubaki pale kwa sababu kazi inaendelea kuchapwa mkoani mara. Vilevile, maagizo yake yamekuwa ni mwongozo mkubwa na utekelezaji wa mambo na changamoto za wananchi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI, Mheshimiwa Mchengerwa, watu wa Mkoa

wa Mara na Wilaya ya Tarime wanamshukuru sana. Alifanya ziara akiwa Waziri wa Maliasili, kauli aliyoitoa na bahati nzuri amekuja TAMISEMI. Watu wa Nyanungu, Gorong'a, na Kwihancha wametulia na Mkuu wa Mkoa hawasumbui, wanalima. Isipokuwa, ile migogoro inatakiwa ifanyiwe kazi iishe katika eneo lile. Kwa hiyo, wanamkumbuka sana, na kazi inaendelea kufanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru Waziri wa Maji, Mheshimiwa Aweso, kwenye eneo hili pia ametusaidia kupata ule mradi. Kwa maagizo ya Mheshimiwa Rais, maji ya Ziwa Victoria yanakwenda Sirari na Mkandarasi alikuwa amesimama na sasa yuko *site*, watu wameendelea kupata matumaini.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, nampongeza Mheshimiwa Waziri wa Madini, ameniahidi kwamba mwezi Mei atakwenda kugawa leseni kwa wachimbaji wadogo (vijana) ili wapunguze kuvamia mgodi na wafanye kazi ya uchimbaji. Pia, mgodi utapewa mtaji kwa vijana hao. Mheshimiwa Kiruswa naomba upeleke salamu kwa Mheshimiwa Waziri kwa kazi nzuri anayoifanya na kwa Serikali kwa ujumla kwa kutusaidia katika nyanja hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, wananchi wa Bumera wanalalamikia sana shida ya mbolea, jana nilikuwa kule. Naomba achukue hatua ya dharura ili watu wafanye kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna mambo ya jumla. Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI, Kanuni za *CSR* ni changamoto katika Wilaya ya Tarime na Kule Geita. Naomba uchukue hatua ya dharura. Miradi inatekelezwa na mgodi kwa njia ya mkandarasi, gharama ni kubwa. Tunataka miradi itekelezwe na halmshauri kama ilivyo Kahama pale Nyang'hwale ili fedha ziweze kutosha katika miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri achukue hatua aangalie uwezekano kwa Wenyeviti wa Vijiji, Madiwani, Mitaa na Vitongoji kupata posho. Tumeona Njombe wameanza; kwa *RC* Mtaka wameanza, nimeona Arusha inafanyika na Kanali Mtambi

ataanza hivi karibuni katika Wilaya ya Tarime, Halmashauri ya *Tarime DC*.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, ni vizuri ukaangalia hawa watu nchi nzima. Wasilazimishe wananchi kuchangia gharama za uendeshaji, mihuri na barua. Weka utaratibu wa kupata posho ili wapate mihuri na nauli za kwenda kwenye matukio ambayo wanakwenda kutatua changamoto za wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri, siyo jambo jema sana leo katika karne hii tuanze kuzungumzia matundu ya vyoo, watoto kukaa chini, madawati, viti na meza. Weka mpango mkakati wa muda mfupi, muda mrefu na mpango wa kati. Nchi nzima ifikie wakati tusizungumze humu Bungeni habari ya matundu ya vyoo, madawati, ila tuzungumze mambo makubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, shule zimejengwa mikoa yote 26. Tunataka shule za sekondari zote ziwe na maabara na vifaa vipatikane ili tufundishe watoto masomo ya sayansi vizuri zaidi na tuweze kupata wanasayansi katika nchi hii. Ni jambo la msingi sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nina maombi katika maeneo ya Tarime Vijijini. Tumepata Barabara ya Mugumu – Tarime – Serengeti, mkandarasi yuko *site*. Vilevile, kipande kutokea pale Kwinogo kwenda Serengeti kazi haifanyiki, tunaomba wapewe fedha. Barabara hii ni muhimu, itaongeza uchumi, ulinzi, watalii na itatuunganisha Tarime na Serengeti kwa kiwango cha lami. Vilevile, naomba nikupongeze Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, Mheshimiwa Rais kupitia kwako na kupitia Bunge hili, kitendo cha kuleta ubunifu wa *Samia Bond* na kukusanya fedha zaidi ya shilingi bilioni 300, wakandarasi wa ndani watakopa fedha. Pia, *CRDB* tunaipongeza sana na tutaendelea kuwaunga mkono kwa kazi nzuri ya kusimamia huu utekelezaji ili vijana wetu wapate fedha na wajenge barabara kupitia *TARURA*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mungu ampe Mheshimiwa *Engineer* Seff maisha marefu na afya. Amefanya kazi kubwa iliyotukuka. Vyeti ambavyo anapata siyo kwa bahati mbaya, ni kwa sababu ya utendaji. Mheshimiwa Waziri na wenzako wote Wizarani mnachapa kazi na mnaendelea kutupatia ushirikiano.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, nakushukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa niaba ya watu wa Nyamongo, eneo la Matongo, Nyarwana na kibasuka kwa kutupatia Daraja la shilingi milioni 400, smetuunganisha, lakini pongezi hizi ziende pale Kebweye na Magoma ambapo kuna daraja limejengwa, watu wanaungana na mawasiliano yapo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka niseme, sisi eatu wa Tarime Vijijini, popote utakapokwenda utamkuta Mama Samia na tunasonga naye mbele. Ukienda Tarafa ya Inano, hapa Komaswa utakwenda Manga Sekondari, pale Manga kuna mtaa na kituo cha afya, pale Bumera kuna kituo cha afya, kuna mradi wa maji na kuna barabara. Ukienda Kiore, kuna zahanati tatu, sekondari mbili, mradi wa maji, na barabara zimelimwa. Kazi na utu, Samia na Waitara tunasonga mbele Tarime Vijijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, ukienda Tarafa ya Uchugu, Susuni kuna jengo la mama na mtoto, Mwema utakuta kuna Kupetire Sekondari. Ukienda Sirari kuna Bukura Sekondari, Mradi wa Maji, taa za barabarani, barabara zinalimwa, madarasa yamejengwa, fedha za *CSR* zimefika Sirari.

Mheshimiwa Naibu Spika, nenda Pemba utakuta pale Nyaibara Sekondari, maabara ya kisasa inapatikana, mradi wa maji upo, na umeme utawaka hivi karibuni. Vilevile, ukienda Regicheri, sekondari mbili, zahanati inapatikana, barabara zimelimwa, madarasa yamejengwa mpaka chekechea imepatikana pale Regicheri. Mama Samia yupo, tunasonga mbele 2025. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukienda kule Inchage, Ganyange Sekondari, kuna mradi wa maji. Vilevile, ukienda Nyakarima kuna zahanati inajengwa. Nenda kule Magoto, kituo cha afya cha

zaidi ya shilingi milioni 500 kipo, magari ya wagonjwa manne Tarime Vijijini. Kazi na utu, Samia na Waitara, Tarime Vijijini tunasonga mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukienda kule Kibasuka, Genge sekondari, Nyarwana pale, uende mpaka pale Magoto, Nyarero, Zahanati utaikuta, pamoja na Mradi wa Maji. Vilevile, nenda Seroneta - Rozana kazi inaendelea katika eneo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukienda pale Bonchugu, nenda Nyanungu, Getena, sekondari mpya inajengwa. Kuna mradi wa maji na tumepata *High school*. Vilevile, barabara inapitika kutoka Tarime Mjini, inakwenda mpaka Mriba, inakwenda mpaka Nyanungu na Kwihancha.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, ukienda Gorong'a zahanati ipo, na mradi wa maji upo. Ukienda Nyarukoba, kituo cha afya, zahanati na dawa zipo. Ukija Itiryo kwenye Kata yangu, sekondari ipo, zahanati ipo, umeme umewaka, na barabara inapitika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda pale Mriba, tumejenga maabara, tumepata *X-Ray machine* ya kisasa ya kidigiti pale Sirari na unaipata pia Nyamwaga. Ninavyozungumza, hivi sasa pale Nyamwaga kuna *ICU* utafikiri upo Ulaya kumbe upo Tarime Vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi na utu, tunasonga mbele na Mama Samia 2025. Ninaposema Tarime Vijijini, hatuna mbambamba, maana yake ni hii ninayoizungumzia. Wananchi wa Tarime Vijijini na Wananchi wa Mkoa wa Mara wanajua kila mahali ukigusa Mama Samia yupo na pochi limetema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi iliyobaki kwa Watanzania na kwa Wabunge wa Chama cha Mapinduzi, chama kimefanya vizuri, mgombea mwenza yupo, na Wa-*NEC* wamefanya vizuri na ratiba imewekwa sawa, tarehe 28 tunavuta fomu na ushindi upo. Hao wengine acha wahangaike na ya kwao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Watanzania kazi imekwisha na Mama Samia. Mliotaka maendeleo, shule, barabara, maji, na madarasa, michango haipo. Mama Samia Mungu akupe nini? Tunakuombea uzima na Mungu akubariki. Mheshimiwa Mchengerwa, kazi uliyoifanya TAMISEMI na Wakuu wa Mikoa, Wakurugenzi, Wakuu wa Wilaya na Watendaji mbalimbali, sisi tunasubiri muda na ratiba ya Tume ya Uchaguzi tumalize kazi, turudi humu ndani kuendelea kuwatumikia Watanzania. Chama cha Mapinduzi kimepata kibali kwa Mungu, nani apinge? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hapo, naunga mkono bajeti hii ya Chama cha Mapinduzi, Bajeti ya TAMISEMI, bajeti ya wananchi trilioni 11 kwa 100% kwa niaba ya Wananchi wa Tarime Vijijini, Mkoa wa Mara na Kanda ya Ziwa…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Haya ahsante…

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, tutakuwa bega kwa bega kutafuta kura za Mama Samia, Dkt. Nchimbi na Chama cha Mapinduzi. Tunataka Halmashauri zote CCM, majimbo yote CCM, Serikali yote CCM, kila mahali CCM, ukienda chumbani CCM, barabarani CCM, kwenye msiba CCM, ukienda sokoni CCM, kwenye Vijiwe CCM, kwenye gari yako CCM. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana na Mwenyezi Mungu akubariki saba. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Kanyasu, jiandae Mheshimiwa Kapinga na Mheshimiwa Kapufi.

**MHE. CONSTANTINE J. KANYASU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana, nami naomba nianze kwa kuunga mkono hoja. Pia, naomba nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu Mawaziri kwa hotuba nzuri ya bajeti ambayo wameitoa. Vilevile, watendaji wote wa Wizara ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ambavyo wachangiaji wengi wamezungumza, nichukue nafasi hii kipekee kabisa kumpongeza Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kazi kubwa ambayo ameifanya nchi nzima, lakini hasa katika Mkoa wangu wa Geita na Jimbo la Geita Mjini.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilipata nafasi ya kuchangia kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, lakini naomba nirudie kwamba wananchi wa Geita tunamsubiri kwa hamu na tunasubiri uchaguzi kwa hamu. Sisi tulishamaliza, yako mambo makubwa mengi ambayo ameyafanya na kwa kweli itakuwa ni dhambi kubwa kwa mtu yeyote ambaye leo hayaoni.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, namshukuru sana Mheshimiwa Waziri. Baada ya kuwa amepata Wizara hii tulikuwa na ombi letu la muda mrefu sana Geita la kupata Manispaa. Vilevile, wananchi wa Geita wanafahamu kuja kwa Manispaa kunakuja na neema nyingi. Kwa hiyo, atufikishie shukrani zetu kwa Mheshimiwa Rais, kuifanya Geita kuwa Manispaa. Hata hivyo, nimeona kwenye bajeti yake iko ndani ya Manispaa na Miji 33 ambayo imeingizwa kwenye mpango kabambe wa uendelezaji. Nashukuru sana Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la pili, nawashukuru sana viongozi wetu Wakuu wa Mkoa. Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa, Martin Shigela, anafanya kazi yake vizuri sana. Yeye pamoja na Katibu Tawala wa Mkoa, lakini pia Mkuu wetu wa Wilaya, Bwana Hashimu Komba, kijana mchapakazi kweli kweli, pamoja na Mkurugenzi Bwana Yefred Myenzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naweza kusema kwamba, hata unapokuwa nje ya Bunge, unaona jimbo liko salama kwa sababu viongozi hawa wanafanya kazi kweli kweli na wanasema kazi ambazo zimefanywa na Chama cha Mapinduzi kwa niaba ya Serikali na kwa niaba ya Mheshimiwa Mbunge, tunawashukuru sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri, nimeona ongezeko la bajeti yako mpaka shilingi trilioni 11.9. Kwanza

tunampongeza sana, ni robo ya bajeti nzima ya nchi. Yaani bajeti yote, ukichukua robo imekwenda TAMISEMI. Hii ni ishara kwamba, hii ni Wizara muhimu na ni Wizara kubwa, lakini ni Wizara ambayo wananchi wanaitegemea. Hizi shilingi trilioni 11.9 zinakwenda kumgusa kila Mtanzania katika kila kona ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, wamesema wenzangu kwamba, ni kama Wizara zote ziko TAMISEMI. Hata watu wa Wizara ya Maji, na hata Wizara ya Ardhi ambao waliondoka, ukiangalia vizuri kule chini wanasimamiwa na viongozi ambao wanasimamia Ofisi ya Rais, TAMISEMI. Maana yake hii ni Wizara inayogusa kero, inayogusa changamoto ambazo zinagusa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi wananchi wa Geita Mjini, tunataka tukuhakikishie kwamba utekelezaji wa bajeti hii pamoja na miaka mingine iliyopita ndiyo chagizo la kusema tunampa Mama yetu Samia miaka mitano tena.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kuzungumza changamoto iliyozungumzwa na Kamati. Kamati ya TAMISEMI imesema kwenye ukurasa wake wa 82, "Kamati imebaini kuwa Mkoa wa Geita peke yake una takribani bilioni 18 zinazotakiwa kutumika kama CSR zikiwa hazijatumika kwa sababu mbalimbali." *Actually,* siyo shilingi bilioni 18, tuna zaidi ya shilingi bilioni 27 ambazo ni haki ya wananchi wa Geita. Kinachotokea katika sehemu hii ni kanuni ambayo tumeshaieleza kwa Mheshimiwa Waziri wa madini na changamoto ameiona.

Mheshimiwa Naibu Spika, huu uwajibikaji kwa jamii ni sheria na wala siyo hisani, lakini namna ambavyo inachukuliwa na mgodi ni kama vile anakupa *offer* ya bia au chakula. Kwa hiyo, kuna muda anafikiri ni haki yake kuzuia hiyo pesa isitumike, jambo ambalo siyo sahihi. Sasa tumetoa mapendekezo kwenye kanuni na tumesema wao wabaki na pesa zao kwenye akaunti, waziruhusu halmashauri zitangaze kazi, zipate wazabuni kwa sababu zina uwezo wa kuwasimamia wale wazabuni.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapotenga pesa za *CSR* na wakazisimamia wao, wanatafuta wazabuni wa bei mara tatu

zaidi. Kwa mfano, wanaweza wakatafuta wazabuni 25, wana mtu mmoja peke yake wa kusimamia hizi kazi, matokeo yake kazi moja inachukua miaka miwili, mitatu na washindwa kuzimaliza.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa umezuka mgogoro mkubwa, wameshindwa na tunazungumza mambo hatufiki mwisho. Hata hivyo, tunamshukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Madini, amelichukua hili na juzi baada ya Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa kuchukia na kuwafukuza kwenye kikao hawa *GGM* baada ya kuonekana wanaleta dharau, Mheshimiwa Waziri ameamua kuingilia na kupata suluhu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni dharau ya hali ya juu sana. Wanasema barua ya kuruhusu miradi iendelee ilicheleweshwa kutoka Ofisi ya Rais, TAMISEMI. Maana yake wanamwadhibu Waziri wa TAMISEMI, wakati wanajua Waziri wa TAMISEMI yuko Ofisi ya Rais. Wanasema kwamba, ilichelewa kujibiwa kuwa sasa miradi itekelezwe. Sisi kwenye sheria tumetunga kwamba, pesa isipotumika ndani ya muda itavuka mwaka. Wao wakaja na ajenda kwamba baada ya muda kuchelewa wanarudisha pesa *South Africa*.

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa, na nilimwambia Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa kuwa, kwa mara ya kwanza wananchi wa Geita wamegundua kwamba hapa Serikali ipo. Aliwafukuza na aliwaambia, "Kama mnadhani mko hapa Geita kwa ajili kufaidika ninyi, na wananchi wasifaidike, sasa kuanzia leo sitaki mawasiliano na ninyi kwenye ofisi yangu." Tangu wakati huo, tumeanza kuona wakiwa na nidhamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hawa watu ni wakorofi sana. Wananyanyasa sana wafanyabiashara, wananyanyasa sana watumishi. Mtumishi akipatikana na kosa dogo anakuwa *blacklisted* na hawezi kufanya kazi sehemu nyingine yoyote kwa sababu wanapeana taarifa. Maana yake ni kwamba, kuna muda wanafikiri wana Serikali ndogo kwenye eneo lile au Tanzania. Mimi nasema tunampongeza Mheshimiwa Waziri kwa kusimamia zoezi hili, lakini tunaitaka Serikali iwe kali zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tulipitisha sheria hapa ya 16% *percent* ya *free carried interest,* wao peke yao kwenye migodi yote Tanzania wamekataa kusaini. Kuna maeneo ambayo viongozi wote wakuu wa nchi walishatoa maelekezo wawalipe watu waondoke. Wao peke yao wamekataa kusaini. Maana yake hawa jamaa kuna muda wanatutazama sisi Watanzania wanatuona kama ni wajinga.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuendelee kuwabana, na Kamati imenifurahisha sana kuliweka jambo hili kwenye bajeti kwa sababu huu mgogoro sasa uko katika mikoa yetu ya Tarime, kwetu na maeneo mengine wanaambukizana. Mheshimiwa Waziri, nakushukuru sana na tutaendelea kuchangia, lakini tutaendelea kuwabana mpaka watakapotimiza.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili ni kwenye *TARURA*. Mheshimiwa Waziri, nakushukuru sana, nilikuomba pesa ya Daraja la Nyakabale, ukanipatia shilingi milioni 600 daraja limejengwa. Nikakuomba pesa ya Daraja la Igwata ambalo lilichukuliwa na maji, ukanipatia shilingi milioni 400 na daraja limejengwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, shida kubwa tuliyonayo, wale wakandarasi baada ya kumaliza ujenzi wa madaraja, hawajaruhusu magari yapite kwa sababu hawajalipwa. Vilevile, zile barabara zinazounga darajani hazijajengwa…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa malizia…

**MHE. CONSTANTINE J. KANYASU:** Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba sana Mheshimiwa Waziri atusaidie wale wakandarasi walipwe. Hata tulipopitisha *supplementary budget* tulitarajia watalipwa, hawakulipwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunampigia Seff anapokea simu na kwa kweli ni mtu muungwana sana, lakini anakwambia hana hela. Tusaidie hao walipwe ili hizi barabara zipitike, kwani ndizo zinazoleta mazao Geita Mjini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana, ahsante sana na ninaunga mkono hoja.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa tumebakiwa na wachangiaji saba. Naongeza muda mpaka hapo tutakapomaliza.

Mheshimiwa Kapinga, jiandae Mheshimiwa Kapufi.

**MHE. BENAYA L. KAPINGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Awali ya yote nami nianze kwa kuunga mkono bajeti hii kwa asilima mia moja. Pili, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri. Kwa kweli wanasema mnyonge mnyongeni, haki yake mpeni. Hata hivyo, huyu sio mnyonge. Mheshimiwa Waziri anafanya kazi. Wamesema wenzangu hapa, kila Wizara aliyopelekwa kwa kweli unaiona *impact*. Kwa kweli hongera sana Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nawapongeza pia Mheshimiwa Dkt. Dugange, Mheshimiwa Zainab, pamoja na watumishi wote wa Wizara hii ya TAMISEMI, wakiongozwa na Ndugu Adolf Ndunguru, kwa kweli wanafanya kazi nzuri sana ya kumsaidia Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, nampongeza Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan. Niliongea kwenye bajeti ya Waziri Mkuu kwa mambo aliyoyafanya Tanzania, lakini mambo aliyoyafanya kwenye Jimbo langu la Mbinga Vijijini, nikianza kuyasema hapa, *session* yote hii utaniachia mimi nianze kuorodhesha. Kwa hiyo, sitayasema yote, bali nitayasema machache tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la kwanza ni kwa kutuletea viongozi wazuri Mkoa wa Ruvuma wakiongozwa na Kanali Abbas, yupo hapa. Kwa kweli anafanya kazi nzuri sana. Mkoa wa Ruvuma umetulia na anachapa kazi vizuri na maendeleo yanaonekana.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, kwa maana ya wilaya yangu, ni kwa kutuletea Mkuu wa Wilaya ambaye anafanya kazi vizuri sana. Tatu, ni kwa kutuletea Mkurugenzi, Kashushura; anafanya kazi nzuri sana. Ni kwa nini nayasema haya? Kashushura huyu aliyekuja hivi karibuni, sisi huko tulikotoka tulikuwa na mapato ya kawaida sana, lakini leo hii tumefika shilingi bilioni 10 kutoka kwenye shilingi bilioni mbili miaka iliyotangulia. Kwa hiyo, ni mtu wa kumpongeza sana, amekuwa ni mbunifu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tulikuwa na vyanzo viko pale. Siku zote hatukuviona, lakini hivi karibuni kaja yeye, tuna makaa ya mawe tunachimba. Tulikuwa tunachukua tozo kwenye malori yanayoanzia kwenye *dry port* kupeleka huku, lakini kule chini tunakochimba tulikuwa hatuchukui.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo hii Kashushura kaja akaweka utaratibu, tumetunga na sheria na Mheshimiwa Waziri hakusita akaisaini. Leo hii kwa chanzo hicho tunapata mapato mengi. Leo kimetufikisha kwenye shilingi bilioni 10 tena kabla ya kumaliza mwaka wa mapato. Mheshimiwa Waziri chanzo hiki kinafanya vizuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nawapongeza na kuwashukuru wenzetu au Kampuni yetu hii ya Jitegemee, inatekeleza kanuni hii vizuri na wengine pia wanatekeleza. Ipo kampuni moja imeleta shida. Imegomea kutozwa ushuru ambao kampuni nyingine zote zinatozwa, yenyewe imegoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa shida sijui ni nini? Ile ni kanuni na Waziri ameisaini na wameeleweshwa na walishirikishwa vizuri tu wakati wa kuipitisha hiyo kanuni. Leo hii wao wanaongoza kugomea kanuni hii. Sasa wameongezeka, wako watatu, wanne na wenyewe wanamuiga yule aliyetangulia kusema mimi sitoi tozo hiyo. Wanaturudisha nyuma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nazishukuru zile kampuni nyingine wakiongozwa na Jitegemee, wameendelea kutoa ule ushuru vizuri na leo hii tuna mapato mazuri sana. Nawapongeza sana

Mkuu wa Mkoa na timu nzima kwenye Mkoa wetu wa Ruvuma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, niendelee kuishukuru sana Serikali hii ya Awamu ya Sita. Awamu hii sisi tulikuwa na shida sana na eneo hili la afya. Tulikuwa tunategemea zahanati na hospitali hasa za Wamisheni, lakini nina fahari kutamka hapa mpaka sasa tayari tumefungua huduma 24 za kiafya, ikiwemo hospitali ya wilaya humo na vituo vya afya vitano na zahanati za kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, mwaka huu wa fedha tunaokwendanao tumepeleka fedha kwenye zahanati 17. Ukija kuongeza na zile 24 maana yake tutakuwa na zahanati na sehemu za kutolea huduma za kutosha kabisa kwenye halmashauri yetu ya Mbinga Vijijini. Naishukuru sana Serikali hii ya Awamu ya Sita kwa sababu imeweka mazingira mazuri. Inatoa fedha, lakini na wale watumishi pale kwenye ngazi ya halmashauri wanapata nafasi ya kukusanya mapato.

Mheshimiwa Naibu Spika, baadhi ya fedha hizi ni mapato yetu ya ndani ndio yameenda kutekeleza hii miradi kwa mfano hizi zahanati 17, tunaishukuru sana. Ombi langu hapo, kwa sababu tulikuwa hatuna sehemu za kutolea huduma, sasa tumepata maeneo mengi ya kutolea huduma lakini tunashida kubwa sana ya watumishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa 70% hatuna watumishi. Tuna watumishi 300 tu ambao kwa kupata ile hospitali ya wilaya ndio watumishi wanaotakiwa kuwa kwenye hospitali ya wilaya. Kwa hiyo, kwa maana hiyo hizi sehemu nyingine zote hazina watumishi. Nakuomba sana na sisi utufikirie.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine hapo hapo, hatuna *ambulance*. Tunashukuru tumepata *ambulance* moja na nyuma kule tulikuwa nayo moja ambayo sasa imechakaa. Tunaomba sana katika mgao huu unaondelea, na sisi mtufikirie. Hapa niwe muwazi, kwa kweli Mheshimiwa Waziri Serikali yetu inafanya vizuri. Imenunua magari mengi. Utaratibu wa kuyagawa yale magari ndiyo naona kidogo siyo mzuri sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, haiwezekani kwenye Halmashauri kubwa kama ile ya Mbinga yenye milima na mabonde inapata gari moja, lakini ziko halmashauri ndogo zinapewa magari mawili mpaka matatu. Kwa hiyo, naomba sana wakati wa mgawanyo huu, wataalamu wetu waangalie isiwe tu kwamba sasa yanatolewa tu kwa sababu yapo, hapana. Lazima tuangalie na uhitaji. Gari moja haliwezi kuzunguka kwenye Halmashauri ile ya Mbinga Vijijini ambayo ni kubwa sana. Naomba sana tupewe kipaumbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, wakati tunaingia madarakani, halmashauri yangu ilikuwa na upungufu wa sekondari nyingi sana, lakini nashukuru mpaka sasa tumebakiwa na sekondari mbili tu; ya Ngima pamoja na Mhongozi. Mwaka 2024 wakati Mheshimiwa Rais amefanya ziara nilimwomba pale na alikiri akasema tayari ametutengea fedha pale shilingi milioni 900. Kilichobaki kwa watumishi wetu ni kwenda kusimamia. Naomba Mheshimiwa Waziri tutekeleze hii ahadi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, nashukuru, sasa hivi, mwaka huu wa fedha uliotangulia tumepata sekondari sita zinajengwa. Tumejenga Amani Makoro, Kitumbalomo, Muungano, Litembo, Langiro na Nyoni. Zote hizi tayari zimeshaanza kuchukua wanafunzi wa Kidato cha Kwanza na nyingine zimefika Kidato cha Pili. Tunaishukuru sana Serikali ya Awamu ya Sita kwa utekelezaji huu mzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, nashukuru sana kwa mpango huu wa *TARURA.*

*(Hapa kengele ililia kuashirtia kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Malizia.

**MHE. BENAYA L. KAPINGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri, kwani *TARURA* wamefanya kazi nzuri. Tulikuwa na bajeti kidogo, tumeongezewa bajeti. Sasa hivi barabara nyingi sana kwenye Jimbo la Mbinga Vijijini zinapitika vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi langu, tumeleta maombi maalum huko ya barabara muhimu sana na tumeleta maombi ya dharura. Tunaomba sana, *Engineer* Seff anafanya kazi nzuri, mimi mara kadhaa nimemwona na amenisaidia sana, atusaidie kwenye yale maombi ya dharura yaliyofika huko na yale maombi maalum.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, *termination* ile tuliyopeleka, maana yake tulipata wakandarasi na baadhi yao hawakufanya vizuri. Kwa hiyo, Mkoa umepeleka maombi ya kuwa-*terminate* wale. Naomba sana tuwabadilishe ili yale madaraja matano yakamilike.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante.

**MHE. BENAYA L. KAPINGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, apatikane mkandarasi, tukamilishe yale madaraja, Ahsante sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Naibu Waziri. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, mambo ni mengi unaruhusiwa kumwandikia Waziri sasa hivi mahitaji yako mengine ambayo unayahitaji.

Waheshimiwa Wabunge, sasa namwita Mheshimiwa Kapufi, wajiandae Mheshimiwa Butondo, Mheshimiwa Kuchauka, Mheshimiwa Mtaturu, Mheshimiwa Stella na tutamalizia na Mheshimiwa Nusrat. *(Makofi)*

**MHE. SEBASTIAN S. KAPUFI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Kama ilivyo ada, nami nakushukuru Mheshimiwa Waziri na timu nzima ya TAMISEMI. Nikisema timu nzima maana yake tutakwenda kwa Wakuu wa Mikoa, Makatibu na wengine wote ambao wanahudumu kwa maana ya TAMISEMI, bila kumsahau Mkuu wangu wa Mkoa ambaye ni Mrindoko na timu nzima ya Mkoa wangu wa Katavi ambao wananipa ushirikiano mkubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mara ya mwisho tulisafiri katika maeneo mbalimbali nchini. Hii niseme kwamba, kuhudumu kwenye Kamati hii ya TAMISEMI, kumenipa faida moja na wote ndani Bunge hili, siyo kwamba Kamati nyingine siyo muhimu, bali nilichojifunza kuhudumu kwenye Kamati hii kumesaidia kutupa picha, na hata unapokuwa unaongea, unaongea kwa picha pana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mara ya mwisho tulikwenda mpaka Kiteto. Nilijifunza jambo moja na hili tuliweke kwa maana ya mtandao mzima wa nchi nzima. Mlipokuwa mnazungumzia habari ya kugawa fedha kwa kuangalia jiografia ya maeneo, tafsiri yake ni hii. Tumekwenda Kiteto, tumekuta katika ujenzi wa shule mchanga anautoa mbali na gharama yake inafika mpaka shilingi 300,000/= kwenda 400,000/=.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kusema nini? Mlipokuja na wazo kwamba mtaanza kugawa fedha kulingana na jiografia ya maeneo, ni kwa sura hiyo. Maeneo hayafanani. Gharama za uchukuzi hazifanani. Kwa hiyo, hilo kwenye kumbukumbu zangu natamani kumkumbusha Mheshimiwa Waziri, tuendelee kugawa fedha kwa kuangalia jiografia za maeneo, gharama ya vitu na vitu vingine vya namna hiyo. Tutakuwa tumewasaidia sana watu wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kiujumla pia tumejifunza kwa maana ya ujenzi wa madaraja ya mawe. Ni teknolojia rahisi ambayo inapunguza gharama. Kwa hiyo, hili nalo natamani maeneo yote yenye changamoto, ujenzi wa madaraja ya mawe uendelee kuzingatiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa na changamoto ya Mfumo wa *NeST* na maeneo mengine kazi zimesimama kwa sababu hiyo. Naendelea kukumbusha wataalamu waendelee kuwaelimisha watu wetu kuhusu Mfumo mzima wa *NeST* na isiwe kikwazo, iwe ni namna ya kutusaidia kufanya ufumbuzi katika maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, tulikutana na changamoto ya watu ambao wanapewa ukandarasi. Kwa mfano, pale Kahama ni watu wenye uwezo mdogo. Kwa hiyo, naomba uchunguzi wa hawa watu ambao tunakwenda kuwapa kazi wajaribu kuzingatia hilo kwa sababu kuna mtu unakuta kapewa kazi uwezo ni mdogo, hivyo anakwamisha shughuli za watu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, nikitoka hapo, nilikuwa naomba eneo la *TACTIC*. Manispaa ya Mpanda tuko kwenye awamu ya pili ya *TACTIC*. Naomba kulisogeza mbele jambo hili kwa kasi kubwa. Tuko awamu ya pili. Nimetoka naongea na mhandisi wangu anasema yuko Tanga kwa ajili ya kuendelea kupewa mafunzo ya jinsi gani ya kufanyia kazi mradi huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni mradi mzuri. Tuna kilometa takribani 8.5 za lami kwa Mji wa Mpanda. Pia, tutakuwa na soko la kisasa eneo la Kazima. Ni *project* nzuri. Kama huko nyuma kwa kupitia Mradi wa *ULGSP* tulipata kilometa 7.7 ikaupendezesha mji wetu ikiwa ni pamoja na Stendi ya Mizengo Pinda, *this time around* tukipata hizo kilometa 8.25 itatusaidia sana kuuboresha Mji wetu wa Mpanda na kuupa sura nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, rai yangu na ombi langu, nafahamu kuna changamoto za fedha, lakini wenzetu wa *TARURA* kuna kazi ambazo zimefanyika, wakandarasi hawajalipwa. Naomba sana ili waweze kutangaza kazi nyingine tuwalipe wale watu ambao wametufanyia kazi hizo za mwanzo.

Mheshimiwa Naibu Spika, najua tuna changamoto kwenye barabara ya kutoka Misunkumilo kwenda Milalashongo. Kazi zimesinzia na ni barabara muhimu. Kuna eneo la daraja ambalo watu wanashindwa kuvuka na kwa sisi wanasiasa tumekuwa tukipata kelele nyingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, ukienda Kata ya Kakese ziko barabara kutoka Mabanini kwenda Mbugani na kutoka Kawanzige kote huko hakupitiki. Unafika sehemu ukienda kuwatembelea wananchi wanatamani kuona Mbunge

mwenyewe ukiwa umekwama na gari lako ili iwe fundisho. Sasa tusaidieni ili hizi changamoto tukae nazo mbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikumbushe pia kwa maana hiyo hiyo. Nakumbuka kuna barabara ya kutoka Ilembo kwenda Dirifu na baadaye kwenda Itenka. Mtendaji Mkuu wa *TARURA* katika ahadi zake arejee kwenye kumbukumbu zake, kilometa tatu za lami ni ahadi ya muda mrefu. Wananchi wanaikumbuka kwa sababu kwenye majukwaa tumezungumzia jambo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la mwisho, lakini siyo kwa maana ya umuhimu. Nafahamu nimesema kwa maana ya awamu hii *TACTIC* tumepewa kilometa hizo, lakini ipo barabara ya kimkakati ya kutoka Mwamkulu kuja Kakese na baadaye kumalizia Misunkumilo. Ni kwa nini nasema barabara hii ni ya kimkakati? Tuna mradi mkubwa wa umwagiliaji wa shilingi bilioni 31 kwa maana ya eneo la umwagiliaji la Mwamkulu, tunategemea wananchi hawa watazalisha mara tatu kwa mwaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa uzalishaji huu mkubwa bila kuwa na barabara na mkumbuke Katavi kwa ujumla wake ni mkoa wa kimkakati kwa maana ya uzalishaji. Sisi tukiomba barabara hii, lengo letu ni ili ninyi watu wa Dodoma tuwaletee chakula, watu wa Dar es Salaam tuwapelekee chakula, na watu wa Shinyanga tuwapelekee chakula.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tutakapofungua barabara hizi itasababisha ninyi wenzetu ambao mko huku wakati mwingine mna shida ya mvua, sisi kule mvua siyo tatizo kiasi hicho. Sasa mnatamani kupata chakula, tutawafikishiaje kama barabara hizi hazipitiki? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuyasema hayo, naunga nmkono hoja.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Tunaendelea na Mheshimiwa Butondo, wajiandae Mheshimiwa Kuchauka na Mheshimiwa Miraji.

**MHE. BONIPHACE N. BUTONDO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia katika hotuba hii ya bajeti yenye jumla ya shilingi trilioni 11.7 ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI.

Mheshimiwa Naibu Spika, kimsingi naunga mkono hoja. Kwanza, naomba niendelee kutoa shukrani kwa Mheshimiwa Rais wetu, pongezi nyingi zimwendee yeye mwenyewe. Kazi kubwa ya kuleta maendeleo katika nchi yetu inayofanyika imekuwa ya mfano kwa nchi za Afrika na hata dunia nzima. Ndiyo maana Mheshimiwa Rais wetu ameendelea kupongezwa na kupewa tuzo mbalimbali za Kimataifa kutokana na utendaji kazi uliotukuka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue fursa hii pia kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mchengerwa, Naibu Mawaziri Mheshimiwa Dkt. Dugange pamoja na dada yangu Mheshimiwa Zainab kwa namna ambavyo wanamsaidia sana Mheshimiwa Mchengerwa na kwa ujumla wanavyomsaidia Mheshimiwa Rais katika kuhakikisha kwamba Wizara hii muhimu inafanya kazi vizuri. Kwa kweli wamekuwa msaada mkubwa sana kwa Mheshimiwa Rais kwa sababu wamekuwa wakitekeleza majukumu yao kwa weledi mkubwa sana. Sisi Wabunge tunashuhudia haya matendo makubwa wanayoyafanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimpongeze Mheshimiwa Mkuu wangu wa Mkoa, Mheshimiwa Anna Mringi Macha, kwani amekuwa Mkuu wa Mkoa wa mfano. Kwa kweli sisi wananchi wote wa Mkoa wa Shinyanaga na viongozi kwa pamoja anatuongoza na tunaona mabadiliko makubwa ya jitihada za kimaendeleo kwa sababu kazi nyingi sasa zinakwenda kwa kasi kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, tunaona namna anavyosimamia na kufuatilia utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi katika Mkoa wake. Kwa hiyo, naomba nimpongeze sana Mkuu wa Mkoa huyu wa mfano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, namshukuru na kumpongeza Mkuu wangu wa Wilaya ndugu yangu Matindi, mmoja kati ya vijana wenye kasi. Ametoka katika nafasi ya u-*DAS* na sasa kapewa nafasi ya kuwa Mkuu wa Wilaya ya Kishapu na kazi anayoifanya ni kubwa. Kwa muda mfupi amekuwa akifanya mambo makubwa sana. Yapo mabadiliko makubwa katika Wilaya ya Kishapu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni lazima niipongeze *crew* yake ya wilaya kwa sababu tunajua kuna *PCCB* na vyombo vingine ambavyo vinamsaidia kuhakikisha kwamba mambo yanakwenda vizuri. Ushirikiano ni mkubwa sana na tunaona jitihada kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, naomba nimpongeze Mkurugenzi wangu wa Halmashauri Ndugu Emmanuel Johnson. Ni Mkurugenzi ambaye ametutoa mbali sana. Sasa tunaye kwa mwaka wa tano, lakini jitihada aliyoifanya ni kubwa sana. Halmashauri yetu ilikuwa inakusanya shilingi bilioni 1.7 kwa mwaka. Leo tunavyozungumza, tumekwenda kwenye shilingi bilioni 3.4. Ni jitihada kubwa sana, na ni kama imekwenda mara mbili yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ukusanyaji wa mapato ni wa hali ya juu na usimamizi wa fedha na wenyewe umekuwa ni mzuri sana. Pongezi hizi ni lazima tumrudishie Mkurugenzi wetu Ndugu Emmanuel Johnson. Kwa kweli tunamtakia heri sana katika kipindi kinachokuja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, nampongeza Mwenyekiti wa Halmashauri, ndugu yangu Jijimya pamoja na Waheshimiwa Madiwani wote. Kazi hii ya kimaendeleo bila Madiwani, na wao kuwa wafuatiliaji na wasimamizi wazuri wa fedha zinazotoka Serikalini, huwezi ukaleta maendeleo. Kwa hiyo, nawapongeza sana Waheshimiwa Madiwani chini ya ndugu yangu Mheshimiwa Mwenyekiti wa Halmashauri Ndugu Jijimya kwa namna ambavyo tunafanya kazi vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, niwapongeze wananchi kwa namna ambavyo kwa kweli kwa ujumla tumekuwa tukisimamia

fedha za umma zinapokuja maeneo mbalimbali kwa sababu hata wananchi wako tayari kuona kwamba miradi inatekelezwa katika kiwango na ile *value for money* inaonekana. Pale panapokuwa na sintofahamu, wamekuwa wakipaza sauti kukataa kile kinachofanyika kinyume.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie upande wa barabara. Kishapu tumefanya vizuri sana. Mwaka 2020 tulikuwa na kilometa 670 tu. Sasa tuna kilometa 1,100. Hizi ni barabara zinazopitika na kata zote 29 sasa zinapitika.

Mheshimiwa Naibu Spika, jitihada tunayoifanya ni kuhakikisha sasa tunaunganisha vijiji, lakini tumetoka kwenye bajeti ya shilingi milioni 900, sasa tuko kwenye zaidi ya shilingi bilioni 2.5. Ni jitihada kubwa sana za Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan anafanya kazi kubwa ambayo kwa kweli lazima tumpongeze. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mji wetu wa Munze tulikuwa na kilomita moja ya lami, sasa tumekwenda kwenye kilomita nne na sasa tunakamilisha kilomita moja twende kilomita tano katika Mji wa Munze ambao kwa kweli kabla ya hapo tulikuwa katika maeneo ambayo hayakupendezesha mji wetu, lakini tumeweka taa, kwa kweli mji wetu unapendeza pakubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nipongeze sana jitihada za namna ambavyo mtiririko wa fedha unakuja japokuwa kwa kipindi hiki kidogo unasuasua. Kuna Kata ya Itilima ambayo haiendi vizuri. Kuna madaraja ambayo bila kujengwa kwa kipindi hiki Kata ya Itilima haipitiki. Naomba sana Mheshimiwa Waziri alione hili, Kata hii iweze kufanyiwa utaratibu wa kuletewa fedha hasa katika maeneo ambayo yana ukorofi wa makalavati na madaraja.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna daraja moja la Bulekela Mwajidalala. Hili ni daraja kubwa sana ambalo lilijengwa mwaka 2016/2017. Daraja hili halijaweza kuunganishwa na barabara inayoiunganisha daraja hili na bahati nzuri daraja hili linaunganisha Wilaya ya Igunga na Wilaya ya Kishapu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tumelijenga kwa shilingi bilioni 2.3, lakini barabara ya kusafiri kutoka eneo la Mwajidalala kwenda mpaka eneo la daraja, haipo, ni kama kilomita tatu, sasa ni kama tumeweka tu pale fedha, lakini daraja hili halifanyi kazi. Kwa hiyo, naomba tupewe fedha kwa ajili ya kutengeneza kilomita tatu kufikia daraja hili ili tuweze kuunganisha na wenzetu wa Igunga. Wenzetu wa Igunga kwa kweli wamefanya jitihada kubwa, wamejenga barabara mpaka usawa huo huo wa daraja hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie elimu ya msingi. Tumefanya vizuri, tumeongeza madarasa, na tumeongeza madawati bila kuchangisha wananchi. Kwa kweli tunamshukuru sana Mama Samia Suluhu Hassan kwa kuleta fedha nyingi, madarasa yetu sasa yanapendeza sana sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia tunamshukuru kwa shule kubwa za msingi mbili. Katika Shule ya Msingi Maganzo nimeletewa shilingi milioni 670, na Shule ya Msingi Vinenekeja Kata ya Igaga nimeletewa shilingi milioni 650. Hizi siyo fedha kidogo, ni nyingi sana sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nashukuru kwa shule za msingi sita ambazo zimejengwa kwa nguvu ya wananchi na mapato ya ndani ya Halmashauri. Hizi ni jitihada kubwa ambazo tunaenda nazo. Ombi langu tu ni maboma ambayo yameanzishwa na wananchi ambayo ni mengi sasa. Tunayo zaidi ya maboma 64 yanayohitaji tuungwe mkono. Nilikuwa naomba katika bajeti hii kwa kweli Wilaya ya Kishapu tupewe fedha ili waje kukamilisha haya maboma ambayo yamebaki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, elimu ya sekondari kuna Kata ambayo tumeletewa mpya Shagihilu shilingi milioni 670 sasa ,hivi iko kwenye asilimia 97; Mwaweja imeshakamilika, inafanya kazi, shilingi milioni 630; na pia Upigi shilingi milioni 650 sekondari hizi zinafanya kazi. Kwa hiyo, tunamshukuru sana Mama Samia Suluhu Hassan na sasa tumekuwa na kata zote katika Wilaya ya Kishapu zina sekondari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna Sekondari ya Masagala ambayo sasa hivi inaendelea kujengwa na yenyewe iko katika hatua nzuri sana, iko katika Kata ya Maganzo na hii ikikamilika itakuwa na gharama ya shilingi milioni 650. Hii ni kazi nzuri sana. Sekondari moja inaendelea kujengwa pale Mwasubi kwa nguvu za wananchi na mapato ya ndani ya Halmashauri. Tuna upungufu wa nyumba za walimu, tuna upungufu wa maabara karibu 53 ambazo zimeanzishwa kwa nguvu za wananchi. Tunaomba Serikali iweze kutukumbuka katika hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye afya tumejitahidi sana, tunayo hospitali ya wilaya nzuri inatoa huduma nzuri, vifaatiba vya kutosha, madawa ya kutosha, na sasa hivi tuna Madaktari.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri nakuomba kuhusu suala la Mwadui, tumeomba kupewa hospitali ya wilaya…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Malizia.

**MHE. BONIPHACE N. BUTONDO:** Mheshimiwa Naibu Spika, tumeomba hospitali iliyokuwa ya Mwadui irejeshwe kwa Halmashauri, bahati nzuri tumekubaliwa na Mheshimiwa Waziri, tunamshukuru sana. Tunachoomba ni kibali cha watumishi waliokuwa katika hospitali ya Mwadui.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Butondo malizia tafadhali.

**MHE. BONIPHACE N. BUTONDO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante naomba nishukuru sana kwa bajeti nzuri na Mheshimiwa Waziri tutaonana nawe, nitakuongezea baadhi ya maelezo ili uweze kunisaidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, Mheshimiwa Kuchauka, jiandae Mheshimiwa Mtaturu, Mheshimiwa Stella, na Mheshimiwa Nusrat.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa nafasi nami nipate kuchangia hotuba iliyopo mbele yetu. Kama ilivyo ada, nami nianze kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kunipa uhai na kuniwezesha kusimama mbele yako leo hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, nami nianze kwa kumshukuru sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Daktari Samia Suluhu Hassan, kwa kweli amelitendea haki Taifa hili kwa mambo mengi sana. Wananchi wa Liwale tunalo deni kwa Mheshimiwa Rais kwa mambo makubwa aliyotufanyia kwenye Wilaya yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapoendelea kumshukuru Mheshimiwa Rais, vilevile namshukuru sana na kumpongeza Mheshimiwa Omar Mchengerwa mwenye Wizara hii na wasaidizi wake wale Mawaziri wote wawili wanaomsaidia kwenye Wizara hii. Kwa kweli wanafanya kazi nzuri, kazi iliyotukuka na wataacha alama kwenye Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapomshukuru Mheshimiwa Waziri na wasaidizi wake bila kusahau Watendaji Wakuu wa Wizara hii wakiongozwa na Katibu Mkuu, ndugu yangu Ndunguru, na Makatibu wake wale wanne, kwa kweli wanafanya kazi nzuri na pongezi zote tunazoziona hapa ni kwa sababu watendaji hawa wanne wamesimama vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye Wizara hii yuko Mnyamwezi mmoja anaitwa Cheyo, ndiyo mwenye mipango. Tunamshukuru kwa mipango mizuri, tunaiona wizara hii inaenda vizuri, maana yake mipango yake imepangika vizuri na mnyamwezi yule anafanya kazi nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapomsifu Mheshimiwa Rais, na tunapoisifu Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, tunasema Serikali ya Chama cha Mapinduzi ni Serikali sikivu. Kwenye bajeti iliyopita nilitaja hapa nikasema, Wilaya ya Liwale haina majengo yanayokidhi kuwa na hadhi ya Wilaya, na hapa nilitaja majengo matano.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishukuru sana Serikali ya Chama cha Mapinduzi. Leo ninapozungumzia yale majengo yote matano yapo Liwale kwenye hatua mbalimbali, jengo la Halmashauri karibu linaisha, jengo la Mahakama limeisha, jengo la Ofisi ya Mkuu wa Wilaya limeisha, jengo la *TRA* linaenda kwisha, nimebakiza jengo moja tu la ndugu yangu hapa Waziri wa Mambo ya Ndani, yeye kidogo ameniangusha, bado lile jengo halipo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli Askari wale wanafanya kazi kwenye mazingira mabovu mno. Pamoja na kwamba mimi nilitoa shilingi milioni 10 pale kuwa-*support,* lakini ndugu zangu hawa wa Mambo ya Ndani nao wameniangusha. Imani yangu ni kwamba, kwa sababu bado tupo jengo hilo nitakwenda kulipata. Kwa hiyo, jambo hilo nashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sijamalizia shukrani zangu. Namshukuru sana Mwenyekiti wangu wa Kamati, Mheshimiwa Justin Nyamoga amefanya vizuri sana, ameitendea haki hotuba yetu. Hotuba ambayo imejaa weledi, hotuba ya kizalendo ameitendea haki, ameisoma vizuri na imejaa ushauri. Hapa naomba nimwambie Mheshimiwa Waziri, hotuba hii kama ataifuatilia na kuitendea haki, basi nchi yetu itakwenda vizuri sana na kila jambo litaenda vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie suala la *TARURA*. Kwa kweli taasisi hii wakati nachangia hotuba ya Waziri Mkuu nilisema kwamba, *TARURA* inafanya vizuri sana. Katika taasisi tatu, nne za nchi hii, *TARURA* huwezi kuiacha. Jambo kubwa ambalo linaikwaza *TARURA* ni ukosefu wa fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Liwale bado ni Wilaya ambayo ina barabara chache sana za lami. Wilaya ya Liwale, mpaka leo hii nina zaidi ya miaka 45, Wilaya ile ina kilomita tatu tu za lami. Naomba Mheshimiwa Waziri hebu ajaribu kuona ni namna gani wanaweza wakatusaidia?

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naleta maombi matatu kwenye Wizara hii. Ombi la kwanza la shule

chakavu. Naomba sana Mheshimiwa Waziri atufikirie kuona hizi shule ambazo zilijengwa miaka ya 1970, sasa hivi shule hizi zote hazina milango wala hazina madirisha, yaani mwanafunzi anaingia popote na kutokea popote.

Mheshimiwa Naibu Spika, shule hizi nazitaja chache kama mfano, Shule ya Msingi Kipule, Shule ya Msingi Mbaya, Shule ya Msingi Mangirikiti, Shule ya Msingi Mtawango, Shule ya Msingi Nduruka, Shule ya Msingi Kipelele, Shule ya Msingi Ngumbu, Shule ya Msingi Ngunja, Shule ya Msingi Naluleo, Shule ya Msingi Mpengele, Shule ya Msingi Mkundi, Shule ya Msingi Ndumiungu, Shule ya Msingi Makinda.

Mheshimiwa Naibu Spika, hizi shule ni shule chakavu, shule ambazo mwanafunzi anaingia popote na kutoka popote. Kwa hiyo, naomba sana sana tusaidie tuone namna gani tunaweza kusaidiana shule hizi zikapata majengo mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi la pili ni kuhusu vitendea kazi. Tunayo shida sana ya vitendea kazi kwa mfano magari. Idara ya Mipango haina gari, Idara ya Ujenzi haina gari, na hii Idara ndiyo Idara ambayo inasimamia miradi mingi ya fedha nyingi ambazo Mheshimiwa Rais analeta Jimboni kwetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, utaona kwamba, ufuatiliaji unaweza ukakuta wakandarasi wa ndani amepewa *site* lakini huyu ili aweze kufanya vizuri lazima Injinia afike pale. Anafikaje? Kwa kutumia gari, na kuombaomba, anaenda kuomba gari labda elimu. Kama kuna mambo ya mitihani, basi magari hayapatikani.

Mheshimiwa Naibu Spika, maana yake ni kwamba, zipo kazi aidha, zisimame au zifanywe chini ya kiwango. Kwa hiyo, tunaomba sana Idara ya Mipango, Idara ya Ujenzi, Idara ya Kilimo na Maliasili hawa wote hawana magari. Naomba sana Mheshimiwa Waziri aone namna ya kutusaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ni la utawala bora. Tunapozungumzia utawala bora maana yale ni kwamba

tunasogeza huduma kwa wananchi na kusogeza huduma kwa wananchi, maana yake ni nini? Tunayo maeneo mengine ambayo ni makubwa sana kiutawala. Sasa yale maeneo makubwa maana yake, kuwafikia wananchi kiutawala inakuwa ni ngumu. Tunayo maombi kwenye Wizara hii, tunaomba kugawa maeneo ya utawala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile tunazo Kata ambazo ni kubwa sana, ni ngumu sana kiutawala kwa sababu Kata zetu zimetawanyika sana na ziko mbali. Umbali kutoka kwenye Kata mpaka kwenye Kijiji ni mkubwa sana kiasi kwamba huduma zinakuwa ni ngumu kuwafikia. Kata hizi ni Kata ya Liwale B. Tumeomba kuigawa na kwenye vikao vyetu, tumeshapitisha, tunaomba tuigawe Kata ya Liwale B, Kata ya Mbaya na Kata ya Mangirikiti.

Mheshimiwa Naibu Spika, Liwale Mjini pia tunazo Kata tatu, Kata hizi zote za Liwale Mjini nazo ongezeko la watu ni kubwa sana ikikupendeza Mheshimiwa Waziri ufikirie kwenye ofisi yako uzigawe hizi Kata tatu Kata ya Nangando, Kata ya Likongowele na Kata Liwale Mjini. Kwa hiyo, kwa ujumla wake, hizi Kata sita zote kama ikikupendeza maeneo haya yangefanyiwa utaratibu ili Kata hizi ziweze kugawanywa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa, ni suala la watumishi. Suala la watumishi Wilaya ya Liwale ni kizungumkuti, wanahama sana. Wanaohama ni wengi kuliko wanaoletwa pale Wilayani, hasa kwenye kada ya ualimu na kada ya afya, watumishi wanahama sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo hili ni kubwa na wanasema kwamba sasa hivi wanahama kupitia mtandao, lakini hawa wanaohama kwa njia ya mtandao wanakidhi vigezo? Hili ufumbuzi wake mimi nimeona twende tufanye ajira hizi kwa kanda kwa sababu sidhani kama mtu atatoka Mtwara akaenda Liwale ataomba kuhama au akitoka Songea, lakini mtu anayetoka Kigoma…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kuchauka kwanza ukizungumza unatakiwa unitazame mimi, siyo Waziri, halafu pili muda wako umekwisha malizia.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa mwongozo wako, na ninaomba kuunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Mtaturu jiandae Mheshimiwa Stella, jiandae Mheshimiwa Nusrat.

**MHE. MIRAJI J. MTATURU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia hoja iliyoko mezani hotuba ya Wizara yetu ya TAMISEMI ambayo ndiyo Wizara mama inayobeba wananchi wengi katika nchi yetu kama ambavyo tumesema na ndiyo maana hata bajeti yake imefikia shilingi trilioni 11 ambayo ni fedha nyingi sana, ni karibia robo ya bajeti kuu ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii ni Wizara ambayo inagusa kila mahali. Tumesema ni Wizara ya huduma kwa sababu huduma nyingi zinazotolewa katika nchi zinasimamiwa na Wizara hii. Kwa hiyo, naomba nitumie nafasi hii kwanza kabisa kumshukuru na kumpongeza sana Mheshimiwa Rais, Daktari Samia Suluhu Hassan, ndio mwenye hii Wizara ambaye anasaidiwa na ndugu yangu kaka yangu Mheshimiwa Mohamed Mchengerwa ambaye ni Waziri wa Nchi, anafanya kazi nzuri sana kumsaidia Mheshimiwa Rais. Kwa hakika, tunakuona namna ambavyo unapambana kuhakikisha kwamba maendeleo ya wananchi wetu yanapatikana na huduma zinafika kule zilikostahili. Nikisema nakupongeza wewe Mheshimiwa Waziri, ni pamoja na Manaibu wako, Daktari Dugange pamoja na Dada yangu Mheshimiwa Zainab Katimba mkisaidiwa na Katibu Mkuu pamoja na watumishi wote wa Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaposema Wizara hii ya TAMISEMI, lazima nimtaje Mkuu wa Mkoa wetu wa Singida, dada yetu Mheshimiwa Halima Dendego, anafanya kazi nzuri sana. Toka amekuja Singida, tunaona Mkoa wetu unapaa na ndiyo

maana mnaleta shughuli mbalimbali katika Mkoa wetu. Mwaka huu tutakuwa na wafanyakazi Sikukuu ya Mei Mosi, tunawakaribisha sana Singida tuje tusherehekee kwa pamoja siku ya wafanyakazi duniani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza na kumshukuru Mheshimiwa Thomas Apson ambaye ni Mkuu wetu wa Wilaya, anafanya kazi nzuri, anasikiliza kero za wananchi kila Alhamis, anaita Kliniki ya Kusikiliza Kero. Ni kazi kubwa anaifanya kwa ajili ya kusikiliza wananchi wetu ili kuondokana na kero. Pia nampongeza na kumshukuru *DAS* wetu ndugu yetu Rashid pamoja na Mkurugenzi mpya Ndugu Msigala ambaye amekuja hivi karibuni wanafanya kazi nzuri ya kuisaidia Halmashauri yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeanza na shukrani kwa sababu suala la shukrani ni lile jambo la kimungu. Tunasikia watu wengi wanaongelea habari ya kwamba sisi tunashukuru, naomba wasituletee tabia mpya ambazo siyo zetu. Tabia zetu sisi hata tunakua na wazazi wetu, unaambiwa ukimaliza kula chakula unamshukuru baba kwa chakula, unamshukuru mama kwa chakula, unamshukuru na dada aliyepika.

Mheshimiwa Naibu Spika, maana yake ni kwamba tulifundishwa toka udogo wetu kushukuru ni jambo kubwa sana kwa sababu ni tabia njema, na kushukuru ni uungwana. Kwa hiyo, lazima tuwe waungwana katika Taifa letu. Hao wanaosema sisi tunashukuru, tutaendelea kushukuru kwa sababu ni jambo la kiungwana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama haitoshi, jambo hili hata kwenye Quran na Biblia imeandikwa, eeh Mwenyezi Mungu, anasema katika Quran, "mkinishukuru nitawazidishia." Maana yake ni kwamba wanaoshukuru wanazidishiwa kwa Mwenyezi Mungu. Kama haitoshi, kwenye Biblia imesema, "moyo usio na shukrani, hukausha mema yote." *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maneno hayo, kwa hiyo, maana yake siyo dhambi kushukuru na tutaendelea

kushukuru kwa sababu sisi ni waungwana na Mheshimiwa Mzee Mkapa aliwahi kusema kushukuru ni kuomba tena. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maneno haya, baada ya kuwa nimeshukuru, naomba nieleze maeneo machache ambayo naweza kupongeza kwa maana ya afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Halmashauri yetu ya Ikungi tumepata fedha nyingi sana zinazohusiana na afya. Tulikuwa hatuna hospitali ya wilaya, sasa hospitali ya wilaya imekamilika. Tulikuwa na changamoto ya karibia shilingi 1,300,000,000/=, tumeshaletewa sasa tumemaliza jengo lile la mama na mtoto, tumejenga wodi za wanaume, akina mama na watoto, tumeweza kujenga hata jengo la mochwari kupumzisha wenzetu ambao wametangulia mbele ya haki wakati tunasubiri kuwahifadhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, hilo ni jambo la kibinadamu ambalo umetufanya. Kwa hakika tunashukuru sana Wizara kwa kuratibu jambo hili na leo hii. Tunaendelea kuomba kwamba tuendelee kukamilisha majengo machache yaliyobaki kwa sababu hata ile *standby generator* sasa hivi inafanya kazi, kwa maana hiyo, upasuaji unafanyika vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama haitoshi, tumepata zahanati na vituo vya afya. Kituo cha afya pale Ntutu tumekipata. Shilingi milioni zaidi ya 500 tayari tumejenga na umbali ule karibia kilomita 200, huduma zinaanza kutolewa. Kwenye eneo hili naomba sana, tulishauliza swali mara tatu, tumalize kile kituo cha afya kwenye jengo la mama na mtoto, vifaa viko tayari, vinasubiri karibia shilingi milioni 40 tu tumalizie vitu vidogo vidogo ili Kituo cha Afya cha Ntutu kianze na tukafanye sherehe pale. Wananchi wa Ntutu wanasubiri kwa hamu jambo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tumejenga zahanati tatu Ighuka, Msule pamoja na Samaka. Zahanati zile ziko kwenye hatua za umaliziaji ili huduma ziendelee kuanza, na kwa hakika tukizikamilisha hizi tutapunguza kero za wananchi upande wa afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama haitoshi, nikumbushe tu Kituo kile cha Mkakati wamesema Waheshimiwa wengi, mimi nilielekeza pale Misughaa, naomba kituo cha mkakati kianze kujengwa hata kama ni fedha zikiingia mwisho wa mwezi huu wananchi wale watafurahi wa Misughaa wanakisubiri kwa hamu kile kituo cha mkakati ambacho Mbunge wao nilipendekeza kijengwe pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Katibu Mkuu wa chama chetu, alipokuja Daktari Nchimbi baada ya ombi langu pale Isuna, alikubali tujengewe kituo cha afya. Naomba hilo Mheshimiwa Waziri nalo alibebe kwa sababu alisema kabla ya uchaguzi tutaweza kujengewa kituo cha afya pale Isuna kwa sababu ni Kata kubwa ambayo ina wananchi wengi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napongeza vifaatiba, tumepokea madawa ya kutosha, tunaendelea kuomba eneo la wazee liendelee kuboreshwa kama Mheshimiwa Waziri ulivyosema kwenye eneo lako tuhakikishe wale wazee wetu ambao walifanya kazi kubwa waendelee kupata matibabu kama ambavyo inafanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishukuru sana Serikali kwa kuunga mkono sekta binafsi, katika hospitali yetu ya Makiungu Misheni, iliboreshwa na sasa hivi ilitakiwa iwe hospitali ya rufaa, tayari imeshapata kibali, ni hospitali ya rufaa, huduma zote zinatolewa na ni hospitali nzuri sana inashirikiana na Serikali katika kutoa huduma za afya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza sana *Father* Alessandro ambaye ndiye anasimamia hospitali ile kupitia wenzetu wa *RC* ambao wanafanya vizuri sana kwenye eneo la afya. Kwa hiyo, eneo hili nalo wameleta shukrani nyingi kwa Serikali kwa kuwasaidia jambo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili ni la elimu. Elimu ni msingi wa maendeleo, tunaona namna ambavyo imeboreshwa. Katika maeneo haya, tumepata vyumba vya madarasa, tumepata

maabara na pia, tumejenga shule mpya za msingi 13 katika maeneo mbalimbali ambayo yalikuwa yanachangamoto ya umbali. Katika hizo shule chache Sindikwa, Taru Mlimani, Mbwanjiki, Mao, Mbonkatika na Mtaturu Shule ya Msingi imejengwa pale katika Shule ya Ikungi. Nalo hili ni jambo zuri limefanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tumejenga sekondari tatu. Sekondari ya Matongo imeanza kufanya kazi, Sekondari ya Nkui Mtaturu nayo iko tayari inaendelea kutoa huduma, lakini tumeongezewa majengo, kwa ajili ya Kidato cha Tano na cha Sita.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana, kwenye shule zile chakavu, naomba sana tuweze kujengewa. Tuweze kupata ukarabati Kinyamwandio, Mahambe, Dung'unyi, Mwau pamoja na Kikio. Tusaidiwe kupata ukarabati Choda, Mkiwa, Sambaru pamoja na Shule ya Msingi Msule, ambayo imekuwa ni ya muda mrefu tuweze kupatiwa fedha za ukarabati ili zile zianze kurudi kwenye hali ya kawaida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, zaidi niendelee kuomba sana eneo hili la barabara. Barabara zimekuwa zinachongwa sana na katika muda huu mfupi uliopita tumepata changamoto ya mvua nyingi. Tunaomba sana, pamoja na kazi nzuri inayofanyika tuombe tuweze kujengewa madaraja katika maeneo ambayo yana changamoto kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pale daraja la Matongo – Ntuntu – Misughaa – Ighuka – Ikuwa, Barabara ya Kikio – Nakimbwi. Pale Kimbwi ilikatika kabisa, mawasiliano hamna kati ya wilayani na kwenda Hospitali ya Makiungu. Naomba sana madaraja hayo, Nilishamletea Mheshimiwa Waziri anisaidie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho ni mambo matatu; ajira naomba ziongezwe kwa ajili ya elimu na afya, nyumba za walimu na hosteli.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, naomba sana viongozi wetu wa vijiji waweze kupata posho za vijiji, kwa maana ya uongozi wao ili waweze kufanya kazi inavyotakiwa. Baada ya maneno haya, naunga mkono kwa asilimia mia moja, ili tuweze kutekeleza bajeti ya wananchi, ambayo Mheshimiwa Rais anafanya kazi nzuri. Mungu awabariki sana, ahsanteni sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Stella, jiandae Mheshimiwa Nusrat.

**MHE. STELLA S. FIYAO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi, ili nami niweze kuchangia katika Wizara hii muhimu ya TAMISEMI, Wizara ambayo imebeba mambo mengi sana, kwa ajili ya maendeleo ya Taifa letu na ni ya msingi mno. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimefuatilia sana mjadala kuanzia kwenye Wizara ya Waziri Mkuu na pia, tunakuja TAMISEMI. Naona namna Wabunge wengi ambavyo wanazungumza kwamba, Rais Samia anastahili pongezi kwa namna yoyote ile. Naomba niwatoe hofu Wabunge waliomo humu ndani na umma wa Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, umma wa Watanzania unatambua jitihada kubwa ambazo Mheshimiwa Rais anazifanya ndani ya nchi yetu. Kila mwananchi mwenye akili timamu anampongeza Rais kwa sababu amefanya mambo makubwa ambayo hayaelezeki. Tukianza kuyaeleza hapa, hatuwezi kumaliza leo, lakini ukweli ni kwamba, Mheshimiwa Rais anastahili pongezi kwa namna yoyote ile na mwananchi yeyote yule, ilimradi ni Mtanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mambo aliyofanya Mheshimiwa Rais ni makubwa sana. Jambo la kwanza, Mheshimiwa Rais ametufundisha kwamba, uongozi siyo kelele, ni vitendo. Hili tumeliona kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili, Rais ametufundisha kwamba, kumbe Watanzania tunaweza kuishi kama ndugu bila kujali itikadi za vyama vyetu wala dini zetu. Jambo hili, Mheshimiwa Rais, ametufundisha kwa vitendo, tumeona na ni lazima tuseme, Watanzania wanasema mnyonge mnyongeni haki yake mpeni, lakini hatumnyongi, tutasema ukweli, mambo aliyoyafanya Mheshimiwa Rais yanastahili pongezi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukisoma Biblia, uko wakati Yohana aliwatuma wanafunzi wake alipokuwa gerezani, waende wakamwulize Yesu baada ya kuona mambo makubwa ambayo anayafanya. Akawaambia nendeni mkamwulize Yesu kwamba, wewe ndiye au tusubiri ajaye?

Mheshimiwa Naibu Spika, Yesu hakuwa na maneno mengi ya kuwaambia wanafunzi wa Yohana. Alichowajibu, akawaambia, vipofu wanaona, viwete wanatembea, viziwi wanasikia. Hayo yalikuwa ni majibu tosha ya Yesu kuwajibu wanafunzi wa Yohana; na wanafunzi wa Yohana wakajua huyu ndiye. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukweli ni kwamba, mambo ambayo tunaendelea kuyaona ni wazi kabisa kwamba, Rais Samia Suluhu Hassan anastahili kuendelea kutuongoza ndani ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, jambo la pili, amelinda heshima ya wanawake. Ninyi wote ni mashahidi, sisi wanawake 19 tumeitwa majina mabaya, mpaka tukaitwa *Covid-19,* lakini Rais aliposimama kwenye Sherehe ya Wanawake, Siku ya Machi 8, 2023 alikanusha akasema wazi kwamba, *COVID* ni ugonjwa, lakini sisi tumeitwa majina haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuonyesha uzalendo na kulinda heshima ya mwanamke, Rais ameweza kulinda heshima yetu. Sisi wanawake tuna sababu ya kumpa pongezi. Niseme wazi kabisa, mimi kuna wakati naona CCM kwenda kutangaza kwamba jina liwe moja, kama ni muziki ulioanzwa na wanawake wa upinzani siku ya tarehe 8 Machi, 2023. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2023 Wanawake wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) walisimama wao wenyewe wakiwa na akili timamu na wakatoa tuzo ya uongozi bora kwa Rais Samia Suluhu Hassan. Ilikuwa inaudhihirishia umma kwamba, Rais sio wa mchezo mchezo, ana uwezo mkubwa wa kuongoza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna wakati ni lazima tuseme ukweli bila kumung'unya maneno, Tusifike mahali tukajitoa ufahamu, inapofikia masuala ya uchaguzi, tuongee ukweli, maana Biblia inasema msema kweli ni mpenzi wa Mungu. Ni lazima tuseme ukweli bila kuogopa jamii inasemaje, lazima tumtie moyo Rais. Kazi anazozifanya zinaonwa na umma wa Watanzania, amejitahidi kwa kadiri awezavyo kuhakikisha anayagusa makundi mbalimbali; amehakikisha kwa kadiri awezavyo kuhakikisha anawagusa wanawake vijana, walemavu, wazee na watu wa aina zote. Ni lazima tufike mahali tuuseme ukweli, maana ukweli humfanya mtu kuwa huru. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili, naomba nimpongeze pia Mheshimiwa Waziri Mkuu, amekuwa mstari wa mbele kuhakikisha nchi inakaa kwenye utulivu. Tusiposema haya, tutakuwa hatujamtendea haki. Tumpe maua yake, amekuwa akituthamini pasipo kujali tofauti za vyama vyetu, ametuunganisha, naye anastahili pongezi kwa namna yoyote ile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la tatu, nikupongeze Mheshimiwa Waziri Mchengerwa pamoja na timu yako. Wizara ya TAMISEMI imetulia sasa. Huko kwenye maeneo yetu kumetulia, kazi mnayoifanya siyo ya kitoto, inaonekana, mnastahili pongezi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia, nami nitumie nafasi hii kumpongeza Mkuu wa Mkoa Wangu, Mheshimiwa Chongolo, ametuunganisha Wanasongwe bila kujali tofauti za vyama vyetu. Tunasimama mahali popote na tunasema kwa sababu, ametubeba na kutufanya kuwa watoto wa mama mmoja, anastahili pongezi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba niende moja kwa moja kwenye mambo ya msingi. Pamoja na pongezi nilizozitoa, haimaanishi kwamba, Rais amekamilika kwenye kila sekta, kuna maeneo bado mambo hayajakamilika, ni lazima tuombe Serikali iweze kuyafanya tena. Naomba nizungumzie kwenye suala la hospitali iliyoko Kata ya Itumba, Wilaya ya Ileje, Hospitali ya Wilaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye hospitali hii, nimesema na nitasema tena, niiombe Serikali. Mheshimiwa Waziri tunaomba utusaidie kwenye hii Hospitali ya Wilaya ya Ileje kujenga *fence* ambayo itatenganisha makazi ya watu na eneo la hospitali kwa sababu, jambo hili kwanza ni hatari, hospitali haina *fence*, anaweza kuingia kichaa akafanya uharibifu hata kwa wagonjwa. Tunaomba mwone umuhimu wa kujenga *fence* kwenye Hospitali ya Wilaya ya Ileje, ili kutengeneza mazingira yawe safi, salama na kutenganisha maeneo ya hospitali na maeneo ya wananchi, hii inaweza ikatusaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili, naomba pajengwe kichomea taka kinachoendana na hadhi ya Hospitali ya Wilaya ndani ya Hospitali yetu ya Wilaya ya Ileje. Kichomea taka kilichopo kilijengwa wakati hospitali ikiwa kituo cha afya, lakini sasa hospitali imepandishwa hadhi na kuwa Hospitali ya Wilaya. Hivyo, kichomea taka kilichopo hakikidhi mahitaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pajengwe kichomea taka ambacho kitaendana na hadhi ya Hospitali ya Wilaya kwenye eneo hili, ili kuepusha changamoto za kiafya kwa watumishi wa hospitali, wagongwa na wananchi waliozunguka hospitali hii. Hili litatusaidia sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili kwa Mheshimiwa Waziri nilikuwa naomba, sisi pia tuna changamoto kwenye eneo la *TARURA*, kwenye eneo la madaraja. Jambo la kwanza ni daraja ambalo linapita katika Mto Mafumbo, daraja hili linaunganisha kata mbili, Kata ya Myale na Kata ya Ndola, kwa maana ya Kijiji cha Ibezya na Kijiji cha Mlale.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mheshimiwa Waziri, daraja hili lijengwe ili wananchi wetu waweze kunufaika kwa sababu, mwisho wa siku wananchi wanaenda umbali mrefu kutafuta njia wakati daraja hili likijengwa litarahisisha mawasiliano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la tatu, kuna daraja ambalo linapita katika Mto Isenga. Daraja hili linaunganisha wilaya mbili, Wilaya ya Mbozi kwa maana ya Kijiji cha Namwangwa na Wilaya ya Ileje, kwa maana ya Kijiji cha Ilanga. Daraja hili limekatika, limebomoka zaidi ya miaka kumi iliyopita, na kwa bahati mbaya limeweza kupoteza maisha ya wananchi zaidi ya watatu, wamekufa pale kutokana na changamoto inayokuwepo kipindi cha mvua.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri tunaomba daraja hili liweze kuchukuliwa kwa uzito wake lijengwe na mwisho wa siku tunusuru hatari ambazo zinatokea kwa wananchi wetu, ikiwa ni pamoja na kupoteza maisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini jambo la tatu, iko shule ambayo inaitwa Shule ya Msingi Ilanga…

*(Hapa kengele ililia kuaashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Malizia.

**MHE. STELLA S. FIYAO:** Mheshimiwa Naibu Spika, sawa nashukuru.

Mheshimiwa Naibu Spika, iko shule inaitwa Shule ya Msingi Ilanga. Shule hii ipo katika Kata ya Mlale imeezuliwa mwaka huu yakabaki madarasa matatu tu. Hayo madarasa wanasoma wanafunzi kuanzia awali mpaka darasa la saba. Wananchi wamejitahidi kadiri wawezavyo, wamechimba msingi, wamekusanya mawe, wameweka mchanga pale, hebu tuombe Serikali mtusaidie kwenye hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, shule hii iangalieni, ikiwezekana, kama mna mfuko wa dharura nendeni, pelekeni pale, shule hii iweze kujengwa kwa sababu, mwisho wa siku madarasa matatu kutumika na wanafunzi kutoka awali mpaka darasa la saba ni hatari, tunadhoofisha masuala ya ufaulu kwa wanafunzi wetu. Serikali chukulieni jambo hili kwa uzito, wananchi hawa waweze kujengewa majengo na wanafunzi waendelee kusoma kama ilivyo ada. Mungu awabariki sana, nashukuru. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Nusrat.

**MHE. NUSRAT S. HANJE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia Hotuba ya Bajeti ya Ofisi ya Rais – TAMISEMI. Kwanza naomba niwapongeze sana Mheshimiwa Waziri na timu yako; Naibu Mawaziri, Mheshimiwa Dkt. Festo Dugange na Mheshimiwa Zainab Katimba, pamoja na Watendaji wote wa Wizara. Tunawapongeza sana, mnafanyakazi nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, kwa nukta hii nimpongeze na nimshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa sababu, kuna namna amefanya tuone kwamba Ofisi au Wizara ya TAMISEMI ndiyo ambayo kimsingi inahusika na maisha ya Watanzania, kwa sababu, ukizungumza TAMISEMI ndiyo Tawala za Mikoa, ambapo kuna Watanzania wanaishi huko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kitendo cha kwamba, amewaweka watu ambao nafikiri anawaamini zaidi katika kazi, kwenye Wizara hii, inaonesha ni kwa namna gani Mheshimiwa Rais anawajali Watanzania. Ndiyo maana amewapa watu anaowaamini sana Wizara hii, ili wafanye kazi na kweli wanafanya kazi na amekuwa akisema hivyo mwenyewe hadharani mara kadhaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia nimpongeze Mkuu wa Mkoa wangu, mama yetu Mheshimiwa Halima Dendego, anafanya kazi nzuri. Huyo mama ni mtu wa kazi kweli kweli, yaani unaona namna ambavyo anajitoa. Mheshimiwa Dendego yaani anaweza akakupa kazi na akakufuatilia huko huko

ukakutananaye sehemu aliyokutuma kazi. Kwa hiyo, nampongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, nampongeza sana Mheshimiwa *DC* wetu wa Wilaya ya Ikungi, *DAS* pamoja na watu wanaomsadia. Kuna Mkurugenzi wa zamani, Justice Kijazi, ameondoka juzi juzi, lakini kuna Mkurugenzi mpya amekuja, Mheshimiwa Kastory Msigala, nao wanafanya kazi pale. Vile vile Baraza la Madiwani pamoja na Madiwani wa Kata zote za Wilaya ya Ikungi, wilaya ambayo mimi natoka, nawapongeza sana, wanafanya kazi nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upekee sana, nampongeza Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi wa Wilaya ya Ikungi, Mheshimiwa Michael Kapakapa. Namtaja huyu kwa upekee, unajua kuna wakati mwingine, kwanza nchi yetu ikumbuke inatekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi na wakati mwingine kuna watu wanafanya kazi na hawaonekani. Yule mzee anakimbia, yaani anakimbizana na watu wa Serikali kuhakikisha kwamba ilani inatekelezwa. Naomba hili jambo lieleweke kwa umakini wake kwa namna ilivyo. Najua, na kuna maeneo mengine wanafanya kazi na inawezekana shukrani hizi na pongezi pia ziende kwao.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawapongeza Madiwani pamoja na Mwenyekiti wa Halmashauri ambao nao wanafanya kazi kubwa kwa upande wao. Sisi Wilaya ya Ikungi, sana sana Singida Mashariki, tunaishukuru sana Serikali, Mheshimiwa Waziri naomba utufikishie salamu kwa Mheshimiwa Rais kwa sababu, tangu mwaka 2020/2022 mpaka 2024/2025, wamepeleka takribani shilingi 12,741,000,000. Ni fedha zilizokwenda kutekeleza miradi ya maendeleo, ambayo inamgusa mwananchi moja kwa moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, fedha hizi zimepelekwa katika ujenzi wa Hospitali ya Wilaya ya Ikungi, ujenzi wa shule tatu mpya za sekondari na shule za msingi mpya mbili. Ujenzi wa vyumba vya madarasa kwa wanafunzi wetu pale, maabara, vyoo, nyumba za watumishi, majengo ya utawala, mabweni na mabwalo ya

wanafunzi. Kwa hiyo, tunaomba utufikishie salamu zetu. Watu wa Ikungi tunashukuru sana na sisi tutakuja kumlipa huko mbele, mtakuja kuona baadaye. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Wanyaturu wanasema, *intulilihendika vijeruhe ndiyo anang'honjo*. Yaani maana yake ni jambo ili lifanyike vizuri, jambo linalofanyika vizuri linafanywa na wenye shughuli yao. Kwa hiyo, sisi watu wa Ikungi tuna shughuli yetu, hapo mbele kidogo mtakuja kuona kwa sababu, kuna namna kuna sehemu tulikuwa tumekwama huko nyuma, lakini sasa hivi mambo yanaenda na yanaonekana na maneno siyo mengi, tutayaona baadaye. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hayo, kuna changamoto kadhaa ambazo bado zipo. Kuna jambo moja ambalo hapa niseme, tumejengewa vyoo, lakini bado kwenye taarifa zetu huku za kwenye mawasilisho ya humu Bungeni, mapendekezo ya Kamati, michango ya Wabunge, bado tunazungumza vyoo. Yaani hakuna kitu kinakera kama mpaka leo bado tunazungumza ukosefu wa vyoo shuleni. Yaani sehemu ya mtu kujistiri, hapa penyewe kwenye jengo la Bunge kuna vyoo vingi kweli kweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa natamani Serikali ije na mwarobaini wa kudumu wa kutatua tatizo la upatikanaji wa matundu ya vyoo shuleni kulingana na mgawanyiko. Ndiyo maana tunazungumza na kupanga bajeti kwa mlengo wa kijinsia, kuangalia mahitaji, kwa sababu, huwezi kuweka vyoo sawasawa kulingana na watoto wa kike na watoto wakiume. Hata hivyo tu ambavyo ni vya muhimu, ni vichache, au havipo, havitoshi bado. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Shule ya Msingi Mahambe pale Unyati, Kata ya Unyati, kuna tatizo la vyoo na Shule ya Msingi Manjaru, iko Kata ya Isuna kuna tatizo la vyoo. Hizo nimezitaja chache kwa sababu ya muda. Kamati pia, imeshauri nami naungananao, hebu tuje na mkakati madhubuti ambao ni *crash,* wa *immediately*, tutafute namna ya kutibu tatizo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna jambo lingine, sisi tuna *CSR* pale Ikungi, kwenye Mgodi wa Shanta, lakini fedha zinazotengwa zipelekwe kwa kupitia *CSR* kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo haziendi. Yaani unakuta ya mwaka uliopita imekutana na ya mwaka huu. Saa nyingine kwa mfano, Mang'onyi pale, kuna Shule ya Sekondari ilitakiwa ijengwe, kwa ajili ya kutatua tatizo la wanafunzi kutembea umbali wa karibu kilomita 30 kwenda kufuata shule, watoto wanakaa kwenye mageto wanapata ujauzito.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa Baraza la Madiwani limepanga, limeona kwamba tupeleke hiyo shule, lakini fedha hazitoki, halijatekelezwa sasa. Nakuomba sana, hebu Serikali ipitie upya mwongozo wa utoaji wa *CSR* ili miradi ambayo ipo kwenye upande wa TAMISEMI, sasa hii ni *cross cutting,* najua *CSR* haihudumii TAMISEMI peke yake. Hebu mpitie upya *CSR,* ndugu zangu Watanzania wanategemea madini yao na rasilimali walizonazo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi watu wa pale tuna jembe na nyundo, hatuwezi kwenda kuchimba wenyewe madini, tumeweka mwekezaji. Sisi ndiyo wenye hiyo rasilimali, ndiyo tunaishi kwenye hilo eneo, hatuwezi kwenda wote kuchimba, tumeweka mwekezaji ndiyo maisha na utaratibu wa kiuchumi unavyoenda, lakini sisi basi tufaidike, ndiyo vitu kama hivi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, zahanati, vituo vya afya, shule za msingi, shule za sekondari, barabara ndiyo vitu tunavyotegemea tufaidike navyo kwa kuwepo na madini kwenye ardhi yetu, ikiwemo sisi watu wa Ikungi. Kwa hiyo, nawaomba sana mpitie upya mwongozo wa *CSR* ili tuone ni namna gani ambavyo pesa inatengwa, milolongo ipungue, wapewe pesa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ni Wizara ya TAMISEMI inahusiana na suala la adhabu kali za watoto shuleni ndugu zangu. Watoto wetu wanapigwa na mateke. Tunawapenda walimu, tunawapongeza wanafanya kazi kubwa, lakini adhabu zinazotolewa kwa watoto, kwenye mitandao tumeona mara nyingi tu watoto wanaripotiwa wamepigwa na

nyaya, wamepigwa mateke, mtu anapigana na mwanafunzi kama anapigana na mtu mzima mwenzake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kwa sababu, tunatekeleza Mwongozo wa Adhabu Shuleni kwa Mwongozo ule wa Mwaka 2022, hebu Wizara uiteni huo Mwongozo, upitieni upya. Mimi pia ni Mwalimu, kuna namna nyingi za kumwadabisha mwanafunzi, badala ya kumwadhibu mpaka unamfanyia ukatili wa kijinsia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tuwape watoto adhabu ambazo zitawa-*discipline,* siyo kuwadhuru kwa sababu, kuna wengine mpaka wanaacha shule kabisa. *Dropout* nyingi zinasababishwa na walimu wengine ambao ni wakali. Kuna wengine mpaka walikuwa wanapewa majina ambayo unajua kabisa akitajwa huyo shughuli ipo huko shule. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, jambo lingine la kumalizia, kuna jambo la *school feeding program*. Ndugu zangu, hapa Bungeni tulivyo, hapo nje kuna *canteen*. Hapa watu wote tumekula, labda ambaye amefunga ana *program* nyingine. Watoto wetu wanakaa shuleni hawali, hakuna utaratibu mzuri wa watoto kupata chakula shuleni.

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri, kama ambavyo wanasema, wewe ni mtu kazi, hebu katika mambo ambayo utapanga kuyatatua, tatua hili ambalo linahusiana na watoto kula shuleni. Shirikiana na Mheshimiwa Bashe kwenye kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi kweli tunashindwa kulima? Watoto walime, mbona zamani shule zile kubwa; Ilboru, Weruweru, watoto walikuwa wanalima?

Mheshimiwa Naibu Spika, yaani shule inakodi trekta, wanalima, watoto wanakuja kupalilia wenyewe. Tuna *SIDO,* hebu *SIDO* itusaidie kutu-*inform,* yaani zi-*inform* matatizo yetu ni pamoja na haya. *SIDO* tutengeneze vifaa ambavyo vitasaidia kulima na kumwagilia shuleni. Hebu tumalize hili jambo, yaani ni kitu cha

ajabu sana, watoto wanashinda na njaa na ndiyo maana hata ufaulu unashuka kwa sababu hiyo.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Malizia.

**MHE. NUSRAT S. HANJE:** Mheshimiwa Naibu Spika, sasa niwakaribishe wote Singida, Mei Mosi. Karibuni sana Singida, Mei Mosi, tunawasubiri, pale kutakuwa kuna mambo yote mazuri, karibuni sana. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa, niwashukuru sana kwa michango. Wachangiaji wetu wote wamemalizika, lakini vilevile nimshukuru Mheshimiwa Waziri na timu yake pamoja na watalamu wenu, Katibu Mkuu na Wakuu wa Idara mbalimbali kwa kazi nzuri mnazofanya. Bajeti hii ni bajeti kubwa sana na Mheshimiwa Rais ameiona, sababu ndiyo inagusa maisha ya Watanzania. Tuna Rais ambaye ni *result oriented,* Rais ambaye amezaliwa kuleta matokeo kwenye Taifa letu. Tunampongeza sana. *(Makofi)*

Sasa nina tangazo muhimu sana la mabadiliko ya ratiba. Siyo ratiba ya CCM kuchukua fomu, hii ni nyingine. Katibu wa Bunge, anaomba kuwatangazia Waheshimiwa Wabunge kuwa, yamefanyika marekebisho madogo ya Ratiba ya Mkutano wa Kumi na Tisa wa Bunge unaoendelea.

Sasa Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari itawasilisha bajeti yake Tarehe 16 Mei, 2025; na Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa itawasilisha bajeti yake Tarehe 20 Mei, 2025. Ratiba yenye mabadiliko itatumwa kwenye vishikwambi vyenu hivi punde. *(Makofi)*

Baada ya maneno hayo, naahirisha Shughuli za Bunge mpaka tarehe 22/4/2025, saa 3.00 asubuhi.

*(Saa 8.00 Mchana Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Jumanne, Tarehe 22 Aprili, 2025, Saa Tatu Asubuhi)*